# Nipashe

Jumatatu Novemba 21, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581136

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US





UKURASA 13


JACKPOT BABA LAO!

TZS. 407,110,340

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#




RIPOTI MAALUM: **Kijiji** chenye wakazi wasiojua maji ya bomba

UKURASA 4



# Mtikisiko biashara ya kuku nchini

UKURASA 2



Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye (kushoto), akimkabidhi Tuzo ya Mshindi wa Jumla Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna, katika hafla ya Tuzo za Mlipakodi Bora 2021/22 jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kulia ni Ofisa Mkuu wa Fedha NMB, Juma Kimori. **NA MPIGAPICHA WETU**

## YALIYOMO

UKURASA WA 5

**NMB MLIPAKODI MKUBWA ANAYEZINGATIA KANUNI BORA**

BENKI ya NMB imeibuka mshindi wa jumla katika Tuzo za Walipakodi za Mwaka 2022 wakati...

UKURASA WA 8

**HOJA 10 ZA WANANCHI ZIARA YA SAMIA MANYARA**

RAIS Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kuzuru mkoani Manyara juma hili, huku wenyeji...

## Akiri kuua kaka yake akidai alitaka kumlawiti

UKURASA 3



## Ripoti Shule ya Sheria: Walimu wahamishwe

UKURASA 2


MICHEZO | VIKOSI VYOTE KOMBE LA DUNIA QATAR UK.16 | KABWELA UK.7

# Kilio biashara ya kuku

Na Maulid Mmbaga

BAADHI ya wazalishaji wa vifaranga, wafugaji na wauzaji wa kuku wa nyama nchini wameiomba serikali kuongeza nguvu kuzuia mianya ya uingizwaji vifaranga kutoka nje ya nchi wanavyodai kwa sasa vimefurika sokoni.

Vilevile, wadau hao wa kuku wanadai kukata tamaa kuendelea kuzalisha vifaranga kutokana na idadi kubwa ya kuku walioko sokoni, hali inayoua uwekezaji na ustawi wao kiuchumi kutokana na kuporomoka kwa bei ya kuku huku bei ya chakula cha kuku ikizidi kupaa.

Mfugaji wa kuku na mkazi wa Gongo la Mboto jijini Dar es Salaam, Neema Elikunda jana kuwa kuku wamekuwa wengi sokoni, jambo lililoshusha bei ya kitoweo hicho akibainisha sasa wanauza kwa Sh. 6,500 hadi 5,000.

Alilalamika kuwa wakati bei ya kuku inashuka, bei ya chakula inazidi kupanda, hivyo kuwa mzigo kwa wafugaji wengi.

Elikunda alisema chakula cha kawaida mfuko wa kilo 50 sasa unauzwa Sh. 88,000 na cha kukuzia ni Sh. 85,000.

"Mwezi uliopita nilinunua vifaranga 500 lakini hadi sasa zaidi ya 190 wako bandani, hakuna soko, tunatumia gharama kubwa kuwakuza lakini mtu anakuja kuku mkubwa anataka anunue kwa Sh. 5,000 ukikataa anaondoka.

"Kama serikali haitodhibiti vifaranga kutoka nje, wazalishaji wa ndani watazidi kuumia, wanaototolesha kwa sasa wanashindwa kutokana na bei, hawa ni wawekezaji nchini, wanalipa kodi zote muhimu lakini sasa wanauza kwa hasara, hata serikali inapata hasara," alisema.

Mfugaji mwingine, Allan Massawe alisema uingizaji holela wa vifaranga nchini unachangia kuleta mlipuko wa magonjwa ya kuku.

Pia alisema kutokana na vifaranga hivyo kusafiri kwa muda mrefu vinakuwa dhaifu na mfugaji anapovinunua, akianza kufuga vinakufa na hivyo kupata hasara.

"Nilikuwa ninafuga vifaranga 2,000 mpaka 3,000 lakini kwa sasa nimepunguza hadi 300, hii hali inayoendelea itasababisha baada ya muda kuwe na shida ya kuku nchini, serikali iweke utaratibu maalum waagizaji wawe ni kampuni zilizosajiliwa na isiwe mtu binafsi, na kampuni hizo ziwe zinaingiza kiwango maalum ambacho hakiathiri wazalishaji wa ndani, kuacha hivi ni kuua soko la ndani," alisema.

Mwakilishi wa Kampuni ya Organia Ltd inayojishughulisha na sekta hiyo, alisema wanasikia uchungu na hasira kutokana na kinachoendelea katika biashara hiyo.

"Tutaendelea kuwasaidia wakulima na mawakala wetu wote, hasa katika nyakati hizi ngumu. Tutahakikisha kwamba sauti zako zinasikika na katika ngazi za juu zaidi nchini. Tunashirikiana na idadi kubwa ya wadau," alisema.

Mfugaji Flora Kamote, mkazi wa Bunju mkoani Dar es Salaam, alisema biashara ya kuku imekuwa mbaya kutokana na uingizaji holela wa vifaranga kutoka nje.

"Kuna vifaranga kutoka Uganda, Kenya na Malawi, na watu sasa wanauza hadharani. Mwanzoni walikuwa wanajificha kwa kubadilisha maboksi ya kubebea, lakini sasa wako wengi na ukimuuliza anakwambia 'nina kibali' na anakuonyesha, tunajiuliza kibali hicho kakitoa wapi ilhali zilizoruhusiwa ni kampuni mbili?" alihoji Flora.



Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji wa Kuku wa Nyama (TABROFA), Aloyce Makoye, alisema wafugaji wanapata hasara kwa sasa kutokana na kupanda kwa bei ya chakula na soko kufurika vifaranga kutoka nje.

Makoye ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika wa Wafugaji Kuku Kinondoni, alisema anapofuga huuza na kununua kutoka kwa wafugaji wengine lakini kwa sasa ameacha kwa sababu hakuna faida.

"Nilikuwa ninanunua kuku Sh. 6,000 hadi 6,500 halafu ninauza hadi kwa Sh. 7,000 lakini kwa sasa hupati faida maana kuku anauzwa Sh. 5,000 hadi 5,500. Pia hali ni ngumu kiuchumi, watu hawanunui sana kuku.

"Tulikutana na Naibu Waziri tukamweleza kilio chetu kuhusu soko kujaa vifaranga kutoka nje, aliahidi kufanyia kazi lakini hali imezidi kuwa ngumu, tunaiomba serikali ilinde watu wake, kuna watu wamewekeza kuuza vifaranga watauza wapi ikiwa vya nje vinashushwa bei?" Alihoji.

**KAULI SERIKALINI**

Akizungumzia malalamiko hayo, Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo, Prof. Hezron Nonga, aliiambia Nipashe wizara haijatoa vibali vipya vya uingizaji wa vifaranga nchini.

Prof. Nonga ambaye ndiye mtoaji wa vibali vya kuingiza mifugo ikiwamo vifaranga, alisema hadi sasa kampuni zinazoingiza vifaranga ni mbili ambazo ni Wolowolo Animal Care Center na The One Agro Enterprise ambazo zilipata vibali kuanzia mwaka jana na kwamba vifaranga vinavyoingizwa ni katika kumalizia maombi yao ya zamani.

"Hizi kampuni ziliomba vibali katika kipindi ambacho nchi ilikuwa na changamoto ya uhaba wa vifaranga ambapo The One Agro Enterprise imeruhusiwa kuingiza vifanga 494,000 kutoka Uganda na Wolowolo vifaranga 150,000 kutoka Malawi na mwisho wa kuingiza ni Januari 15, 2023," alibainisha.

Mkurugenzi huyo alisema kushuka kwa bei ya kuku katika soko kunatokana na kipindi husika na hali ya uchumi, akieleza kuwa matarajio yao Desemba mwaka huu biashara itakuwa nzuri.

Alisema serikali iko macho kufuatilia watu wanaoingiza vifaranga kwa njia za panya ili kulinda wazalishaji wa ndani, akisisitiza kampuni za uzalishaji wa vifaranga kuzingatia ubora ili kuchochea ushindani katika soko.

# Ripoti Shule ya Sheria: Walimu wahamishwe

Na Elizabeth Zaya

KAMATI ya tathmini ya mafunzo yanayotolewa na Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania (LST), imesema haijapokea uthibitisho wa kutosha kutoka kwa wanafunzi na walalamikaji wengine kuhusu tatizo la kufeli kwa wingi wanafunzi wanaosomea mafunzo ya uanasheria.

Kamati hiyo iliyoongozwa na Mwenyekiti, Waziri mstaafu wa Sheria, Dk. Harisson Mwakyembe, ilipewa mwezi mmoja kukamilisha uchunguzi wake na jana iliwasilisha ripoti hiyo.

"Pamoja na wadau kuwasilisha malalamiko ya rushwa, uonevu au upendeleo katika utungaji au usahihishaji wa mitihani, hakuna ushahidi uliowasilishwa kuthibitisha tuhuma hizo," alisema.

"Hata hivyo, kwa kuzingatia unyeti wa taasisi na wajibu ilionao ambao unahitaji uadilifu wa hali ya juu wa taasisi ili uweze kufuatilia mienendo yao. Tuhuma zikiendelea, kamati inashauri wakufunzi wanaolalamikiwa wahamishiwe katika idara nyingine za serikali ili kulinda taswira ya taasisi."

Kamati hiyo ilibaini kasoro kwenye taasisi hiyo ni pamoja na kukosekana na huduma ya chakula katika eneo hilo, hosteli hususani kwa wanafunzi wanaotoka nje ya Dar es Salaam hali inayowafanya waishi maisha magumu.

Pia miundombinu chakavu ambayo haijafanyiwa ukarabati muda mrefu ikiwamo kutofanya kazi kwa kangavuke (generator), uchakavu wa viti vya kukalia, mifumo ya sauti katika kumbi za mihadhara kutokufanya kazi vizuri, kumbi za mikutano kuvuja, mifumo ya Tehama na viyoyozi kutokufanya kazi.

Mengine ni baadhi ya vyumba vya semina kutokuwa na vifaa vya kazi kwa vitendo kama vile vizimba vya kujifunzia vinavyochangia kuathiri mfumo mzima wa uendeshaji wa mafunzo ya uanasheria kwa vitendo.

Kutokuwapo kwa mahakama ya kufundishia kwa vitendo ili kuwezesha wanafunzi kujifunza kwa kushuhudia wenyewe mashauri yanayoendeshwa na mahakama, nyaraka zinazotegemewa na weledi katika kujenga hoja na utetezi.

Kuhusu malalamiko ya wanafunzi kwa Taasisi hiyo ya sheria nchini Dk. Mwakyembe alisema: "Kamati ililalamikiwa na wanafunzi kuwa LST kwa mujibu wa kanuni za rufani inatoa fursa kwa wanafunzi kukata rufani ndani ya siku 14 tangu kutangazwa kwa matokeo endapo hawakubaliani nayo, lakini wanafunzi wanadai kuwa fursa hiyo ni kiini macho kwa sababu mwanafunzi anaruhusiwa kukata rufani bila kuona karatasi yake ya mitihani iliyosahihishwa au bila kuelezwa swali gani alishindwa kujibu vizuri."

"Pili, mwanafunzi anaruhusiwa kukata rufani akilalamikia ukokotoaji wa alama za ufaulu bila kuona karatasi yake ya mitihani iliyosahihishwa. Wanafunzi walilalamikia utaratibu wa LST kukaa na mitihani iliyokwisha kufanyika kwa zaidi ya miezi saba bila kutoa majibu kwa wanafunzi na kuwafanya wasijue udhaifu na ubora wao na namna ya kujipanga."

"Walilalamikia mfumo wa utoaji matokeo kielektroniki kuwa unatoa matokeo yenye mkanganyiko, mathalani, kubadilika kwa alama za ufaulu na kusababisha taharuki kwa watahiniwa,"alisema na kuongeza:

"Kamati ilipokea malalamiko kuhusu kuwapo kwa mgongano wa kiutendaji ndani ya bodi ya uendeshaji wa taasisi katika kushughulikia rufani za wanafunzi. Bodi hiyo inathibitisha matokeo ya mitihani na majibu ya rufani kutoka kwenye kamati ya mafunzo na mitihani na wakati huohuo bodi hiyo inafanya kazi kama chombo cha mwisho cha maamuzi ya rufani."

Mwenyekiti huyo alisema kamati iliona msingi wa hoja hizo za wanafunzi za malalamiko na kushauri ufanyiwe marekebisho.

"Kamati imeuona msingi wa hoja wa malalamiko ya wanafunzi kuhusu mchakato wa rufani dhidi ya matokeo ya mitihani yanayolalamikiwa kwamba haujakaa vizuri kwani haumpi haki mlalamikaji kujua kwa uhakika msingi wa malalamiko yake.

"Vilevile kanuni za rufani tajwa hazilazimu taasisi kushughulikia rufani na kutoa majibu kwa mwanafunzi katika kipindi mahsusi. Kuhusu chombo kimoja ambacho ni bodi ya taasisi kuidhinisha taarifa za rufani na wakati huohuo kuwa chombo cha mwisho cha rufani, kamati nayo inauona mkwamo bayana wa uwajibikaji.

"Hivyo inashauri kanuni ziweke sharti litakalomtaka mwanafunzi wa somo ambalo ameshindwa, kuainisha maswali ambayo alishindwa na alama alizopata. Pili, kanuni ziainishe muda mahsusi wa kushughulikia rufani na kutoa matokeo kwa mlalamikaji na ziweke sharti kuwa matokeo ya mitihani yakitangazwa, michakato yote ikiwa ni pamoja na rufani za mitihani ziwe zimekamilika."

Kuhusu taasisi hiyo kukaa muda mrefu bila kusahihisha mitihani ya wanafunzi hao, Dk. Mwakyembe alisema: "Kamati haijaridhishwa na sababu za Taasisi na kushauri iondokane na utaratibu huo na imeshauri iimarishe mfumo wa Tehama ili kuondoa malalamiko. Pia ilishauri kutumia vitendo zaidi kuliko nadharia."

Kamati hiyo ilishauri kwamba umefika wakati kwa serikali kuunda kwa haraka Baraza la Elimu ya Sheria nchini, sekretarieti yake, ofisi zake na kuipa bajeti yake ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake yote yaliyoainishwa kisheri ikiwamo kushirikiana na TCU kupandisha vigezo vya ufaulu wa mitihani ya kidato cha sita na nne kwa watakaotaka kusoma sheria vyuo vikuu nchini.

Kamati hiyo iliundwa Oktoba 13, mwaka huu na Waziri wa Katiba na Sheria kwa ajili ya kufanya tathmini ya mafunzo yanayotolewa kufuatilia malalamiko ya wanafunzi kuwa kuna rushwa mbalimbali ikiwamo ya ngono na kufelisha wanafunzi bila sababu.

HABARI KITAIFA

# Akiri kumuua kaka yake akidai alitaka kumlawiti

**Na Grace Gurisha**

MKAZI wa Majohe, Dar es Salaam, Ramadhani Juma, amekiri kumuua kaka yake Fikiri Juma bila kukusudia baada ya kutokea ugomvi baina yao, mshtakiwa huyo akidai chanzo cha ugomvi ni kaka yake huyo kutaka kumlawiti.

Inadaiwa wakati ugomvi huo unaendelea, mshatakiwa alichukua chepe na kumpiga nalo kaka yake kichwani kabla ya kumchoma kisu tumboni, hivyo kusababisha kifo chake.

Ramadhani alikiri kosa hilo la mauaji mwishoni mwa wiki mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Susan Kihawa wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu baada ya kusomewa maelezo ya awali na Wakili wa Serikali, Esther Chale na kuyakubali yote.

Wakili Esther alidai Ramadhani na Fikiri ni ndugu waliokuwa wanaishi pamoja eneo la Majohe jijini Dar es Salaam na kabla ya tukio, mshtakiwa na kaka yake huyo walikuwa na ugomvi, Ramadhani akilalamika kwamba kaka yake Fikiri alitaka kumlawiti.

Alidai ndugu hao walishauriwa na mtu ambaye alitambulika kwa jina la Abdallah Seleman kuwa wanatakiwa kutengena, wasiishi pamoja tena na wote wakakubaliana na ushauri huo wa kutengana.

Hata hivyo, ilidaiwa mahakamani huko kwamba Januari 22, 2017, wakiwa nyumbani, ugomvi uliibuka tena, Fikiri (marehemu) alikuwa akimlalamikia mshtakiwa kwa kwanini amemsaliti.

"Wakati ugomvi huo unaendelea, mshtakiwa alimchukua chepe na kumpiga nalo marehemu kichwani kabla ya kumchoma kisu tumboni na baada ya hapo kilichotokea aliyepigwa alifariki dunia.

"Mshitakiwa alifungua mlango na kuanza kukimbia lakini alikamatwa na polisi jamii na kurudishwa eneo la tukio na wakati wanaingia ndani, walikuta mwili wa marehemu, kisu na chepe vikiwa na damu," alidai Wakili Esther.

Baada ya mshtakiwa kukiri kufanya mauaji hayo, Hakimu Kihawa alimwambia mahakama inaona ana hatia katika kosa la kuua bila kukusudia, huku Wakili Esther akidai hawana kumbukumbu za makosa ya nyuma ya mshtakiwa.

Wakili huyo aliomba mahakama itoe adhabu stahiki ili iwe funzo kwa mshtakiwa na kwa watu wengine kwa sababu kitendo kilichofanyika ni cha kukatisha uhai wa mtu.

Baada ya wakili huyo kuwasilisha ombi hilo, Wakili wa Mshtakiwa, Precious Hassan aliomba mteja wake aachiwe kwa masharti kwa sababu akiwa gerezani alilazwa hospitalini kutokana na maradhi ya figo zake kushindwa kufanya kazi na taarifa hizo Jeshi la Magereza linazo.

Pia alidai kuwa kwa miaka mitano na miezi 11, mshtakiwa alipokuwa mahabusu, alipata tatizo la afya ya akili na alipelekewa Hospitali ya Taifa Muhimbili na baadaye alipelekewa Dodoma kwa matibabu zaidi.

Hakimu Kihawa baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili, alisema adhabu ya mshtakiwa ataitoa Novemba 29, mwaka huu, huku akiagiza kuwa siku hiyo Jeshi la Magereza liwasilishe mahakamani huko vielelezo vya mshtakiwa kuwa alikuwa mgonjwa.




Waziri Mkuu na Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM Taifa, Kassim Majaliwa, akitoa salamu katika Mkutano Mkuu wa CCM wa Uchaguzi Mkoa wa Lindi kwenye ukumbi wa Chuo cha Ualimu Nachingwea mwishoni mwa wiki. **PICHA: OWM**

**SHERIA YA ARDHI NAMBA 4 YA MWAKA 1999**

**ILANI YA KUFUTWA JINA LA UMILIKI WA KIPANDE CHA ARDHI**

**MWOMBAJI: MARIA JOSEPH KASAMBALA NAMBA YA KIPANDE CHA ARDHI: TMK/CHB/ZBK5/253**
**JINA LILILOANDIKISHWA: COLLETHA SALUSTIAN MUTAYOBA**

Ilani inatolewa kwamba nakusudia kufuta jina la mmiliki wa Leseni ya Makazi iliyotolewa kwenye kipande cha ardhi kilichotajwa hapo juu kutokana na hukumu iliyotolewa na **"Mahakama Kuu ya Tanzania (Land Division) katika rufaa ya Ardhi No. 51 ya Mwaka 2015** na kuandikwa jina la **MARIA JOSEPH KASAMBALA".**

Utekelezaji utafanyika ndani ya siku 28 tangu tangazo hili kutolewa gazetini.

**E.R. PALLANGYO**
**MSAJILI MSAIDIZI WA NYARAKA**
**TEMEKE**

# ACT yashauri kikao mashauriano migogoro ardhi

**Na Mwandishi Wetu,** KILWA

KIONGOZI wa Chama cha ACT - Wazalendo, Zitto Kabwe, amewataka wenyeviti wa kamati ya usalama katika mikoa ya Ruvuma, Mtwara na Lindi, kuitisha vikao vya mashauriano baina yao na wawakilishi wa wakulima na wafugaji kwa ajili ya kujadiliana njia bora ya kutatua migogoro ya ardhi kabla hayajaleta maafa makubwa kwa taifa.

Alisema mbali na wawakilishi wa pande hizo mbili pia kikao hicho kihusishe taasisi na watu wasiokuwa na maslahi ya upande wowote na uamuzi utakaofikiwa hapo uheshimiwe na kila mmoja.

Zitto alitoa kauli hiyo jana akiwa katika siku yake ya mwisho ya ziara ya ujenzi wa chama katika Mkoa wa Lindi, alipotembelea kata za Mandawa, Kiranje Ranje na Kivinje Singino, katika Wilaya ya Kilwa.

Alisema katika mikoa yote mitatu kilio kikubwa cha wananchi ni migogoro ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji ilhali mikoa hiyo ina maeneo makubwa ambayo hayajatumika ipasavyo.

"Kuna haja ya watu kukaa pamoja, lakini ni jambo la kusikitisha kuona wanaolalamika ni wakulima zaidi sasa hawa nao wakichoka hakutakuwa na amani ni vyema wakakutanishwa waangalie njia bora ya kila mmoja kufanya shughuli zake bila kuingia katika maeneo ya mwingine," alisema Zitto.

Akizungumzia maendeleo ya gesi asilia katika maendeleo ya watu wa Lindi, Zitto alisema, ujio wa mradi mkubwa wa kusindika gesi asili kuwa kimiminika (LNG) ni muhimu ukawanufaisha wananchi wa maeneo husika kwa kuanza kuwaandaa kushiriki katika kila fursa itakayopatikana kupitia mradi huo.

"Kila hatua ya utekelezaji inapaswa kutazamwa kwa kiasi gani watu wataweza kunufaika mfano katika hatua ya sasa ya uthamini wa eneo la mradi wapo watu wamehamishwa na wengine watahamishwa baada ya mradi kuanza kutoka kwenye ardhi yao ya asili ili kupisha uwekezaji huu mkubwa, ni muhimu watu hawa wapate fidia sahihi," alisema.

Aliongeza kuwa hofu ya wananchi ni kubwa na kutolea mfano eneo la Likong'o wananchi wanalalamika kucheleweshewa fidia, huku utata wa zoezi lenyewe la uthamini ukidaiwa kuingiliwa na Halmashauri ya Lindi kwa kutaka kuwapunja malipo.

"Halmashauri isifanye udalali katika hili. Lakini, ufinyu wa fidia kwa kutozingatia uendelevu wa wananchi wenyewe, hasara za kuondolewa kwenye shughuli zao za uzalishaji mali na kujipatia vipato vya kujikimu uangaliwe," alisema Zitto.

Akizungumzia kadhia ya stakabadhi ghalani, Zitto alisema uzoefu wa miaka takribani 15 tangu mfumo huo uanze kutumika, inaonekana wazi mfumo umeanza kupoteza malengo na unatumika kumkandamiza mkulima badala ya kumsaidia kama ilivyotarajiwa.

Alisema serikali inapaswa kujua uamuzi wowote unaogusa maisha ya watu, wenyewe ndio wanaopaswa kuamua, sio kuburuzwa kama mifugo.

"Sisi ACT tumeshazungumza na Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe na Kamishna wa stakabadhi ghalani kwa kuwataka kushughulikia matatizo haya kwa haraka, pili, tunapendekeza kwa serikali iende kidigitali kwenye mfumo wa malipo ya mazao ya korosho ili iwe inawalipa wakulima papo kwa papo, yaani unauza ufuta au korosho zako unapata fedha yako hapo hapo. Mifumo ya kukopana ni ya kizamani na ya kinyonyaji," alisema Zitto.

**IN THE DISTRICT COURT OF KIGOMA**

**AT KIGOMA**
**CIVIC CASE No. 10 OF 2022**

**CHRISTINA CHARLES...............DECREE HOLDER**

(Arising from DC Civil Appeal No 25of 2022)
**ZAKARIA LAZARO.........JUDGEMENT DEBTOR**

**TO: ZAKARIA LAZARO**
**NOTICE OF DATE OF MENTION/HEARING**
**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for mention on 8th day of December, 2022 at 08:30 am before Hon. Hassan Momba , PRM
**YOU ARE** required to appear in this Court on the fixed date without fail.
**GIVEN UNDER MY HAND** and **SEAL** of the Court this…17…day of …November....2022

HASSAN MOMBA
PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA MOROGORO**

**SHAURI LA RUFAA YA JINAI NA. 27/2022**

**(Iliyotokana na Shauri la Jinai NA. 157/2022 katika mahakama ya Mwanzo Chamwino)**
**PHILIPHO ROBERT..........................................MRUFANI**

**DHIDI YA**

**JUMA SALUM HASSAN..................................MRUFANIWA**

**KWA: JUMA SALUM HASSAN**
**POPOTE ULIPO,**

Unafahamishwa kwamba mrufani katika shauri la Rufaa ya Jinai tajwa hapo juu, amefungua shauri la rufaa katika mahakama hii na sasa lipo katika hatua ya kutajwa. Hivyo shauri hilo limepangwa kutajwa tena mnamo tarehe 28/11/2022 saa 02:30 asubuhi na unatakiwa kuwepo, ili shauri hili liweze kuendelea dhidi yako kama sheria inavyoeleza.
**ZINGATIA KWAMBA,** kutokufika kwako tarehe hiyo, mahakama itaendelea na hatua inayofuata bila ya uwepo wako kwa kusikiliza shauri hili upande mmoja.
**IMETOLEWA,** na kutiwa sain na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 18 mwezi 11 mwaka 2022

HAKIMU MKAZI MFAWIDHI
MAHAKAMA YA WILAYA
MOROGORO

**ANATAFUTWA**



Ndugu **MOHAMMED ABDALAH MOHAMMED** pichani anatafutwa na polisi kwa tuhuma za kujihusisha na vitendo vya kinyume na maadili taarifa imeripotiwa polisi no. **BUG/RB/3725/2022** tarehe 1/5/22 yeyote mwenye taarifa zake anaombwa atoe taarifa polisi kituo cha karibu.
**DONGE NONO ATAKAE MUONA**

**ANATAFUTWA**



Ndugu **SULEIMAN SALUM SULEIMAN** pichani anatafutwa na polisi kwa tuhuma za kujihusisha na vitendo vya kinyume na maadili taarifa imeripotiwa polisi no. **BUG/RB/2332/2022** tarehe 1/5/22 yeyote mwenye taarifa zake anaombwa atoe taarifa polisi kituo cha karibu.
**DONGE NONO ATAKAE MUONA**

RIPOTI MAALUM

# Kijini Matemwe: Kijiji chenye kaya 730 na wakazi wasioyajua maji ya bomba

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR



Wakazi wa Kijiji cha Kijini Matemwe, Mkoa wa Kaskazini Unguja wakipata huduma ya maji katika kisima kilichoko kijijini kwao mwishoni mwa wiki iliyopita. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

ILIKUWA majira ya saa saba mchana Jumanne iliyopita katika Kijiji cha Kijini Matemwe, Mkoa wa Kaskazini Unguja, Nipashe ilipolishuhudia kundi la wanawake wakishirikiana kuvuta kamba yenye kidumu maalum kwa shughuli hiyo kwenye kisima chenye urefu wa mita 50 kuyafikia maji chini ya ardhi.

Pembeni kunashuhudiwa wakazi wengine wamepanga foleni kusubiri zamu yao ifike wachote maji ambayo kipindi hiki umekuwa mtihani kwa wenyeji kuyapata huku Nipashe ikidokezwa kijiji hicho hakijawahi kupata huduma ya maji kutoka Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA).

Kutokana na kutofikiwa na huduma hiyo muhimu, wanakijiji wanalazimika kutumia maji ya kisima ambayo uchotaji wake ni wa kijima, wakitumia kidumu maalum kilichofungwa kamba ya kukiwezesha kuyafikia maji umbali mrefu chini ya ardhi.

"Kila siku ninalazimika kuja hapa katika kisima hiki kutafuta maji na kama unavyokiona, maji yake yako mbali sana, ninatumia nguvu kubwa kuyapata," analalamika Miza Mcha Simai, binti mwenye umri wa miaka 19 na mkazi wa kijiji hicho.

Miza anasimulia uzoefu wake kwamba tangu familia yao imwingize kwenye orodha ya wanaopaswa kusaka mahitaji ya maji nyumbani akiwa na umri wa miaka tisa, yaani miaka 10 iliyopita, hajawahi kuyaona maji ya bomba kijijini kwao na kwamba maisha yao yote yanategemea maji hayo ya kisima.

Mwanakijiji huyo ana angalizo lingine kwamba kwa sasa visima wanavyovitegemea kupata maji, vina uhaba wa maji, hivyo anaiomba serikali kuwasogezea huduma ya maji ili kuondokana na maumivu wanayoyapa katika kutafuta huduma hiyo.

Siti Lihu Khamis (40), mkazi wa Kijiji cha Kijini Matemwe, anasema anatumia muda mwingi kutafuta huduma hiyo ya maji, hivyo anaungana na mtangulizi wake Miza kupaza sauti kwa serikali ili iwasogezee huduma ya umeme kijijini huko ili wavute maji kwa mashine.

"Kwa sasa lazima uwe na afya nzuri na nguvu mwilini ndipo upate huduma ya maji kwa sababu visima tunavyotumia havina mashine ya kuvuta maji, badala yake mikono ndiyo hutumika kuvuta maji kisimani," anasema Siti.

Mama huyo wa watoto sita anasema wanawake ndio wanaoathirika zaidi kutokana na kukosekana kwa huduma ya maji ya uhakika kijijini huko kwa kuwa wakati mwingine maji hukauka katika visima hivyo.

Anasema kwa sasa utaratibu uliowekwa ni kuchota maji kwa zamu kwa sababu maji yaliyoko katika kisima hayatoshelezi kwa wananchi wote wa kijiji hicho kutokana na visima kuwa na kiwango kidogo cha maji.

"Vifua vinatuuma kwa kuvuta maji kisimani, tunaiomba serikali itusogezee huduma hii ya maji ili wananchi wa Kijini, hasa wanawake tuondokane na uchovu unaotokana na kuchota maji kisimani," anasema.

Fatma Omar Juma anakumbusha kuwa awali kijiji hicho kilizungukwa na miti ikiwamo ya asili lakini kwa sasa hali ya mazingira ni mbaya, akisisitiza ndicho kiini cha uhaba wa maji katika visima vyao.

"Wanawake wa kijiji hiki tunatumia muda mwingi kutafuta maji badala ya harakati za kiuchumi ambazo zingetuingizia kipato na kuondokana na hali ngumu ya maisha inayotukabili.

"Maji ni changamoto kubwa kwetu, hasa sisi wanawake, maana hata unapofika muda wa kupumzika usiku, mwili wote unauma kwa kubeba ndoo za maji na kuyatoa katika kina kirefu cha kisima," analalamika.

Haji Adam, mkazi mwingine wa kijiji hicho, anasema kuwa badala ya kuhangaika kutafuta mlo kwa ajili ya familia yake, analazimika kutafuta huduma ya maji kutoka kwenye visima kijijini huko.

Adam anasema kumwachia mkewe jukumu la kutafuta huduma hiyo ni kumuumiza kimwili kwa kuwa ameshabaini unatakiwa uwe na mwili uliojengeka kwa lishe na mazoezi kuvuta maji katika kisima na kubeba ndoo za maji kutoka eneo hilo lenye kisima hadi anakoishi.

"Inanilazimu nimsaidie mke wangu kutafuta huduma hii ya maji maana maji ndio kila kitu katika maisha ya binadamu, huwezi kula chakula bila kupata maji.

"Kwa sasa kuna shida ya upungufu wa maji kijijini hapa kulinganishwa na miaka 10 iliyopita kwa sasabu zamani visima vilikuwa na maji ya kutosha lakini sasa maji yanapatikana kina kirefu," Adam anasema.

Sheha wa Kijini Matemwe, Msiyakwe Makame Haji anasema katika shehia hiyo, kuna visima 30 lakini vingi vimekauka na vichache maji yanapatikana kwa shida.

Anabainisha shehia hiyo ina kaya 730 na imeathiriwa na mabadiliko ya tabianchi kukotoka na ukataji wa miti ambayo husaidia kuwapo kwa mvua, ikizingatiwa ardhi ya kijiji hicho ina mawe.

Kiongozi huyo anawanyoshea kidole wanakijiji kwa kusababisha kutoweka kwa miti ya asili iliyokuwapo kijijini huko na hivyo kuuondoa uoto wa asili kutokana na ukataji wa miti kwa ajili ya kuni na mkaa.

Anataja mikakati yao kukabiliana na tatizo hilo katika kijiji hicho kilichoanzishwa kabla ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964, inajumuisha kupanda miti ili kuondokana na ukame ambao umeshaanza kuleta athari kijijini huko.

"Tujitahidi kulinda mazingira, hali ni mbaya kijijini hapa, mifugo imeanza kufa kutokana na kukosa maji, juzi tu mbuzi watatu walikufa," anasema.

Haji anasema Mradi wa Kuhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa Kutumia Mifumo Ikolojia Vijijini (EBARR) pia unakisaidia Kijiji cha Kijini Matemwe katika kukabiliana na athari hizo.

Alawi Haji Hija, mratibu wa mradi huo kutoka Idara ya Mazingira Zanzibar, anasema lengo la mradi huo ni kurejesha uoto wa asili katika shehia tatu za Matemwe ikiwamo Kijini kuhimili mabadiliko ya tabianchi ili kurejesha uoto wa asili.

Anabainisha kuwa mradi huo pia unakwenda sambamba na mradi wa utengenezaji wa majiko sanifu kijijini huko ambayo hayana matumizi makubwa ya kuni wakati wa kupika chakula.

Anasema majiko hayo yamesaidia kupunguza matumizi ya kuni, akibainisha kuwa asilimia 95 ya wananchi wa kijiji hicho wanatumia kuni wakati wa kupika.

Mratibu huyo anasema kuwa kupitia mradi huo, wamechimba visima sita kwa ajili ya wakazi wa Matemwe ambako kila shehia ya kijiji hicho imepatiwa visima viwili ili wananchi kupata huduma ya maji safi na salama.

"Tumemaliza kuchimba visima hivyo na hatua inayofuata ni kujenga minara kwa ajili ya kuweka tangi la maji na kuweka mashine ya kuvuta maji ili kuwapunguzia maumivu wananchi wa kijiji hicho ambao wanapata usumbufu mkubwa katika kupata huduma hiyo," anasema.

Mtaalamu huyo wa mazingira anawataka wananchi kuacha kukata miti ambayo ni chanzo cha mvua na kuongezeka kwa kina cha maji katika visima.

Mradi huo pia unatekelezwa Tanzania Bara katika wilaya nne za Mpwapwa (Dodoma), Mvomero (Morogoro), Kishapu (Shinyanga) na Simanyiro (Manyara) na kwa Tanzania Zanzibar unatekelezwa Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa lengo ni kupunguza kasi ya uharibifu wa mazingira katika maeneo hayo yaliyoathiriwa na mabadiliko ya tabianchi.

Mradi huo unatarajiwa kufikia ukomo Febuari 2024, ukiratibiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira).

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), Omar Yussuf anasema Zanzibar ni kisiwa na sababu kimeathiriwa zaidi na mabadiliko ya tabianchi.

Anasema mamlaka hiyo kwa kushirikiana na wadau wengine, wanakusudia kudhibiti upotevu wa maji, ikiwa ni pamoja na kutibu maji taka ili kuyarejesha tena kwenye matumizi ya jamii.

Mkurugenzi huyo anawataka wananchi na asasi za kimazingira kuungana kuyalinda mazingira kwa kupanda miti ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Waziri wa Nishati, Maji na Madini, Hassan Kaduara, anasema tatizo la uhaba wa maji halipo katika Kijiji cha Kijini Matemwe pekee, bali ni shida kwenye maeneo mengi ya visiwa Zanzibar na kwa sasa serikali iko katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya maji ili kukabiliana nayo.

Anasema lengo la serikali ni kuhakikisha wananchi wanapata maji kwa asilimia 100 na kwa sasa inatekeleza mradi wa maji wenye gharama ya dola milioni 92.18 kwa kujenga matangi ya kuhifadhi maji lenye ujazo wa lita milioni 32 na uchimbaji wa visima 14.

"Lengo la serikali ni kuleta huduma bora ya maji na kuwaondoshea usumbufu katika kutafuta huduma ya maji ambayo ni muhimu kwa maisha ya kila siku," anasema.

Waziri huyo pia anasema serikali inatekeleza mradi mwingine wa maji, ikitumia fedha za mkopo wa kukabiliana na athari za UVIKO-19, mradi huo ukigharimu Sh. bilioni 34 ukihusisha ujenzi wa matangi 10 ya kuhifadhi maji yenye uwezo wa kuhifadhi lita milioni moja kwa kila tangi.

"Tuna mradi mwingine wa uchimbaji wa visima 64 kupitia ufadhili wa India ili huduma ya maji iimarike Zanzibar na sasa ZAWA inakwenda kutoa huduma bora ambayo wananchi wanaitegemea," anafafanua.

Hata hivyo, waziri huyo anaweka wazi kwamba baada ya kumalizika kwa miradi hiyo ya maji, wananchi watapaswa kuchangia gharama za uendeshaji wake ili huduma hiyo iwe endelevu.

HABARI KITAIFA

# NMB yatangazwa mlipakodi mkubwa anayezingatia misingi na kanuni bora

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imeibuka mshindi wa jumla katika Tuzo za Walipakodi za Mwaka 2022 wakati wa hafla ya utoaji tuzo hizo iliyoandaliwa na Mamlaka ya Mapato (TRA) jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki iliyopita.

Tuzo hizo hutambua, kusherehekea na kuwapongeza wafanyabiashara na walipakodi wanaofuata misingi na utaratibu wa ulipaji kodi kwa hiari katika mwaka wa fedha husika.

Mbali na kunyakua tuzo ya mshindi wa kwanza kama taasisi inayozingatia misingi na kanuni bora za ulipaji kodi, NMB pia ilishinda tuzo ya mlipakodi mkubwa na bora kitaifa katika sekta ya fedha huku ikiibuka mshindi wa tatu katika kitengo cha walipakodi wakubwa katika sekta zote, na kufanya jumla ya tuzo ilizoshinda kuwa tatu.

**Tunaposherehekea tukio hili muhimu, hatuna budi kuendelea kufanya kazi kwa viwango bora ili kuongeza mchango wetu katika ukuaji wa uchumi kama mbia wa kweli wa serikali katika kutimiza ajenda ya maendeleo.**

Akizungumza baada ya kupokea tuzo hizo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna, alisema tuzo hizo zinathibitisha dhamira ya benki hiyo kufuata misingi na kanuni za ulipaji kodi na kuchangia maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini.

Alisema tuzo hizo zimewezeshwa na maono ya uongozi wa benki hiyo, kujituma na ufanisi wa wafanyakazi pamoja na kufanya kazi kwa uadilifu na kwa kuzingatia viwango bora vya uendeshaji biashara.

"Uzingatiaji wa kanuni za udhibiti wa biashara ni nguzo kuu ya muundo wa utawala bora wa Benki ya NMB na tuzo hizi zinaendelea kutupa hamasa ya kuendeleza azma yetu ya kudumisha utekelezaji na utii wa sheria za kodi kama sehemu ya maadili yetu ndani ya benki.

"Tuzo hizi zinaendelea kuthibitisha kwamba kama benki kubwa zaidi nchini Tanzania, mafanikio ya benki yetu yanaleta ustawi kwa mamilioni ya Watanzania wenzetu.

"Ninawashukuru wafanyakazi wenzangu wa Benki ya NMB kwa kufanya kazi kwa bidii, uadilifu na kwa dhamira yao ya kuchochea ukuaji wa benki yetu na taifa letu kwa ujumla," Zaipuna alipongeza.

Zaipuna aliongeza: "Tunaposherehekea tukio hili muhimu, hatuna budi kuendelea kufanya kazi kwa viwango bora ili kuongeza mchango wetu katika ukuaji wa uchumi kama mbia wa kweli wa serikali katika kutimiza ajenda ya maendeleo."

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, wakati wa hafla hiyo alibainisha kuwa kodi zilizokusanywa katika mwaka wa fedha huo ziliiwezesha serikali kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo nchini kote.

"Serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan inatambua mchango wa walipakodi katika kuchangia maendeleo ya nchi. Bila kodi hizi, serikali haitakuwa na uwezo wa kutekeleza miradi ya maendeleo kwa ukamilifu.

"Hivyo, tunapoadhimisha siku hii leo, ninapenda kuchukua fursa hii kuzishukuru kampuni na watu binafsi kwa kuendelea kulipa kodi kwa hiari," alisema.

Nape pia aliipongeza TRA kwa kutimiza malengo yaliyowekwa ya ukusanyaji wa kodi kwa mwaka 2021/22, huku akiomba mamlaka hiyo kuendelea kujenga uhusiano mzuri na walipakodi ili kuongeza ufanisi wa ulipaji wa kodi kwa hiari.

"Kitendo cha TRA kukusanya kodi Sh. trilioni 22.28 ikiwa ni asilimia 99 ya lengo la kukusanya Sh. trilioni 22.4, ni mafanikio makubwa sana na ninatumia fursa hii kuipongeza menejimenti ya TRA na wafanyakazi kwa ujumla kwa mafanikio haya," Nape alisema.

Alisisitiza kuwa dhamira ya serikali ni kuendelea kuboresha mazingira ya biashara nchini ili kuwawezesha wafanyabiashara wa ndani na nje kufanya biashara katika mazingira mazuri zaidi.



Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, akikabidhi Tuzo ya Mlipakodi Bora kwa Meneja wa Barrick (Fedha na Utawala), Melkiory Ngido (katikati) wakati wa hafla ya mlipakodi ya TRA iliyofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa. (Kulia) ni Meneja wa Kodi wa Twiga, Judith Chambua. **PICHA: MPIGAPICHA**

## Mbunge awa mwenyekiti mpya wa CCM Njombe

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MBUNGE wa Makambako mkoani Njombe, Deo Sanga, amechaguliwa kwa kura 465 kuwa Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Njombe, akifuatiwa na aliyekuwa akitetea nafasi hiyo, Jasel Mwamwala aliyepigiwa kura 139 na Anna Mlimbila aliyepata kura 15.

Akitangaza matokeo ya uchaguzi huo mwishoni mwa wiki, msimamizi mkuu wa uchaguzi, Saad Mtambule ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Mufindi mkoani Iringa, alisema jumla ya kura 619 zilipigwa.

"Hakuna kura hata moja iliyoharibika, hivyo kura zote ni halali na matokeo ni Anna Mlimbila kura 15, mzee wetu Jasel Mwamwala amepata kura 139 na Deo Sanga amepata kura 465.

"Hivyo basi, ninaomba nimtangaze Deo Sanga kuwa mshindi wa kiti cha mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Njombe," alisema Mtambule.

Pia alitangaza matokeo kwa nafasi ya mjumbe wa Halmashauri Kuu Taifa (NEC), Daniel Okoka akishinda kwa kura 450 huku wagombea wenzake Loy Mbwilo na Oscar Msigwa wakipata kura 41 na 22 mtawalia, kati ya kura 615 zilizopigwa huku mbili zikiharibika.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka aliwataka waliochaguliwa katika nafasi hiyo kutumika kuwaunganisha wana CCM badala ya kuwagawa.

"Niwashukuru wale wote ambao Mungu amewapa bafasi ya kutumika, njooni mtumike kwa kuwaunganisha wana CCM na msije kwenye kuwagawanya, wamewaamini, ninaamini viongozi wote mtakuwa kiungo ndani ya chama," aliagiza.

Mwenyekiti mpya wa CCM Mkoa wa Njombe, Sanga, aliwataka wanachama kushirikiana kutekeleza ilani ya uchaguzi ya chama chao.

## Bil. 84/- kutekeleza miradi ya maendeleo

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKOA wa Singida umekadiria kutumia Sh. bilioni 83.9 katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha wa 2022/23.

Kaimu Katibu Tawala Msaidizi - Mipango na Uratibu, Beatrice Mwinuka, akitoa taarifa juzi kwenye kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC), alisema kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 44.5 ni fedha za ndani na Sh. bilioni 39.3 ni za nje.

Alisema kuwa katika kipindi hicho, mkoa unatarajia kutumia Sh. bilioni 155.8 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo kati ya hizo, Sh. bilioni 134.5 zitatumika kulipa mishahara ya watumishi na Sh. bilioni 21.3 za matumizi mengineyo.

Mwinuka alisema Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha wa 2022/23 zimekadiria kutumia Sh. bilioni 80.1 kutekeleza programu na miradi ya maendeleo.

Kuhusu mapato ya ndani kwa mwaka 2022/23, alisema mkoa umekadiria kukusanya Sh. bilioni 19 kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mapato ya ndani, ikiwa ni ongezeko la asilimia 11.2 kulinganisha na makadirio ya mwaka 2021/22.

Vilevile, alisema kuwa katika kipindi hicho, mkoa utatoa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 1.4 kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ili kuviwezesha kujikwamua kiuchumi na kuongeza ajira na tija ya uzalishaji.

Mwinuka alisema katika utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha Julai hadi Oktoba mwaka huu, Sh. bilioni 39.4 zilizotolewa na serikali, zimetumika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Alibainisha kuwa fedha za miradi ya maendeleo zilizotolewa zinajumuisha za ujenzi wa vyumba vya madarasa 290 kwa ajili ya kidato cha kwanza, Sh. bilioni 5.8 zikitumika huku ukarabati wa miundombinu ya elimu ukigharimu Sh. bilioni 590 katika Halmashauri ya Manispaa ya Singida na Halmashauri za Ikungi na Manyoni.

Akizungumzia utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha uliopita, kiongozi huyo alisema baadhi ya miradi iliyopatiwa fedha kutoka serikali kuu na mapato ya ndani, haikukamilika kutokana na gharama za utekelezaji wa miradi hiyo kuwa juu kulinganishwa na bajeti iliyopangwa.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba alisisitiza halmashauri kuongeza juhudi katika usimamizi wa miradi inayoendelea ambayo serikali imetoa fedha ili ikamilike kwa wakati.

"Ujenzi wa vyumba 290 vya madarasa tuhakikishe ifikapo Desemba 30, mwaka huu, uwe umekamilika na kuvikabidhi serikalini ili kuwezesha wanafunzi watakaochagulia kuanza kidato cha kwanza mwaka 2023 kuanza masomo," aliagiza.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Waamuzi wanafifisha juhudi za soka la Tanzania kukua

**USHINDANI** kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu wa 2022/23, unazidi kuwa mkubwa kadri unavyosonga mbele jambo ambalo linadhihirisha wazi kila timu imejiandaa kufanya vizuri huku zikitaka kujiweka katika nafasi salama mapema kwenye raundi hii ya kwanza ili kuepuka pilikapilika ngumu za mzunguko wa pili.

Kuongezeka huko kwa ushindani kunaifanya ligi yetu kuendelea kufuatiwa ndani na nje ya nchi hasa kwa mataifa ambayo wachezaji wake wanazichezea klabu hapa nchini.

Hii inaifanya Ligi Kuu Tanzania Bara kuongeza mashabiki wengi kila uchwao jambo ambalo tunaamini muda si mrefu tutaona matunda kwa wadhamini kuongezeka kuanzia kwa klabu shiriki hadi ligi yenyewe. Hicho ndicho tunachotamani kuona kikitokea kwani kuongezeka kwa wadhamini maana yake ni kwamba maslahi kwa wachezaji yatakua lakini ubora wa soka letu utazidi kuongezeka na kuvutia wachezaji wakubwa zaidi kuja kucheza nchini jambo linaloweza kuifanya kuwa miongoni mwa ligi tano hata tatu bora Afrika.

Hata hivyo, wakati ubora huo ukizidi kuonyeshwa na klabu shiriki, waamuzi sasa wanaonekana kuwa kikwazo kikubwa sana katika nchi hii kwani pamoja na uwekezaji mkubwa unaoendelea kufanywa na klabu, wamekuwa chanzo kikubwa cha kufifisha juhudi hizo jambo linaloweza kuwakatisha tamaa wawekezaji.

Tunasema hayo kutokana na maamuzi mabovu yanayotolewa kinyume cha sheria 17 za soka, hivyo kusababisha baadhi ya timu kupoteza na nyingine kushinda pasipo kustahili, jambo ambalo mwisho wa mchezo kama ukiambiwa kutaja nyota wa mchezo pasipo na shaka utapaswa kutamtaja mwamuzi husika.

Kwa mifano michache tu, mechi kati ya Yanga na Geita Gold FC, Mwamuzi Florentina Zablon na Azam FC dhidi ya Ruvu Shooting iliyochezeshwa na Elly Sasii, tumeshuhudia zikitolewa penalti zisizostahili na kupatikana mabao ya kuamua mechi kwa Yanga na Azam kushinda 1-0, hizo zikiwa ni baadhi tu.

Ikumbukwe alama hizo tatu, mwisho wa msimu zinaweza kuamua bingwa ama timu za kushuka daraja, hivyo Shirikisho la Soka nchini (TFF), Bodi ya Ligi (TPLB) na Chama cha Waamuzi nchini (FRAT), wanapaswa kuchukua hatua kali zaidi kwa waamuzi wote wanaofinyanga sheria za soka ili kulinda juhudi kubwa zinazofanywa na baadhi ya wawekezaji na kuvutia wengine zaidi.


Lakini pia waamuzi nao wanapaswa kutambua, ubovu wanaonyesha katika maamuzi yao kunazidi kuwashusha na kupoteza sifa ya kupangwa kuchezesha mechi kubwa za kimataifa zinazosimamiwa na Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF) na lile la kimataifa, Fifa.

Katika hili Nipashe tumekuwa tukikemea mara kadhaa na kuitaka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini(TAKUKURU), kumulika suala hili kwa makini kwani imekuwa vigumu kwa mashabiki na wadau wa soka nchini kuamini kinachofanywa na waamuzi hawa ni bahati mbaya ama makosa ya kibinadamu.

Kwa haya yanayotendeka katika soka letu, yanatushawishi na sisi kuamini asilimia 75 ya kufinyangwa huku kwa sheria 17 za soka kunafanywa kwa makusudi maalum, mapenzi ama maslahi yao binafsi na si suala la kutokujua sheria jambo ambalo TAKUKURU ikiingia kwa miguu miwili hakika ukweli utajulikana. Tunaamini kama TAKUKURU italivalia njuga ni wazi hali hii itapungua kama si kumalizika kabisa, lakini kuendelea kulifumbia macho soka letu litazidi kudidimia na juhudi kubwa zinazofanywa na TFF chini ya Rais Wallace Karia, kuonekana ni kazi bure, hatutaki kutumbukia kama ilivyoikumba Ligi Kuu Italia mwaka 2006 kwa vigogo vya soka, Juventus kushushwa daraja kutokana na kashifa ya upangaji matokeo.

Hivyo, ni wakati wa kuchukua tahadhari mapema kwa hatua kali kuchukuliwa kwa wote wanaofinyanga sheria za soka kwani likiendelea kufumbiwa macho siku likilipuka litasomba wengi na kuchafua taswira nzima ya soka letu, lakini tunawaonya kama wapo wanaofanya uchafu huo kuacha mara moja.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Waamuzi walindeni wachezaji, au mpaka wavunjane miguu?

Na Adam Fungamwango

**WAKATI** kukiwa na mashaka juu ya uwezo wa uchezeshaji wa baadhi ya waamuzi hasa kwenye matukio ambayo yanatoa ushindi kwa timu zingine, kuna sehemu ambayo watu ni kama hawaioni au kuizungumzia sana.

Naona wachambuzi na watangazaji wengi huwa wanakuja juu pale waamuzi wanapofanya makosa ambayo yanasababisha timu inyimwe bao au ipate kimakosa matokeo.

Kuna eneo ambalo limefumbiwa macho nalo ni waamuzi kulinda afya za wachezaji. Kwa siku za karibuni nimeshuhudia mechi nyingi ambazo baadhi ya wachezaji wako huru kucheza rafu ambazo si za kiuanamichezo zinazoweza kugharimu maisha ya mwenzao kisoka.

Nimeona wachezaji wa sasa wa Ligi Kuu wanacheza soka kama lile la mtaani, la kurukiana miguu tena kwa makusudi na hatua zinazochukuliwa ni ndogo kulingana na kosa lenyewe.

Ni kama vile wachezaji wamekuwa hawawaogopi tena waamuzi uwanjani na hii ni hatari sana kwa mustakabali wa soka la Tanzania.

Wanatawala mechi, wanafanya wanavyotaka, wanacheza wanavyotaka. Nadhani hii inatokana na waamuzi kuonekana kuwa waoga wanapochezesha mechi hizo, labda wakihofia watakosea, au kusakamwa kwenye vipindi vya michezo na hivyo kujikuta wakishindwa kutoa maamuzi ambayo ni sahihi. Siku hizi ni nadra sana kukuta mchezaji anapewa kadi nyekundu ya moja kwa moja. Badala yake wengi ni kadi mbili za njano, tena ni baada ya mchezaji huyo kucheza rafu hatarishi zaidi ya nne.

Nimesema rafu hatarishi, sisemi zile ambazo za kimpira, kumzuia mtu kwenda kufunga au kuleta hatari langoni, ila ni zile ambazo nia ni kumuumiza mwenzake.

Unakuta mchezaji anacheza rafu mbaya za kutaka kumvunja mwenzake, lakini eti mwamuzi wanamhesabia na kumuonyesha ishara kuwa hiyo ni ya mwisho.

Ukweli ni kwamba rafu moja mbaya inaweza kumfanya mchezaji akatolewa moja kwa moja kwa kadi nyekundu na tumeona kwenye nchi ambazo soka kwao ni biashara, na ni maisha ya wachezaji, hivyo hawakubali mchezaji aonekane kuwa ni hatarishi kwa maisha ya soka ya mwenzake.

Kuna rafu mbaya nyingi zinaonekana kwenye baadhi ya mechi za Ligi Kuu ambazo zimefumbiwa macho na waamuzi na wasaidizi wao.

Na hii inatokea hasa kwa wachezaji wa timu ndogo, ambao wanaona kama ili kumzuia mchezaji staa au wa timu kubwa ni lazima umchezee rafu zisizokuwa za kimchezo, kuwakanyaga kwa makusudi, kuwapandishia miguu, kuwapiga viwiko na kadhalika.

Mfano kumpiga mtu kiwiko ni kadi nyekundu ya moja kwa moja na tuliona hilo hata hapa nchini zamani, ikitokea rafu hiyo hata mashabiki hamuulizani, lakini kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara kwa sasa unaweza kukuta mchezaji anampiga mwenzake kiwiko, lakini anaonyeshwa kadi ya njano tu. Hii imewafanya wachezaji wenye uwezo na vipaji kuwa waoga kwa sababu hawalindwi na waamuzi waliogeuka waoga.

Imewafanya pia wachezaji wa timu zinazoitwa au kujiita ndogo kujiona wana haki ya kucheza rafu dhidi ya wachezaji wakubwa.

Kibaya zaidi ikitokea wachezaji wa timu kubwa kama Simba, Yanga na Azam wakicheza rafu hata ya bahati mbaya, itaonyeshwa na kusambazwa zaidi kwenye mitandao ya kijamii na wachambuzi watashinikiza afungiwe. Lakini mchezaji huyo anakuwa amechezewa rafu mbaya nyingi kwenye mechi moja lakini haionyeshwi.

Imefika wakati waamuzi waache kuwafanya wachezaji kama wanyama, wao pia ni binadamu hivyo watendewe haki kwa kuwaadhibu wale ambao wanataka kuufanya mchezo wa soka kuwa wa kihuni.

Tusisubiri mpaka mchezaji avunjwe mguu ndipo tuibuke tuanze kuongea na kuandika, au wenye mamlaka kuanza kuchukua hatua.

HABARI KITAIFA

## RUWASA yapata dawa uhaba wa maji

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WAKALA wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Mkoa wa Singida umepanga kutumia zaidi ya Sh. bilioni 15.5 kutekeleza miradi 52 ya maji katika mwaka wa fedha wa 2022/23 ili kukabiliana na uhaba wa maji mkoani hapo.

Meneja wa RUWASA Mkoa wa Singida, Lucas Said, akitoa taarifa ya hali ya upatikanaji wa maji kwenye kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) mwishoni mwa wiki, alisema miradi hiyo inayotekelezwa kwenye halmashauri zote za mkoa huu, itakapokamilika itawanufaisha zaidi ya wananchi 239,785.

Said alitaja idadi ya miradi ya maji inayotekelezwa kwa kila halmashauri ni 11 kwa Ikungi, 11 kwa Mkalama, tisa kwa Iramba, minane ya Itigi, saba ya Singida Vijijini na minne ya Manyoni.


Kuhusu hali ya upatikanaji wa majisafi na salama vijijini kwa mkoa, alibainisha kuwa hadi kufikia Septemba mwaka huu, ilikuwa ni asilimia 61.4 ikiwa ni sawa na idadi ya watu 916,352 kati ya wakazi 1,492,433 wanaoishi vijijini na wastani wa asilimia 78 kwa wakazi wa Manispaa ya Singida.

Said aliongeza kuwa RUWASA imeendelea kuhuisha na kusajili vyombo vya utoaji wa huduma ya maji ngazi jamii (CBWSOs) ambavyo vimefikia 134 ili kuendana na matakwa ya Sheria ya Maji Na. 5 ya Mwaka 2019.

Alisema pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na RUWASA katika kuhakikisha kiwango cha upatikanaji wa maji safi na salama kinaongezeka mkoani Singida, kumekuwa na vikwazo katika usimamizi na utoaji wa huduma ya maji ambavyo ni pamoja na uhaba wa maji chini ya ardhi katika baadhi ya maeneo.

Alivitaja vikwazo vingine ni ukosefu wa vitendea kazi kama magari katika ofisi ya RUWASA mkoa na wilaya, kutumia mtandao wa zamani wa mabomba ambao takribani kilometa 70 ni tatizo kwa kuwa unachangia kiwango cha maji yasiyolipiwa, uchakavu wa dira za maji kwa wateja na gharama kubwa za tozo za visima.

Alisema ili kukabiliana na vikwazo hivyo, RUWASA itaendelea kufanya utafiti wa kina wa maji chini ya ardhi maeneo mbalimbali hata kama yako nje ya kijiji, kukamilisha ujenzi wa mradi mkubwa wa Kintinku/Lusilile katika Wilaya ya Manyoni na kuendelea kuwasiliana na Wizara ya Maji kupitia RUWASA makao makuu ili kununua vitendea kazi.




Ofisa wa Idara ya Huduma Mbadala Mifumo ya Kidigitali wa Benki ya Exim, Gregory Malembeka (kulia), akiwa na maofisa wengine kutoka Bodi ya Taifa Michezo ya Kubahatisha nchini (GBT), wakizungumza na washindi wa droo ya kampeni "Chanja Kijanja, Kimasta Zaidi" ya benki hiyo inayolenga kuhamasisha wateja wake kutumia kadi zao za Mastercard katika manunuzi ya mtandaoni au kufanya malipo kupitia mashine za malipo (POS) katika maduka mbalimbali na maeneo mengine nchini, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAKUKURU yachunguza mradi ujenzi wa madarasa

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mkoa wa Morogoro imeanza kufuatilia fedha zilizotolewa na serikali kwa ajili ya ujenzi wa madarasa na mabweni ya wanafunzi wanaotarajia kuanza masomo ya kidato cha kwanza mwakani.

Ufuatiliaji wa matumizi ya fedha hizo unalenga kujiridhisha na kuona iwapo zimetumika kwa lengo lililokusudiwa na ujenzi wake umezingatia viwango vya ubora.

Mkuu wa TAKUKURU mkoani hapa, Manyama Tungaraza, alibainisha hayo kupitia taarifa yake kwa vyombo vya habari iliyohusu utekelezaji wa majukumu ya taasisi hiyo kwa kipindi cha Julai hadi Septemba mwaka huu.

"Tumeanza kufuatilia matumizi ya fedha hizo na niwakumbushe wasimamizi wa miradi hiyo watekeleze kwa haraka kama maagizo yaliyotolewa ifikapo mwezi Januari 2023, wanafunzi wa kidato cha kwanza waanze masomo yao," alisema.

Mkuu huyo wa TAKUKURU alisema taasisi hiyo pia inaendelea kufualilia matumizi ya mbolea ya ruzuku zilizotolewa na serikali kwa ajili ya wakulima mkoani hapo.

Tungaraza alitoa onyo kwa wote watakaojihusisha na udanganyifu wowote kwa ajili ya kuhujumu mbolea ya ruzuku, watachukuliwa hatua.

Alibainisha kuwa kwa kipindi cha Oktoba hadi Desemba mwaka huu, TAKUKURU imeweka mikakati ya kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara katika miradi inayotekelezwa mkoani hapo kwa kushirikiana na taasisi zilizopewa jukumu la kuteleleza miradi hiyo.

Alizitaja baadhi ya taasisi hizo ni pamoja na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) na halmashauri za wilaya zilizoko mkoani hapo.

Tungaraza alisema jukumu lingine ni kufuatilia kwa ukaribu mifumo ya ukusanyaji wa mapato katika halmashauri ili kudhibiti upotevu wa fedha za umma na kuendelea kutoa elimu ya mapambano dhidi ya rushwa kwa jamii kupitia mpango wa TAKUKURU inayotembea pamoja na mikutano ya hadhara.

Alisema taasisi hiyo pia inaendelea na uchunguzi wa miradi mitatu ya sekta ya afya na iko katika hatua mbalimbali. Miradi hiyo ni iliyokataliwa kuwekewa mawe ya msingi kwa maelekezo kutoka kwa Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2022 ya kufanya uchunguzi ili kubaini thamani halisi ya fedha za miradi hiyo.

Aliitaja miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa Kituo cha Afya Itete wilayani Malinyi wenye thamani ya Sh. milioni 345.2, mradi wa Kituo cha afya Igima wilayani Kilombero wenye thamani ya Sh. milioni 500 na mradi wa jengo la wagonjwa wa dharura katika Hospitali ya Wilaya ya Gairo lenye thamani ya Sh. milioni 300.

Wakati taasisi hiyo ikitekeleza majukumu yake hayo, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Fatma Mwassa, ametangaza kuwashughulikia makandarasi wa miradi mbalimbali katika mkoa huo ambao hawatekelezi kazi zao za ujenzi kwa ubora, akionya kuwa hawatalipwa fedha yoyote.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED





Diwani wa Kiru, Kelemu Benjamin akionyesha shamba lenye mgogoro kati ya wananchi na mwekezaji lililoko Kiru wilayani Babati mkoani Manyara mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hoja 10 za wananchi ziara ya Samia Manyara

**•Migogoro ya ardhi kilio kikuu cha wenyeji**

**Na Waandishi Wetu,** BABATI

RAIS Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kuzuru mkoani Manyara juma hili, huku wenyeji wakiwa na matarajio mengi kutokana na ziara hiyo ya Mkuu wa Nchi.

Wananchi hao wamebainisha takriban hoja 10 wanazotarajia kupata ufumbuzi kutoka kwa Rais Samia zikijumuisha utatuzi wa migogoro ya ardhi, ujenzi wa miundombinu ya elimu, afya, barabara, skimu za umwagiliaji na tatizo la uhaba wa ajira kwa vijana.

Katika mazungumzo na Nipashe kuhusu matarajio yao kuhusu ziara hiyo, wananchi hao, akiwamo Six Omari, Mkazi wa Kijiji cha Kiru, walisema ujio wa Rais ujio wa Rais Samia utaidia kutatua migogoro ya ardhi ambayo imekuwa kero kubwa wilayani hapo.

Alisema wawekezaji wanawasumbua wananchi kutokana na kushindwa kutambua mipaka yao na hivyo kusababisha kufunguliwa kesi za migogoro ya ardhi kila mara.

Omar pia alimwomba Rais Samia asaidie kupatikana kwa huduma za majisafi, umeme na mbolea ya ruzuku kwa kuwa watendaji wanaotoa huduma hiyo wanakuwa na visingizio vingi ambavyo vinawanyima huduma wananchi.

Hoja ya Omar kuhusu migogoro ya ardhi inaungwa mkono na Diwani wa Kiru, Kelemu Benjamin aliyebainisha kuwa ni matarajio yao ujio wa Rais Samia utakuwa mwarobaini wa migogoro inayowagharimu kiasi cha kufunguliwa kesi za jinai.

Kelemu alisema migogoro ya ardhi imekuwa ikimfanya ashindwe kusimamia shughuli za maendeleo katika kata yake kwa kuwa anaishia kuswekwa rumande.

"Migogoro ipo na usuluhishi wake umeshindikana, mtu anakwenda kufanya tathmini, anarudi anasema eti kwenye mashamba kuna daraja kumbe ni uongo, anataka wananchi wasipate ardhi," alisema Kelemu.

Diwani huyo pia alitumia fursa hiyo kumwomba Rais awasaidie kujenga Kituo cha Afya Kata ya Kiru ambayo ina vijiji sita lakini inatumia zahanati moja ya Kiru Six.

Diwani wa Kisangaji, Adam Ipingika alisema ni matarajio yake ziara hiyo ya Rais itasaidia kujengwa kwa barabara za vijijini zinazopitika majira yote.

Alisema ni vizuri serikali iongeze fedha kwenye bajeti ya barabara za vijijini ili wakulima wasafirishe mazao yao.

Ipingika alisema kwenye kata hiyo, pia kuna ekari 5,000 za umwagiliaji, hivyo kuna haja Rais asaidie upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kujenga miundombinu ya umwagiliaji na kuondoa tatizo la uhaba wa chakula.

Matarajio mengine ya diwani huyo kwenye ziara ya Rais Samia ni kuja na utatuzi wa tatizo la uhaba wa ajira kwa vijana wa kada tofauti ambao wamehitimu vyuoni lakini nafasi za ajira wanaambulia patupu.

Mkazi wa Mtaa wa Mluki wilayani hapa, Ismail Bakari alisema anatamani katika ziara hiyo ya Rais Samia wananchi wapewe nafasi ya kuuliza maswali na kuwasilisha kero walizonazo.

"Babati kuna migogoro mingi ya ardhi, tatizo la umeme na maji. Akitoa nafasi ya kuongea na wananchi, atajua namna ya kutusaidia," alisema.

Bakari aliungana na watangulizi wake kunyoshea kidole migogoro ya ardhi inayoendelea kwenye maeneo mbalimbali, akilitolea mfano eneo la Makatanini ambako alidai kuna shida ya "watu wawili wanauziwa kiwanja kimoja".

Maria Sule, mkazi wa Kiru anasema mgogoro huo umewaathiri kwa kiasi kikubwa kwa sababu masika yaliyopita, wanaume walilazimika kuzikimbia familia zao na kushindwa kulima kutokana na hofu ya kukamatwa na polisi.

"Kulikuwa na msako wa usiku na mchana kuwakamata wanaume waliokuwa wanapinga mwekezaji kuendelea kulima kwenye shamba hili kwa sababu ni haki ya wanakijiji, mwekezaji naye hataki kuliachia.

"Sasa tunakabiliwa na uhaba wa chakula kwa sababu hatukulima vizuri. Na sasa mvua imeanza kunyesha, hali itakuwa ileile maana vijana hawatakubali kuona mwekezaji analima kwenye shamba ambalo Rais ameshafuta hati ya umilki kwa mwekezaji.

"Mimi ni miongoni mwa waathirika wakubwa wa mgogoro huu, mdogo wangu ni kati ya vijana wanne waliohukumiwa kifungo cha miaka 30 gerezani kutokana na mgogoro wa shamba hili. Matumaini yetu kwa sasa ni kauli ya Rais Samia kuhusu suala hili maana wawakilishi wake hapa tunaona wameshindwa," alisema.

Desemba 18, 2015, Idara ya Utawala wa Ardhi ilitoa taarifa ya kubatilisha milki ya shamba lenye ukubwa wa ekari 2,390 lililokuwa linamilikiwa kwa hati Na. 14369 kwenye eneo la Bonde la Kiru wilayani Babati mkoani Manyara.

Idara hiyo iliagiza hati hiyo imefutwa kwa amri ya Rais mnamo Novemba 4, 2015 kutokana na kukiuka masharti ya milki, ikimtaka mwekezaji kutojishughulisha au kujihusisha na lolote juu ya shamba hilo.

Uamuzi wa serikali kubatilisha hati hiyo ulisababisha mgogoro kati ya wananchi na mwekezaji aliyekuwa analimiliki, Hamir Estate Limited.

Baada ya kutolewa kwa uamuzi huo, tathmini ya kumlipa mwekezaji iliainisha zilihitajika zaidi ya Sh. milioni 700, kiasi ambacho Halmashauri ya Wilaya ya Bahati ilidai ni kikubwa, hivyo ikaamua kumega ekari 613 kati ya 2,390 ili kumpa mwekezaji kama fidia ya uwekezaji wake kwenye shamba ambalo Rais amefuta hati yake ya umiliki. Uamuzi huo wa halmashauri ndiyo unaopingwa vikali na wananchi.

Mkazi mwingine wa Babati, Tabu Abdalla (85) alisema anatamani apate fursa ya kumweleza Rais Samia namna alivyodhulumiwa shamba lake alilopewa wakati wa Operesheni Vijiji ili kiongozi huyo wa juu zaidi serikalini amsaidie kurejeshewa shamba lake.

Operesheni Vijiji ilifanyika miaka ya 1970, Rais wa wakati huyo, Hayati Mwalimu Julius Nyerere alipoamua kuwapanga wananchi katika vijiji ili kurahisisha utoaji wa huduma.

Mkazi wa Mtaa wa Negamsi, Mch. Matayo Mlegaiza alisema hatarajii kuona jipya wakati wa ziara hiyo ya Rais mkoani Manyara kwa kuwa wananchi wana kero nyingi na wamekuwa wakiwasilisha kwa viongozi wa serikali pasi na hatua kuchukuliwa.

## Wanafamilia waachiwa huru katika kesi ya mauaji

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA Kuu Tanzania Kanda ya Mwanza iliyoketi Geita, imewaachia huru watu wanne wa familia moja, wakazi wa Kijiji cha Ifugandi, Wilaya ya Nyanghwale waliokuwa wanakabiliwa na kesi ya kumuua mjukuu wao, Simon Kabula mwenye umri wa miaka miwili kisha kumtumbukiza kwenye shimo la mgodi.

Washtakiwa hao wameachiwa huru baada ya upande wa Jamhuri kudai hauna nia ya kuendelea na kesi hiyo namba 78/2020.

Washtakiwa walioachiwa ni Ngeke Lunemya, Mwajuma Petro, Ngeke Lunemya na Maria Faida ambaye ni mama yao.

Washtakiwa wote kwa pamoja walipandishwa kizimbani mbele ya Jaji wa Mahakama hiyo, Kamana Kamana kwa mashtaka ya mauaji ya Kabula.

Jaji Kamana alisema upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili Mwandamizi wa Serikali, Gisela Alex ulidai kesi hiyo ilikuwa imekuja kwa ajili ya kusikiliza lakini hauna nia ya kuendelea na kesi hiyo.

Baada ya upande wa Jamhuri kudai hapo mahakamani kuwa hauna nia ya kuendelea na kesi hiyo, Jaji Kamana aliwaambia washtakiwa wote kwa pamoja kuwa mahakama yake imewaachia huru.

Upande wa utetezi ulikuwa ukiongozwa na mawakili wawili wa kujitegemea Penina Mashimba na Rukia Marandu ambao walikuwa wakiwatetea washtakiwa wote.

Awali ilidaiwa mahakamani huko kuwa tukio hilo lilitokea Oktoba 21, 2019 katika Kijiji cha Ifugandi, Wilaya ya Nyanghwale, Mkoa wa Geita, washtakiwa wote kwa pamoja wakidaiwa kumuua Kabula kisha kuutumbukiza mwili wake kwenye shimo la mgodi wa dhahabu.

**Washtakiwa walioachiwa ni Ngeke Lunemya, Mwajuma Petro, Ngeke Lunemya na Maria Faida ambaye ni mama yao.**

## TaTEDO kuendelea kuelimisha jamii matumizi nishati jadidifu

**Na Grace Gurisha**

MKURUGENZI Mkuu wa Shirika la Maendeleo ya Nishati ya Jadi na Mazingira Tanzania (TaTEDO), Estominih Sawe, amesema wataendelea kushirikiana na serikali kuhakikisha jamii ya kitanzania inaondokana na matumizi ya kuni na mkaa.

Alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki alipozungumza na waandishi wa habari waliotembelea ofisi za TaTEDO kujifunza masuala ya nishati jadidifu na kuangalia majiko ya kisasa yanayotengenezwa ili kuelimisha jamii kuyatumia na kuondokana na nishati chafu.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, wanaunga mkono jitihada za serikali kununua na kutengeneza majiko ya kisasa yanayotumia nishati safi ili kupunguza matumizi ya mkaa katika kukabili uharibifu wa mazingira.

Alisema shirika hilo limeona elimu ni muhimu na wameendelea kuwafikia wananchi maeneo mengi ambao wamekubali kutumia nishati safi na kupunguza matumizi ya kuni na mkaa.

"Ninaomba wanaohusika na wafadhili watoe fedha na msaada wa kutosha ili Watanzania wengi wahame kwenye kutumia mkaa na kuni kwa wingi," alisema Sawe.

Mratibu wa Programu ya Nishati Tungamwataka, Shima Sago, alisema kitu chochote kinachohusu maisha ya binadamu kina fursa ya matumizi na fursa ya biashara ndiyo maana nishati endelevu zina fursa.

Alisema ukiangalia kwa sasa mkaa unaotumika mjini, bei yake iko juu kulinganisha na zamani kwa kuwa unatoka mbali na mtu akiendelea kutumia jiko la zamani la bati, atatumia gharama kubwa kwenye mkaa.

"Lakini ukitumia jiko sadifu utapunguza gharama na utaokoa kipato chako. Kama ukitumia jiko la umeme lenye presha, utatumia umeme kidogo sana, kwa hiyo elimu bado inahitajika kwa wananchi ili waweze kutumia majiko mbadala," alisema.

# Rwakatare aibuka mshindi Jumuiya ya Wazazi CCM

**Na Joseph Mwendapole**

DK. Rose Rwakatare ameibuka na ushindi wa kishindo kwenye nafasi ya Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (UWT) Mkoa wa Morogoro.

Akitangaza matokeo ya uchaguzi huo uliofanyika juzi, msimamizi wa uchaguzi huo, Hassan Nyange alisema kura zilizopigwa zilikuwa 722, zilizoharibika ni 45 na kura halali zilikuwa 677.

Alisema kuwa Dk. Rose alipata kura 413, mgombea aliyeshika nafasi ya pili ni Yusuf kimwaga (156), akifuatwa na Happy Maswa (66) na Milkel Mansuet (12).

Akizungumza baada ya kutangazwa mshindi, Dk. Rose alimshukuru Mungu kwa ushindi huo na kuwataka wajumbe wa mkutano huo kumtanguliza Mungu mbele kwa kila jambo.

Aliwapongeza wajumbe wa mkutano huo kwa kumchagua kwa kishindo, akitamka: "Ninawashukuru sana, kwa kweli leo (juzi) hii nimejua kwamba wajumbe ni watu wazuri sana, Ninawashukuru wasimamizi wa uchaguzi umekwenda vizuri, ninachoomba tufanye kazi kwa pamoja tushirikiane kuinua jumuiya yetu isikike kama zilivyo jumuiya zingine.

"Mimi ninaahidi kuwa mwenyekiti wa dot.com, tuwe na maendeleo ya 5G siyo maendeleo ya mwendo wa kinyonga, ninawaahidi kuwatumikia kwa upendo wa hali ya juu."

Akizungumza baada ya kutangaza matokeo hayo, msimamizi wa uchaguzi huo, Nyange, aliwataka walioshindwa wasikate tamaa na wasinune, badala yake wafanye kazi kwa ushirikiano na uongozi mpya wa jumuiya hiyo ili uweze kutimiza majukumu kwa ufasaha.

"Kura zikipungua unakubali matokeo na maisha yanaendelea. Kwa hiyo, tukitoka hapa uchaguzi usiwe chanzo cha mifarakano na baada ya uchaguzi huu aliyeshinda ni jumuiya, msishangilie sana mkawakwaza wengine, sisi tunajuana kwenye chama chetu, hivyo msiharibu," alisema.




Mkurugenzi wa Maadhimisho na Sherehe za Taifa, Batholomeo Jungu, akitoa mada juzi wakati wa mafunzo ya siku mbili ya wakurugenzi wa utawala na usimamizi wa rasilimali watu kutoka wizara, idara na taasisi za serikali na makatibu tawala, wasaidizi utawala na rasilimali watu kutoka mikoa yote nchini yaliyokuwa yakifanyika mjini Singida. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Vijana wa kike watakiwa kugombea nafasi kisiasa

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI Mtendaji wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Lilian Liundi, amewataka vijana wa kike kujitokeza kuwania nafasi za kisiasa ili washiriki mchakato wa kujenga taifa kwa kuwa kwenye siasa ndiko uamuzi hufanyika.

Akizungumza wakati wa mafunzo ya siku tatu za uongozi wa kifemina kwa viongozi wanawake kabla ya kumkaribisha mgeni rasmi ambaye ni Waziri Mkuu wa Serikali ya Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Ardhi, Dar es Saalam, Nyanzobe Mwakaiya, alisema vijana wengi hawana kadi za vyama na hawagombei nafasi husika.

"Ni wangapi miongoni mwenu wana kadi ya chama cha siasa? Ninaona ni wachache sana, sasa utawezaje kufika ngazi ya uamuzi kama hata kadi ya chama huna? Ni lazima tuwe na kadi na tushiriki shughuli vyema kwenye maeneo yetu na zaidi tugombee nafasi bila kuogopa.

"Chukueni nafasi za uongozi, uongozi sio misuli. Siasa ni kila kitu, tukiwa na viongozi wengi kwenye siasa itasaidia kubadili sheria, sera zetu. Bungeni vijana ni wachache sana na wasichana ndio wachache zaidi, tushuke nafasi tulete mabadiliko," alisema.

Liundi alisema lengo kuu la mafunzo hayo ni kuimarisha uwezo wa uchambuzi wa kifemina na kuongeza uwajibikaji kwenye maeneo yao.

"Mafunzo haya ni muhimu sana kwenu yana malengo mahususi ya kuongeza uwezo wa kutofautisha kati ya uchambuzi wa kijinsia na wa kifemina, kuongeza uelewa wa dhana za uongozi wa kijinsia na kifemina, kuongeza uwezo wa kutumia kanuni za kifemina katika shughuli zenu na kutengeneza mpango kazi na kubadilishana uzoefu,"alisema.

Liundi alisema uongozi thabiti na imara ni fursa ya kipekee kwa vijana wadogo, akifafanua: "Kwenye uongozi wa kifeminia tunaangalia changamoto kama fursa na namna ya kusonga mbele. Sensa ya mwaka huu imeonyesha vijana ni zaidi ya asilimia 60, lakini tukiangalia kwenye uongozi wanawake ni wachache sana na hiyo inakwenda hadi ngazi ya shule."

Liundi alisema takwimu za dunia kiuongozi marais wanawake ni 21, huku viongozi wengine na asilimia zao kwenye mabano ni Spika (29), Naibu Spika (28.3) na wabunge wote (25.5), kwa Afrika Mashariki Rwanda inaongoza kwa kuwa na wabunge wanawake (61.3) huku Tanzania ikiwa ni (36.7).

Alisema Tanzania imebahatika kuwa na wanawake wanaoongoza mihimili miwili ya nchi ambayo ni Rais Samia Suluhu Hassan na Spika Dk. Tulia Ackson huku hali ikiwa sio nzuri kwenye serikali za mitaa ambazo madiwani ni (29.4) na kati yao, wa kuchaguliwa ni asilimia saba.

Pia kwenye vitongoji na vijiji na asilimia zao kwenye mabano viongozi wanawake kwenye vijiji (2.1), vitongoji (6.7) na kwamba kwa ujumla serikali za mitaa ni chini ya asilimia 10.

Akifungua mafunzo hayo, Waziri Mkuu wa Serikali ya Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Ardhi, Nyanzobe alisema kuna vikwazo vingi kuwa kiongozi lakini kuna fursa nyingi ambazo zina faida kubwa huku akiwataka vijana hao kutoogopa kuonyesha uwezo wao.

Alizitaja fursa zilizoko ni pamoja na nafasi ya kuzungumza kwenye vikao, mikutano na semina mbalimbali, kujengwa kisaikolojia kuwa na nguvu ya kuwasemea na kuwapigania wengine, pia kutembea ndani na nje ya nchi.

# Mkandarasi kizimbani mashtaka kujipatia fedha kwa udanganyifu

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MKANDARASI wa Kampuni ya Resa Roofers, Samweli Richard (29), amefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Chato Mkoa wa Geita kwa mashtaka ya kujipatia fedha Sh. milioni 10,080 kwa njia ya udanganyifu kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Chato.

Inadaiwa kuwa mshtakiwa huyo amejipatia fedha hizo kupitia mradi wa Shule ya Msingi Kalema anakodaiwa kupeleka mabati ya geji 32 badala ya geji 28, kitendo ambacho ni kinyume cha sheria.

Mshtakiwa huyo alipandishwa kizimbani mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Amalia Mushi na aliposomewa mashtaka,

**Hakimu Mushi alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo yenye namba 3/2020 hadi Novemba 30 mwaka huu kwa ajili ya kumsomea mshtakiwa huyo maelezo ya awali.**

alikana kuhusika na kosa hilo na yuko mahabusu katika Gereza la Wilaya ya Chato kutokana na kukosa wadhamini.

Hakimu Mushi aliyataja masharti ya dhamana kwa mshtakiwa huyo kuwa anatakiwa awe na wadhamini wawili wenye barua za utambulisho kutoka kwa Ofisa Mtendaji wa Kata pamoja na mali isiyohamishika yenye thamani ya Sh. milioni 12,000 kwa kila mdhamini.

Upande wa Jamhuri unaoongozwa na Wakili wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Geita, Antidius Rutayuga, aliyedai upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na kuomba tarehe nyingine kwa ajili ya kumsomea mshtakiwa maelezo ya awali.

Hakimu Mushi alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo yenye namba 3/2020 hadi Novemba 30 mwaka huu kwa ajili ya kumsomea mshtakiwa huyo maelezo ya awali.

Awali akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa TAKUKURU Mkoa wa Geita, Rutayunga, alidai kuwa kati ya Mei Mosi na Julai 30 mwaka 2021, mshtakiwa Samweli Richard, akiwa mmiliki wa Kampuni ya Resa Roofers, alijipatia fedha kwa njia ya udanganyifu kupitia namba 000622 ya Mei 17, 2021 na P.I.NO.PI/KIM/01 vyote vya Juni 16, 2021 kwa lengo la kujipatia Sh. milioni 10.08 kutoka kwa Halmashauri ya Wilaya ya Chato kupitia Shule ya Msingi Kalema kwa kupeleka mabati ya geji 32 badala ya geji 28, kitendo ambacho ni kinyume cha sheria.




Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango (wa pili kulia), akikabidhi tuzo ya utambuzi kwa uongozi wa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) ukiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Theobald Sabi (wa pili kushoto), ikiwa ishara ya kutambua mchango wa benki hiyo kufanikisha maendeleo ya sekta ya viwanda nchini, katika tuzo 16 za Rais za PMAYA zilizoratibiwa na Shirikisho la Wenye Viwanda nchini (CTI). Hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Habari Uk.26. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Simbachawene aonya ucheleweshaji uamuzi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene amesema moja ya mambo yanayosababisha sekta ya umma isiwe na ufanisi, ni ucheleweshaji katika kutoa uamuzi na urasimu.

Alitoa kauli hiyo jana wakati akifunga mafunzo ya siku mbili ya wakurugenzi wa utawala na usimamizi wa rasilimali watu kutoka wizara, idara na taasisi za serikali na makatibu tawala wasaidizi utawala na rasilimali watu kutoka mikoa yote nchini yaliyokuwa yanafanyika mjini hapa.

"Moja ya kazi ya ofisa wa rasilimali watu ni kuangalia kama kuna urasimu katika ofisi, pia kama waziri au katibu mkuu anachelewa kutoa uamuzi aelezwe maana ninyi ni wakurugenzi rasilimali watu, ni watu wakubwa sana, mna jukumu la kuwasimamia viongozi," alisema.

Simbachawene alisema watumishi lazima watambue kuwa kama mifumo haifanyi kazi vizuri, wananchi ndiyo wanaumia, hivyo wakurugenzi wa rasilimali watu wahakikishe wanawapima viongozi walioko chini na juu wanavyofanya kazi na kuchukua hatua ili kuleta ufanisi wa kazi serikalini.

Simbachawene pia alisema katika suala la itifaki, kumekuwa na mikanganyiko mingi wakati wa maadhimisho, sherehe na matukio ya kitaifa, hivyo ni lazima kuwa mkakati ili kuhakikisha mambo hayafeli.

Pia alisema nembo ya taifa imekuwa ikichezewa na watu ambao wamekuwa wanaitumia ovyo, hata ambao hawajapewa idhibati.

Alisema mafunzo endelevu kwa mtumishi ni muhimu katika kumwendeleza kwenye eneo lake la kiutendaji, kumkumbusha mambo muhimu ambayo anapaswa kuyatekeleza katika majukumu yake ya kila siku pamoja na kumwezesha kubadilika kutokana na mabadiliko ya sera, itikadi, sheria na mazingira ya wakati husika.

Mkurugenzi wa Maadhimisho na Sherehe za Taifa, Batholomeo Jungu, alisema wameamua kutoa mafunzo hayo kwa kuwa kumekuwa na tatizo kubwa kwenye eneo la itifaki ya viongozi wakati wa sherehe na matukio mbalimbali ya kitaifa katika kuwatambua, kujua wajibu wao na masuala ya ustaarabu."

# Sekta binafsi yahakikishwa mazingira bora ya biashara

**Na Gwamaka Alipipi**

SERIKALI imeihakikishia sekta binafsi kuitengenezea mazingira bora ya kuuza bidhaa katika masoko ya jumuiya za kikanda na kutunga sera na sheria zitakazokuwa rafiki kwao.

Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa mkutano uliowakutanisha Maofisa Watendaji Wakuu wa Kampuni (CEOrt) na maofisa wa serikali, uliolenga kuweka mazingira rafiki ya biashara pamoja na kutatua matatizo yanayoikumba sekta binafsi.

Kigahe alisema lengo la serikali ni kuiona sekta binafsi inakuwa kiongozi katika kukuza uchumi wa nchi.

"Tupo hapa kufanya majadiliano na sekta binafsi ili kuwaboreshea mazingira ya ufanyaji biashara pamoja na kutatua kero zinazowasibu. Tutatumia mkutano huu kupata maoni na ushauri juu ya namna bora ya ufanyaji biashara nchini," alisema Kigahe.

Alisema Tanzania iko katika jumuiya mbalimbali kama vile Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), hivyo ni wajibu wa serikali kuwatafutia masoko ya uhakika sekta binafsi katika jumuiya hizo.

"Ili sekta binafsi iweze kukua, ni lazima itengenezewe mazingira bora ya masoko katika kanda. Na hilo ni jukumu la serikali. Bidhaa zetu zinapopata soko katika kanda mbalimbali, zinachagiza ukuaji wa uchumi," alisema.

Kigahe alisema sekta binafsi nchini inakabiliwa na matatizo mengi ikiwamo kukithiri kwa bidhaa bandia na magendo.

Alisema serikali kupitia Tume ya Ushindani (FCC) imekuwa ikisaidia katika kutokomeza uvamizi wa bidhaa feki na za magendo.

Kigahe alisema: "Kutokomeza bidhaa feki na bandia ni mchakato mrefu, siyo wa siku moja lakini tumekuwa tukiweka mazingira wezeshi ili kuwawezesha Watanzania kupata bidhaa bora. Kwa sasa tunaendelea kuboresha suala hilo kwa kutunga sera na sheria rafiki."

Mwenyekiti wa CEOrt, David Tarimo alisema kilio cha sekta binafsi kwa miaka mingi ni uboreshwaji wa mazingira ya biashara, sera, kodi pamoja na masuala ya vibali kutoka Jeshi la Uhamiaji.

Alisema sekta binafsi nchini ina uwezo wa kukuza uchumi wa nchi kama ikiwekewa mazingira rafiki ya kufanya biashara na kutatuliwa matatizo yanayoikabili.

# Kaya 2,000 zakabiliwa na uhaba wa chakula

**Na Cynthia Mwilolezi,** LONGIDO

MBUNGE wa Longido mkoani Arusha, Dk. Stephen Kiruswa (pichani), amesema zaidi ya kaya 2,000 wilayani humo zinakabiliwa na uhaba wa njaa, hali inayosababisha shughuli za kiuchumi kuzorota.

Dk. Kiruswa ambaye ni Naibu Waziri wa Madini, alieleza kuhusu tishio hilo jana wakati akikabidhi tani 40 za mahindi ya chakula aliyonunua kwa ajili ya wananchi wake kutoka kwa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA).

**Achilia mbali binadamu kukosa chakula, lakini hata mifugo inakufa kwa kukosa malisho na maji.**

Mahindi hayo yatauzwa kwa wananchi kwa bei nafuu baada ya kusambazwa katika kata 18 wilayani humo zinazokabiliwa na ukame.

"Longido ni moja ya wilaya zinazokabiliwa na ukame uliopelekea uhaba wa chakula. Achilia mbali binadamu kukosa chakula, lakini hata mifugo inakufa kwa kukosa malisho na maji.

"Leo (jana) nimekuja kukabidhi mahindi tani 40 sawa na maguni zaidi ya 400 ili kusaidia kila mwananchi kupata kilogramu 20 za mahindi. Hii ni mahususi kwa ajili ya kupunguza makali ya njaa," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Kiruswa, serikali imetenga zaidi ya tani 180,000 za mahindi kwa ajili ya kuwauzia wananchi wa Longido kwa bei nafuu.

Alisema kiasi hicho kilichotengwa ni kikubwa kuliko wilaya yoyote inayokabiliwa na njaa kwa sasa na kwamba uamuzi huo umezingatia uhitaji na madhara ya ukame.

Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Arusha, Zaitun Swai, akizungumza kabla ya makabidhiano hayo, alisema serikali haitakubali kuona mwananchi wake anakufa kutokana na njaa.

"Ninampongeza sana Dk. Kiruswa kwa kusaidia kaya hizi 2,000 zilizoko katika Wilaya ya Longido. Anapaswa kuungwa mkono na wadau wa wilaya nyingine kwa kuwa ukame umewakuta wakazi wote," alisema Zaituni.



Katibu Tawala Msaidizi wa Wilaya hiyo, Boniface Lugola, alimshukuru Dk. Kiruswa kwa msaada huo kwa ajili ya wananchi wa jimbo lake huku akielezea kuwa moyo wa kujitolea unapaswa kupongezwa kwa dhati na wengine kuiga mfano huo.

Alisema wakati serikali inajipanga kuuza mahindi kwa bei elekezi, hivyo wadau wengine wajitokeze kununua mahindi hayo ili kuwasaidia wananchi wengine ambao kipato chao si kikubwa ama kimesababishwa na hali iliyoko.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Longido, Saimon Oitesoi, alimshukuru kiongozi huyo kwa kuwa wa kwanza kununua mahindi na kuyasambaza kwenye kata zote huku akisema kuwa chakula hicho kimefika kwa muda mwafaka.

## Serikali yatoa milioni 100/- ujenzi wa shule

**Na Allan Isack,** ARUMERU

SERIKALI imetoa zaidi ya Sh. milioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya Shule shikizi ya Olmapinuu iliyoko Kijiji cha Bwawani, Wilaya ya Arumeru mkoani Arusha.

Shule hiyo ilikuwa na uhaba wa vyumba vya madarasa na wanafunzi kukaa chini, hali iliyokuwa kikwazo katika ustawi wa kitaaluma.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa umma na Mkuu wa Idara ya Mipango wa Halmashauri ya Arusha, Anna Urio, fedha hizo zitatolewa kwa awamu mbili ili kuboresha shule hiyo.

"Kabla ya serikali kupeleka fedha za ujenzi wa miundombinu yake, kwa sababu siku za usoni wazazi na walimu walikuwa na hofu kubwa. Wazazi walisita kuwaandikisha watoto wadogo Olmapinuu na kuwapeleka kusoma Shule ya Msingi ya Olokii.

"Fedha hizo zitatumika kujenga miundombinu ya shule hiyo, ikiwamo za ujenzi wa vyumba vya madarasa, matundu 10 ya vyoo na nyumba ya mwalimu," alisema.

Akifafanua zaidi kuhusu ukarabati wa shule hiyo, Urio alisema serikali katika awamu ya kwanza imetoa Sh. milioni 40 kupitia fedha za Mradi wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19, ambazo zimetumika kujenga vyumba viwili vya madarasa na kuweka madawati 25.

Mjumbe wa Kamati ya Ujenzi wa Shule hiyo, Shaban Rashid, alisema waliguswa kushiriki katika ujenzi huo kutokana na kuona umuhimu wa kuwapo kwa nyumba ya walimu ambayo wataishi hapo na kuwafundisha watoto wao.

Kwa mujibu wa Rashid, wanafunzi wa shule hiyo wanateseka kwa miaka mingi kwa kuwa na shule ya msingi iliyoko mbali na imetenganishwa na korongo, ambalo wakati wa mvua watoto hushindwa kuvuka na kukosa masomo kwa zaidi ya miezi minne mpaka sita.

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Zakayo Lukumai, alisema shule hiyo ilikuwa na kikwazo cha wanafunzi kuketi chini na baada ya muda walipata darasa moja la nyasi, lakini mwaka 2022 serikali ilijenga vyumba viwili vya madarasa na wanatarajia yatasaidia kuongeza idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa shuleni huko.



Ofisa wa Mambo ya Utamaduni kutoka Ubalozi wa Marekani nchini, Chad Morris (kushoto), akitazama picha za wanasayansi katika Kituo cha Sayansi jijini Tanga cha STEM PARK mwishoni mwa wiki wakati wa ufunguzi wa kambi kwa wanafunzi zaidi ya 120 wa sekondari kujifunza mambo ya kisayansi kikiwamo kilimo janja. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

## Shirika lataka hatua za afya lishe kuwasaidia watoto wachanga nchini

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

SHIRIKA la Children Incrossfire (CIC) linalojihusisha na malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto nchini, limesema kama serikali haitachukua hatua za kuimarisha afya lishe, asilimia 43 ya watoto wako katika hatari ya kutokufikia utimilifu wa ukuaji.

Kwa mujibu wa Msimamizi wa Miradi CIC, Frank Kasomangala, ili kudhibiti hatari hiyo, serikali haina budi kuimarisha lishe bora kwa watoto, afya, elimu ya awali, ulinzi na usalama na malezi yenye mwitikio.

Kasomangala aliyasema hayo mwishoni mwa wiki katika Mji wa Babati wakati wa kikao cha mapitio cha robo ya kwanza ya Mradi wa Mtoto Kwanza unaotekelezwa na serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo chini ya Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (PJT-MMMAM).

Akizungumza katika kikao hicho, Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Mkoa wa Manyara, Lilian Bujune, alisema ukatili unaoendelea dhidi ya watoto na wanawake kwa asilimia 60 unafanyika nyumbani.

"Mkakati wa serikali kukomesha vitendo hivi tunahimiza wazazi waache kuficha vitendo vya ukatili wanavyofanyiwa watoto na maofisa elimu wasaidie kutengeneza madarasa ya awali yanayozungumza, ili yawasaidie watoto kuanzia miaka sifuri hadi minane katika ujifunzaji," aliagiza.

Alisema tatizo lililopo hivi sasa katika jamii ni kuwapuuza watoto na kushindwa kufanya uwekezaji wa watoto, ili waje wawe wataalamu wazuri wa baadaye.

Akielezea matarajio yake kuhusu mkakati huo, Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanan'g, Martha Sulle, alisema anatamani kungepatikana kituo maalum cha kuhifadhi watoto wanaofanyiwa ukatili katika mkoa huo kwa kuwa kukosekana kwake kunasababisha kesi za ukatili kumalizwa kienyeji.

Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto, pamoja na mambo mengine, inahimiza umuhimu wa kuwekeza mapema kwa mtoto kwa kuwa ukuaji unaanza wakati wa kutungwa mimba hadi miaka minane, kipindi ambacho ni cha ukuaji zaidi.

# Manyara kukusanya bil. 34/- kutoka kwa wafanyabiashara

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

MKOA wa Manyara umepanga kukusanya zaidi ya Sh. bilioni 34.46 katika kipindi kilichobaki cha mwaka wa fedha 2022/23 kutoka kwa wafanyabiashara na wawekezaji walioko mkoani hapo.

Akielezea utekelezaji wa mpango huo juzi, Meneja wa Mamlaka ya Mapato (TRA) Mkoa wa Manyara, Pendolake Msangi alisema lengo hilo linatokana na ufanisi wa ukusanyaji kodi ya mapato mwaka uliopita.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2021/22, TRA ilikusanya Sh. bilioni 27.2, sawa na asilimia 89 ya lengo lililowekwa.

**Kwa robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2022/23, tumeshakusanya Sh. bilioni 12.7, sawa na asilimia 125.**

"Leo (juzi) tumefanya mazoezi ya utimamu wa mwili kama njia mojawapo ya kupita mitaani kuwashukuru wananchi wa Manyara kwa kulipa kodi bila shuruti.

"Kwa mwaka uliopita, lengo lilikuwa ni kukusanya Sh. bilioni 31.3, ila tulishindwa kutokana na tishio la ugonjwa wa UVIKO-19.

"Kwa robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2022/23, tumeshakusanya Sh. bilioni 12.7, sawa na asilimia 125," alisema.

Msangi alisema mafanikio hayo yamechangiwa na kuimarishwa kwa mifumo ya kulipa kodi, kusikiliza malalamiko ya wafanyabiashara, kufanyia kazi haraka kero za walipakodi na wauzaji kutoa stakabadhi kama sheria inavyotaka.

Mkuu wa Wilaya ya Babati, Lazaro Twange akizungumza na wafanyakazi wa TRA, alisema ulipaji wa kodi ni wajibu wa kisheria na sio hiari.

"Wanaodhani wanaweza kukwepa kodi wajiandae kisaikolojia kwa kuwa hawatabaki salama," alionya.

Ofisa Elimu na Huduma kwa Mlipakodi, Serapio Luanda, alisema kilichowafanya wakusanye kwa ufanisi ni wafanyabiashara kulipa kodi kwa hiari.



Mkurugenzi Mtendaji (DED) wa Halmashauri ya Mwanga, Mwajuma Nasombe (wa pili kushoto), akiangalia masilia ya wanyama waliohifadhiwa Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi mwishoni mwa wiki. **PICHA: JAMES LANKA**

# Kanisa lakabidhi miche ya matunda 30,000 kutunza mazingira Arusha

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

KANISA la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho limekabidhi miche ya matunda 30,000 kwa uongozi wa Mkoa wa Arusha ikiwa ni sehemu ya mikakati ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Akizungumza jana wakati wa kukabidhi miche hiyo ya matunda, Rais wa Kanisa hilo, John Kasongo alisema pamoja na kutunza mazingira, pia wanasaidia usalama wa chakula kwa wananchi mkoani humo.

Kasongo alisema kanisa limekuwa likisaidia masuala mbalimbali ya kijamii katika mikoa mbalimbali nchini, ikiwamo elimu, afya na masuala ya usalama wa chakula.

Kwa mujibu wa Kasongo, mkoa huo ni wa kwanza kupata miche hiyo huku akieleza mipango ya baadaye ni kusaidia masuala ya elimu kwa shule za serikali kama mchango wao katika kuunga mkono serikali.

"Kama kanisa tumekuwa tukisaidia shughuli za maendeleo mikoa mbalimbali ambapo tumeshasaidia Mkoa wa Dodoma na kwa hapa Arusha baada ya kukabidhi miti tuna mpango wa kusaidia masuala ya elimu katika shule za serikali," alisema.

Aliongeza kuwa katika masuala ya chakula wamekuwa wakitoa chakula kunapotokea majanga ili kusaidia waathirika. Katibu Tawala Mkoa wa Arusha, Missaile Musa, alilishukuru kanisa hilo kwa kuona uhitaji uliopo na kugawa miche hiyo.

Alisema miche ya matunda itasambazwa katika shule na taasisi mbalimbali za mkoa huo ili kutunza mazingira na kupata miti kwa ajili ya kivuli, matunda na kukabiliana na ukame.

Alisema kuwa licha ya kupewa miche hiyo, bado wana uhitaji wa miche zaidi kwa ajili ya kusaidia maeneo mbalimbali.

Baadhi ya wadau waliokabithiwa miti hiyo, akiwamo Lukas Anthony na Wahida Kessy, walisema kanisa hilo limetoa miti katika kipindi ambacho mkoa huo una uhitaji mkubwa wa kupanda miti kutokana na tishio la ukame lililosababishwa na mabadiliko ya tabianchi.

# Asasi yajitosa kunusuru msitu

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

ASASI ya Roots & Shoot inayofanya kazi chini ya Taasisi ya Kimataifa ya Uhifadhi na Ulinzi wa Mazingira ya Jane Goodall Institute, imeanza kuchukua hatua kuzuia uharibifu mkubwa wa mazingira unaoendelea katika Msitu wa Hifadhi ya Asili wa Rau uliogeuzwa dampo la taka.

Msitu huo wenye ukubwa wa hekta 584, uko katikati ya Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro.

Akizungumza jana baada ya kuendesha kampeni maalum ya kuokoa hifadhi hiyo isiharibiwe, iliyopewa jina la 'No Waste November', Mratibu wa Roots & Shoots ya Mkoa wa Kilimanjaro, Ahimidiwe Makisa alisema wameanza kuondoa taka zote.

Katika kampeni hiyo, wadau hao wa uhifadhi na ulinzi wa mazingira wameokota uchafu ambao ni viroba 65 vya magunia yaliyojaa chupa za platiki za maji, sharubati, pombe kali na mafuta ya aina mbalimbali yanayotupwa ndani ya msitu huo.

"Tunachokifanya ni kuhakikisha tunaondoa taka zote, kwa sababu msitu huu umezungukwa na makazi ya watu na vijiji. Wakazi wengi ambao wameuzunguka msitu huu ambao sio waaminifu, wanatupa taka kwenye msitu.

"Taka ambazo ni hatari zaidi ni taka za plastiki zinazokaa ardhini kwa zaidi ya miaka 100 bila kuoza. Imetulazimu kuziondoa ndani ya hifadhi, wanafunzi 100 wa Shule ya Sekondari Mji Mpya, Sekondari ya JK Nyerere, Shule ya Msingi Langoni na Shule ya Msingi Shauri Moyo wameshiriki.

"Kila shule imetoa wanachama wa klabu ya Roots & Shoots 25, sawa na wanachama 100 kwa shule zote nne. Tunaamini kampeni hii ni chachu ya usafi kwa miezi mingine ndani ya mwaka," alisema.

Aliongeza: "Tunategemea vitalu hivi vitazalisha miche zaidi ya 80,000 kwa mwaka na tutakuwa tukitoa miche hiyo bure kabisa kwa taasisi za umma kama shule, zahanati na hospitali ili kurudisha ikolojia ya Mkoa wetu wa Kilimanjaro."

Mratibu wa Roots & Shoots wa Ofisi ya Kanda ya Kaskazini iliyoko Mkoa wa Arusha, Erasto Njavike, alisema katika programu zinazotekelezwa hivi sasa, wanatoa fursa kwa wanafunzi wa shule za msingi, sekondari na vyuo kukaa pamoja na kutafakari, kufikiri na kuzungumza juu ya matatizo ya mazingira yanayoizunguka jamii.

NIPASHE JUMATATU OKTOBA 21, 2022
Nipashe
Spotika



VIKOSI VYOTE 32 KOMBE LA DUNIA QATAR 2022 UK. 16

# KIUFUNDI ZAIDI...



Kiungo wa Yanga, Feisal Salum 'Fei Toto', akionyesha ufundi dhidi ya nyota wa Singida Big Stars wakiwamo Wabrazil wa timu hiyo kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Alhamisi iliyopita na Yanga kushinda 4-1. **MPIGAPICHA WETU**

## ISIKUPITE

MECHI tano kali za kutazama za hatua ya makundi Kombe la Dunia la Fifa nchini Qatar 2022; #1. Ureno vs. Uruguay (Kundi H: Jumanne Novemba 29), #2. Hispania vs. Ujerumani (Kundi E: Jumatatu, Novemba 28), #3. Argentina vs. Mexico (Kundi C: Jumapili, Novemba 27), #4. Brazil vs. Uswisi (Kundi G: Jumatatu, Novemba 28) na #5. Ufaransa vs. Denmark (Kundi D: Jumamosi, Novemba 26).



# NYOTA 6 WAKONGWE ZAIDI KOMBE LA DUNIA

Inatosha kusema, Kombe la Dunia la FIFA la 2022 litakuwa maalum kwa safu ya wachezaji kwa sababu tofauti. Bila kuchelewa zaidi, hebu tuangalie wachezaji sita wakongwe zaidi kwenye Kombe la Dunia la FIFA la 2022 nchini Qatar.

Beki wa kati mkongwe wa Chelsea na Brazil, Thiago Silva atajaribu kuweka wazi uzoefu wake wote kwenye Kombe la Dunia la FIFA la 2022.



**Thiago Silva (Brazil)**

**DOHA, Qatar**

KOMBE la Dunia la FIFA 2022, limeanza jana Jumapili nchini Qatar. Mataifa 32 yapo na vikosi vyao rasmi kwa ajili ya michuano hiyo na mashabiki wa soka duniani kote wameanza kushuhudia michuano hiyo.

Ni ndoto kwa mwanasoka yeyote kucheza kwenye Kombe la Dunia na tutaona wanasoka wengi wachanga wakitimiza ndoto zao wakati huu. Lakini kwa upande mwingine wa wigo, tutaona wakongwe kadhaa wakicheza katika kile kinachowezekana kuwa kombe lao la mwisho la dunia.

Inatosha kusema, Kombe la Dunia la FIFA la 2022 litakuwa maalum kwa safu ya wachezaji kwa sababu tofauti. Bila kuchelewa zaidi, hebu tuangalie wachezaji sita wakongwe zaidi kwenye Kombe la Dunia la FIFA la 2022 nchini Qatar.

**#6. Cristiano Ronaldo (Ureno) - miaka 37, miezi 9 na siku 15**

Anapoiongoza Ureno nchini Qatar, Cristiano Ronaldo amejiunga na orodha ya wachezaji mashuhuri ambao wamecheza katika michuano mitano tofauti ya Kombe la Dunia.

Ni Lothaur Matthaus, Antonio Carbajal na Rafael Marquez pekee ndio walikuwa wanashikilia rekodi ya kucheza mara tano michuano hiyo. Gwiji wa Italia Gianluigi Buffon alijumuishwa katika vikosi vitano tofauti vya Kombe la Dunia, lakini amecheza katika michuano minne pekee.

Huenda hili likawa Kombe la Dunia la mwisho kwa Ronaldo anapoingia katika michuano hiyo akiwa mfungaji bora katika soka la kimataifa la wanaume (mabao 117). Ronaldo ataongoza safu ya Ureno kwenye Kombe la Dunia la FIFA la 2022 na atatumaini kulipeleka nyumbani.

**#5. Thiago Silva (Brazil) - miaka 38, mwezi 1 na siku 29**

Beki wa kati mkongwe wa Chelsea na Brazil, Thiago Silva atajaribu kuweka wazi uzoefu wake wote kwenye Kombe la Dunia la FIFA la 2022. Licha ya kuwa na umri wa miaka 38, Silva anaendelea kuwa kiungo mkuu kwenye moyo wa ulinzi kwa klabu na nchi.

Silva, Marquinhos, Eder Militao na Gleison Bremer ni chaguo la kocha Tite katika nafasi ya beki wa kati katika michuano hiyo.

**#4. Dani Alves (Brazil) - miaka 39, miezi 6 na siku 14**

Umeona kwa nini hatukumwita Thiago Silva mchezaji mzee zaidi wa Brazil kwenye Kombe la Dunia? Tofauti hiyo imewekwa na beki wa kulia Dani Alves. Anatazamiwa kuwa Mbrazil mwenye umri mkubwa zaidi kuwahi kushiriki Kombe la Dunia la FIFA.

Rekodi hiyo hapo awali ilikuwa ikishikiliwa na Djalma Santos, ambaye alicheza Kombe la Dunia la mwaka 1966 akiwa na umri wa miaka 37. Alves ameshiriki Kombe la Dunia mara tatu, lakini hakuwa sehemu ya kikosi cha Selecao hao mwaka 2018 kutokana kuwa majeruhi.



CR7 na Pepe

Mashabiki walishangazwa kidogo na uteuzi wake kwani kwa sasa anachezea klabu ya Liga MX Unam. Lakini kocha Tite anaamini kwamba Alves anaweza kuwa rasilimali muhimu katika Kombe la Dunia la FIFA la 2022.

**#3. Eiji Kawashima (Japan) - miaka 39 na miezi 8**

Kipa mkongwe Eiji Kawashima, ambaye atafikisha umri wa miaka 40 Machi 2023, amejumuishwa katika kikosi cha Japan kwa ajili ya Kombe la Dunia la FIFA la 2022. Amekuwa kipa chaguo la kwanza kwa Japan kwa miaka 12 na alifanya kazi nzuri sana kwenye Kombe la Dunia la 2018.

Alikuwa mchezaji mzee zaidi kuichezea Japan kwenye Kombe la Dunia mwaka 2018. Kawashima sasa amevunja rekodi yake mwenyewe.

**#2. Pepe (Ureno) - miaka 39, miezi 8 na siku 25**

Beki wa kati wa Ureno, Pepe amekuwa na kazi nzuri kwa klabu na nchi. Yeye ni mwanamichezo wa ajabu na anaendelea kuwa mmoja wa mabeki chaguo la kwanza wa Ureno akiwa na umri wa miaka 39. Uzoefu wa Pepe kwenye hatua kubwa utakuwa muhimu kwa Ureno kwenye Kombe la Dunia la FIFA la 2022.

Pepe alikuwa sehemu ya timu ya Ureno iliyoshinda Euro 2016 na Ligi ya Mataifa ya Uefa 2019..

**#1. Atiba Hutchinson (Canada) - miaka 39, miezi 9 na siku 12**

Atiba Hutchinson ndiye mchezaji pekee mwenye umri mkubwa zaidi katika kikosi cha Canada na michuano hiyo. Canada imefuzu kwa mara ya kwanza Kombe la Dunia tangu mwaka 1986. Atakuwa mchezaji mwenye umri mkubwa zaidi kushiriki michuano hiyo na kuna uwezekano wa kufanya hivyo huku akivaa kitambaa cha unahodha.

Hutchinson kwa sasa anaichezea Klabu ya Uturuki ya Besiktas na anashikilia rekodi ya kucheza mechi nyingi zaidi katika ngazi ya soka ya kimataifa nchini Canada (mechi 97).

KOM IA QATAR 2022



André-Frank

# WACHEZAJI 3 WA KIAFRIKA WENYE KIWANGO BORA KOMBE LA DUNIA

**DOHA, Qatar**

FAINALI za Kombe la Dunia za 2022 zimeanza jana, Jumapili nchini Qatar. Mashindano hayo yatakamilika Desemba 18, mwaka huu.

Afrika kama bara halijashinda Kombe lolote la Dunia, lakini imetoa wachezaji wa heshima kama Yaya Toure, Didier Drogba, na Jay-Jay Okocha ambao wamejidhihirisha katika ulimwengu wa soka.

Makala haya yanawaangalia wachezaji watatu wa Kiafrika walio katika kiwango bora zaidi kwenye Kombe la Dunia la Qatar 2022.

**#3. André-Frank Zambo Anguissa (Cameroon)**

Mcameroon huyo bila shaka ni mmoja wa viungo wa Kiafrika walio katika kiwango bora zaidi msimu huu na kiwango chake cha kazi kimekuwa kizuri sana akiwa na Napoli katika safu ya kiungo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, amefunga mabao mawili na amesajili pasi mbili za mabao katika mechi 12 za ligi hadi sasa. Vile vile, amefunga bao moja na amesajili pasi tatu za mabao katika mechi tano za Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu.

Ufahamu wake katika safu ya kiungo na uzoefu utakuwa muhimu kwa Cameroon kwenye Kombe la Dunia na itakuwa ya kuvutia kuona kama anaweza kulisaidia taifa lake katika mashindano hayo.

**#2. Boulaye Dia (Senegal)**

Mshambuliaji huyo amekuwa mmoja wa watu walio nyuma ya kiwango kizuri zaidi cha timu ya Salernitana msimu huu na uwapo wake kwenye safu ya ushambuliaji umekuwa na matunda kwa timu yake.

Dia amefunga mabao sita na amesajili pasi mbili za mabao katika mechi 13 za ligi hadi sasa. Vile vile, ndiye mfungaji bora wa tatu katika Ligi Kuu ya Italia, Serie A, msimu huu.

Kiwango chake cha kuvutia cha kufunga kitakuwa muhimu kwa Senegal katika Kombe la Dunia na itafurahisha kuona kama ushirikiano wake kwenye safu ya ushambuliaji utakuwa na matunda.

**#1. Inaki Williams (Ghana)**

Fowadi huyo hapo awali alichagua kuichezea Hispania katika mechi za kimataifa, lakini hivi majuzi alibadilisha uraia wake na kuiwakilisha Ghana katika Kombe la Dunia.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, amekuwa bora katika mashambulizi ya Athletic Bilbao hadi sasa. Vile vile, amefikisha mabao matano na amesajili pasi moja ya bao katika mechi 14 za LaLiga msimu huu.

Kutokana na kiwango chake, uwapo wake utakuwa muhimu kwa Ghana kwenye safu ya ushambuliaji na anabaki kuwa mchezaji muhimu kwa timu yake ya taifa kwani wapo kwenye moja ya makundi magumu zaidi katika michuano hiyo pamoja na Ureno, Uruguay na Korea Kusini.

## NJE YA UWANJA

KATIKA makombe matano ya thamani kubwa zaidi duniani, la kwanza ni Kombe la Dunia (Euro milioni 17), likifuatiwa na Kombe la FA England (Euro milioni moja), Ballon d'Or (Euro 508,000), Kombe la Mataifa Afrika - Afcon (Euro 127,000) na la Ligi Kuu Italia, Serie A (Euro 55,000).



KOMBE LA DUNIA QATAR 2022

# VIKOSI VYOTE 32 KOMBE LA DUNIA QATAR 2022

**Doha, Qatar**

WAKATI Kombe la Dunia 2022 likianza rasmi jana nchini Qatar, Argentina, Ureno na Brazil ni miongoni mwa timu zinazopewa nafasi ya kutwaa ubingwa huo, lakini hapa tunatazama vikosi vyote vya mataifa 32 vinavyoshiriki michuano hiyo mwaka huu...

**KUNDI A - Qatar, Ecuador, Senegal na Uholanzi**

**Qatar**

Makipa: Saad Al Sheeb (Al-Sadd), Meshaal Barsham (Al-Sadd) na Yousuf Hassan (Al-Gharafa).

Mabeki: Pedro Miguel (Al-Sadd), Musaab Khidir (Al-Sadd), Tarek Salman (Al-Sadd), Bassam Al Rawi (Al-Duhail), Boualem Khoukhi (Al-Sadd), Abdelkarim Hassan (Al-Sadd), Homam Al Amin (Al-Gharafa) na Jassim Gabir (Al-Arabi).

Viungo: Ali Asad (Al-Sadd), Assim Madibo (Al-Duhail), Mohammed Waad (Al-Sadd), Salem Al Hajri (Al-Sadd), Mustafa Meshaal (Al-Sadd), Karim Boudiaf (Al-Duhail), Abdulaziz Hatim (Al-Rayyan), Ismaeel na Mohammad (Al-Duhail).

Washambuliaji: Naif Al Hadhrami (Al-Rayyan), Ahmed Alaa (Al-Gharafa), Hassan Al Haydos (Al-Sadd), Khalid Muneer (Al-Wakrah), Akram Afif (Al-Sadd), Almoez Ali (Al-Duhail) na Mohammed Muntari (Al-Duhail).

**Ecuador**

Makipa: Moises Ramirez (Independiente del Valle), Alexander Dominguez (LDU Quito) na Hernan Galindez (Aucas).

Mabeki: Piero Hincapie (Bayer Leverkusen), Robert Arboleda (Sao Paulo), Pervis Estupinan (Brighton), Angelo Preciado (Genk), Jackson Porozo (Troyes), Xavier Arreaga (Seattle Sounders), Diego Palacios (Los Angeles FC), Felix Torres (Santos Laguna) na William Pacho (Royal Antwerp).

Viungo: Carlos Gruezo (Augsburg), Jose Cifuente (Los Angeles FC), Alan Franco (Talleres), Moises Caicedo (Brighton), Angel Mena (Club Leon), Jeremy Sarmiento (Brighton), Jhegson Mendez (Los Angeles FC), Ayrton Preciado (Santos Laguna), Gonzalo Plata (Real Valladolid) na Romario Ibarra (Santos Laguna).

Washambuliaji: Djorkaeff Reasco (Newell's Old Boys), Kevin Rodriguez (Imbabura), Michael Estrada (Cruz Azul) na Enner Valencia (Fenerbahce)

**Senegal**

Makipa: Seny Dieng (Queens Park Rangers), Alfred Gomis (Rennes) na Édouard Mendy (Chelsea)

Mabeki: Fodé Ballo-Touré (AC Milan), Pape Abou Cissé (Olympiacos), Abdou Diallo (Leipzig), Ismail Jakobs (Monaco), Kalidou Koulibaly (Chelsea), Formose Mendy (Amiens) na Youssouf Sabaly (Real Betis)

Viungo: Pathé Ciss (Rayo Vallecano), Krepin Diatta (Monaco), Idrissa Gueye (Everton), Pape Gueye (Marseille), Cheikhou Kouyaté (Nottingham Forest), Mamadou Loum (Reading), Nampalys Mendy (Leicester), Moustapha Name (Pafos) na Pape Matar Sarr (Tottenham)

Washambuliaji: Boulaye Dia (Salernitana), Famara Diedhiou (Alanyaspor), Bamba Dieng (Marseille), Nicolas Jackson (Villarreal), Iliman Ndiaye (Sheffield United) na Ismaïla Sarr (Watford)

**Uholanzi**

Makipa: Justin Bijlow (Feyenoord), Andries Noppert (Heerenveen) na Remko Pasveer (Ajax).

Mabeki: Nathan Ake (Manchester City), Daley Blind (Ajax), Virgil van Dijk (Liverpool), Denzel Dumfries (Inter Milan), Jeremie Frimpong (Bayer Leverkusen), Matthijs de Ligt (Bayern Munich), Tyrell Malacia (Manchester United), Jurrien Timber (Ajax) na Stefan de Vrij (Inter Milan).

Viungo: Steven Berghuis (Ajax), Frenkie de Jong (Barcelona), Davy Klaassen (Ajax), Teun Koopmeiners (Atalanta), Marten de Roon (Atalanta), Xavi Simons (PSV Eindhoven) na Kenneth Taylor (Ajax).

Washambuliaji: Steven Bergwijn (Ajax), Memphis Depay (Barcelona), Cody Gakpo (PSV), Vincent Janssen (Antwerp), Luuk de Jong (PSV), Noah Lang (Club Brugge) na Wout Weghorst (Besiktas).

**KUNDI B - England, Iran, USA na Wales**

**England**

Makipa: Jordan Pickford (Everton), Aaron Ramsdale (Arsenal) na Nick Pope (Newcastle).

Mabeki: Kieran Trippier (Newcastle), Trent Alexander-Arnold (Liverpool), Kyle Walker (Man City), Benjamin White (Arsenal), Harry Maguire (Man Utd), John Stones (Man City), Eric Dier (Tottenham), Conor Coady (Everton, kwa mkopo kutoka Wolves) na Luke Shaw (Man Utd).

Viungo: Declan Rice (West Ham), Jude Bellingham (Borussia Dortmund), Kalvin Phillips (Man City), Jordan Henderson (Liverpool), Conor Gallagher (Chelsea) na Mason Mount (Chelsea).

Washambuliaji: Harry Kane (Tottenham), Callum Wilson (Newcastle), Marcus Rashford (Man Utd), Raheem Sterling (Chelsea), Bukayo Saka (Arsenal), Phil Foden (Man City), Jack Grealish (Man City) na James Maddison (Leicester City)

**Iran**

Makipa: Alireza Beiranvand (Persepolis), Hossein Hosseini (Esteghlal), Payam Niazmand (Sepahan) na Amir Abedzadeh (Ponferradina).

Mabeki: Ramin Rezaeian (Sepahan), Abolfazl Jalali (Esteghlal), Hossein Kananizadegan (Al Ahli SC), Shoja Khalilzadeh (Al Ahli SC), Mortza Pouraliganji (Persepolis), Majid Hosseini (Kayserispor), Sadegh Moharrami (Dinamo Zagreb), Milad Mohammadi (AEK) na Ehsan Hajisafi (AEK).

Viungo: Saeid Ezatolahi (Vejle Boldklub), Ahmad Nourollahi (Shabab Al Ahli), Ali Karimi (Kayserispor), Rouzbeh Cheshmi (Esteghlal), Vahid Amiri (Persepolis), Mehdi Torabi (Persepolis), Alireza Jahanbakhsh (Feyenoord), Ali Gholizadeh (Charleroi) na Saman Ghoddos (Brentford).

Washambuliaji: Sardar Azmoun (Bayer Leverkusen), Karim Ansarifard (Omonia) na Mehdi Taremi (Porto).

**USA**

Makipa: Ethan Horvath (Luton), Sean Johnson (New York City) na Matt Turner (Arsenal)

Mabeki: Cameron Carter-Vickers (Celtic), Sergino Dest (AC Milan), Aaron Long (New York Red Bulls), Shaq Moore (Nashville), Tim Ream (Fulham), Antonee Robinson (Fulham), Joe Scally (Borussia Monchengladbach), DeAndre Yedlin (Miami) na Walker Zimmerman (Nashville)

Viungo: Brenden Aaronson (Leeds), Kellyn Acosta (Los Angeles), Tyler Adams (Leeds), Luca de la Torre (Celta Vigo), Weston McKennie (Juventus), Yunus Musah (Valencia) na Cristian Roldan (Seattle)

Washambuliaji: Jesus Ferreira (Dallas), Jordan Morris (Seattle), Christian Pulisic (Chelsea), Gio Reyna (Borussia Dortmund), Josh Sargent (Norwich), Tim Weah (Lille) na Haji Wright (Antalyspor)

**Wales**

Makipa: Wayne Hennessey (Nottingham Forest), Danny Ward (Leicester) na Adam Davies (Sheffield United).

Mabeki: Ben Davies (Tottenham), Ben Cabango (Swansea), Tom Lockyer (Luton), Joe Rodon (Rennes, on loan from Tottenham), Chris Mepham (Bournemouth), Ethan Ampadu (Spezia, on loan from Chelsea), Chris Gunter (AFC Wimbledon), Neco Williams (Nottingham Forest) na Connor Roberts (Burnley).

Viungo: Sorba Thomas (Huddersfield), Joe Allen (Swansea), Matthew Smith (MK Dons), Dylan Levitt (Dundee United), Harry Wilson (Fulham), Joe Morrell (Portsmouth), Jonny Williams (Swindon), Aaron Ramsey (Nice) na Rubin Colwill (Cardiff).

Washambuliaji: Gareth Bale (Los Angeles FC), Kieffer Moore (Bournemouth), Mark Harris (Cardiff), Brennan Johnson (Nottingham Forest) na Daniel James (Fulham).



**KUNDI C - Argentina, Saudi Arabia, Mexico na Poland**

**Argentina**

Makipa: Emiliano Martinez (Aston Villa), Franco Armani (River Plate) na Geronimo Rulli (Villarreal)

Mabeki: Gonzalo Montiel (Sevilla), Nahuel Molina (Atletico Madrid), German Pezzella (Real Betis), Cristian Romero (Tottenham Hotspur), Nicolas Otamendi (Benfica), Lisandro Martinez (Manchester United), Juan Foyth (Villarreal), Nicolas Tagliafico (Olympique Lyonnais) na Marcos Acuna (Sevilla)

Viungo: Leandro Paredes (Juventus), Guido Rodriguez (Real Betis), Enzo Fernandez (Benfica), Rodrigo De Paul (Atletico Madrid), Exequiel Palacios (Bayer Leverkusen), Alejandro Gomez (Sevilla) na Alexis Mac Allister (Brighton & Hove Albion)

Washambuliaji: Paulo Dybala (AS Roma), Lionel Messi (Paris St Germain), Angel Di Maria (Juventus), Nicolas Gonzalez (Fiorentina), Joaquin Correa (Inter Milan), Lautaro Martinez (Inter Milan) na Julian Alvarez (Manchester City).

**Saudi Arabia**

Makipa: Mohamed Al-Owais (Al-Hilal), Nawaf Al-Aqidi (Al-Nassr) na Mohamed Al-Yami (Al-Ahly).

Mabeki: Yasser Al-Shahrani (Al-Hilal), Ali Al-Bulaihi (Al-Hilal), Abdulelah Al-Amri (Al-Nassr), Abdullah Madu (Al-Nassr), Hassan Tambakti (Al-Shabab), Sultan Al-Ghanam (Al-Nassr), Mohammed Al-Breik (Al-Hilal) na Saud Abdulhamid (Al-Hilal).

Viungo: Salman Al-Faraj (Al-Hilal), Riyadh Sharahili (Abha), Ali Al-Hassan (Al-Nassr), Mohamed Kanno (Al-Hilal), Abdulelah Al-Malki (Al-Hilal), Sami Al-Najei (Al-Nassr), Abdullah Otayf (Al-Hilal), Nasser Al-Dawsari (Al-Hilal), Abdulrahman Al-Aboud (Ittihad), Salem Al-Dawsari (Al-Hilal) na Hattan Bahebri (Al-Shabab).

Washambuliaji: Nawaf Al-Abed (Al-Shabab), Haitham Asiri (Al-Ahly), Saleh Al-Shehri (Al-Hilal) na Firas Al-Buraikan (Al-Fateh).

**Mexico**

Makipa: Guillermo Ochoa (America), Alfredo Talavera (Juarez) na Rodolfo Cota (Leon).

Mabeki: Jorge Sanchez (Ajax), Kevin Alvarez (Pachuca), Nestor Araujo (America), Johan Vasquez (Cremonese), Hector Moreno (Monterrey), Cesar Montes (Monterrey), Gerardo Arteaga (Genk) na Jesus Gallardo (Monterrey).

Viungo: Andres Guardado (Real Betis), Hector Herrera (Houston Dynamo), Charly Rodriguez (Cruz Azul), Erick Gutierrez (PSV), Luis Chavez (Pachuca), Edson Alvarez (Ajax), Orbelin Pineda (AEK Athens) na Luis Romo (Monterrey).

Washambuliaji: Alexis Vega (Guadalajara), Hirving Lozano (Napoli), Raul Jimenez (Wolves), Roberto Alvarado (Guadalajara), Uriel Antuna (Cruz Azul), Henry Martin (America) na Rogelio Funes Mori (Monterrey).

**Poland**

Makipa: Bartlomiej Dragowski (Spezia), Lukasz Skorupski (Bologna) na Wojciech Szczesny (Juventus).

Mabeki: Jan Bednarek (Aston Villa), Bartosz Bereszynski (Sampdoria), Matty Cash (Aston Villa), Kamil Glik (Benevento), Robert Gumny (FC Augsburg), Artur Jedrzejczyk (Legia Warsaw), Jakub Kiwior (Spezia), Mateusz Wieteska (Clermont) na Nicola Zalewski (Roma).

Viungo: Krystian Bielik (Birmingham City), Przemyslaw Frankowski (Lens), Kamil Grosicki (Pogon Szczecin), Jakub Kaminski (VfL Wolfsburg), Grzegorz Krychowiak (Al-Shabab), Michal Skoras (Lech Poznan), Damian Szymanski (AEK Athens), Sebastian Szymanski (Feyenoord), Piotr Zielinski (Napoli) na Szymon Zurkowski (Fiorentina).

Washambuliaji: Robert Lewandowski (Barcelona), Arkadiusz Milik (Juventus), Krzysztof Piatek (Salernitana), Karol Swiderski (Charlotte FC).

**KUNDI D - Ufaransa, Australia, Denmark na Tunisia**

**UFARANSA**

Makipa: Alphonse Areola (West Ham), Hugo Lloris (Tottenham) na Steve Mandanda (Rennes).

Mabeki: Lucas Hernardez (Bayern Munich), Theo Hernandez (AC Milan), Ibrahima Konate (Liverpool), Jules Kounde (Barcelona), Benjamin Pavard (Bayern Munich), William Saliba (Arsenal), Dayot Upamencano (Bayern Munich) na Raphael Varane (Manchester United).

Viungo: Eduardo Camavinga (Real Madrid), Youssouf Fofana (Monaco), Matteo Guendouzi (Marseille), Adrien Rabiot (Juventus), Aurelien Tchouameni (Real Madrid) na Jordan Veretout (Marseille).

Washambuliaji: Karim Benzema (Real Madrid), Kingsley Coman (Bayern Munich), Ousmane Dembele (Barcelona), Olivier Giroud (AC Milan), Antoine Griezmann (Atletico Madrid), Kylian Mbappe (Paris Saint-Germain) na Christopher Nkunku (RB Leipzig).

**Australia**

Makipa: Mathew Ryan (FC Copenhagen), Andrew Redmayne (Sydney FC) na Danny Vukovic (Central Coast Mariners).

Mabeki: Aziz Behich (Dundee United), Milos Degenek (Columbus Crew), Thomas Deng (Aibirex Niigata), Joel King (Odense Boldklub), Nathaniel Atkinson (Hearts), Fran Karacic (Brescia), Harry Souttar (Stoke City), Kye Rowles (Hearts) na Craig Goodwin (Adelaide United).

Viungo: Aaron Mooy (Celtic), Jackson Irvine (St Pauli), Ajdin Hrustic (Hellas Verona), Bailey Wright (Sunderland), Cameron Devlin (Hearts), Riley McGree (Middlesbrough) na Keanu Baccus (St Mirren).

Wahsmbuliaji: Awer Mabil (Cadiz), Mathew Leckie (Melbourne City), Martin Boyle (Hibernian), James Maclaren (Melbourne City), Jason Cummings (Central Coast Mariners), Mitchell Duke (Fagiano Okayama) na Garang Kuol (Central Coast Mariners).

**Denmark**

Makipa: Kasper Schmeichel (Nice), Oliver Christensen (Hertha Berlin) na Frederik Ronnow (Union Berlin).

Mabeki: Simon Kjaer (AC Milan), Joachim Andersen (Crystal Palace), Joakim Maehle (Atalanta), Andreas Christensen (Barcelona), Rasmus Kristensen (Leeds United), Jens Stryger Larsen (Trabzonspor), Victor Nelsson (Galatasaray), Daniel Wass (Brondby) na Alexander Bah (Benfica).

Viungo: Thomas Delaney (Sevilla), Mathias Jensen (Brentford), Christian Eriksen (Manchester United), Pierre-Emile Hojbjerg (Tottenham), Robert Skov (Hoffenheim) na Christian Norgaard (Brentford).

Washambuliaji: Andreas Skov Olsen (Club Bruges), Jesper Lindstrom (Eintracht Frankfurt), Andreas Cornelius (Copenhagen), Martin Braithwaite (Espanyol), Kasper Dolberg (Sevilla), Mikkel Damsgaard (Brentford), Jonas Wind (VfL Wolfsburg) na Yussuf Poulsen (RB Leipzig).

Tunisia

Makipa: Aymen Dahmen (CS Sfaxien), Bechir Ben Said (US Monastir), Mouez Hassen (Club Africain) na Aymen Mathlouthi (Etoile Sahel).

Mabeki: Ali Abdi (Caen), Dylan Bronn (Salernitana), Mohamed Drager (FC Luzern), Nader Ghandri (Club Africain), Bilel Ifa (Kuwait SC), Wajdi Kechrida (Atromitos), Ali Maaloul (Al Ahly), Yassine Meriah (Esperance) na Montassar Talbi (Lorient).

Viungo: Mohamed Ali Ben Romdhane (Esperance), Ghaylane Chaalali (Esperance), Aissa Laidouni (Ferencvaros), Hannibal Mejbri (Birmingham City), Ferjani Sassi (Al Duhail) na Elyas Skhiri (FC Cologne).

Washambuliaji: Anis Ben Slimane (Brondby), Seifeddine Jaziri (Zamalek), Issam Jebali (Odense), Wahbi Khazri (Montpellier), Taha Yassine Khenissi (Kuwait SC), Youssef Msakni (Al Arabi) na Naim Sliti (Al Ittifaq).

**KUNDI E - Hispania, Costa Rica, Ujerumani na Japan**

**HISPANIA**

Makipa: Unai Simon (Athletic Club), Robert Sanchez (Brighton & Hove Albion) na David Raya (Brentford FC)

Mabeki: Cesar Azpilicueta (Chelsea FC), Dani Carvajal (Real Madrid), Eric Garcia (FC Barcelona), Hugo Guillamon (Valencia CF), Pau Torres (Villarreal CF), Aymeric Laporte (Manchester City), Jordi Alba (FC Barcelona) na Jose Gaya (Valencia CF).

Viungo: Sergio Busquets (FC Barcelona), Rodri Hernandez (Manchester City), Gavi (FC Barcelona), Carlos Soler (Paris St Germain), Marcos Llorente (Atletico de Madrid), Pedri Gonzalez (FC Barcelona) na Koke Resurreccion (Atletico de Madrid).

Washambuliaji: Ferran Torres (FC Barcelona), Nico Williams (Athletic Club), Yeremi Pino (Villarreal CF), Alvaro Morata (Atletico de Madrid), Marco Asensio (Real Madrid), Pablo Sarabia (Paris St Germain), Dani Olmo (RB Leipzig) na Ansu Fati (FC Barcelona).

**Costa Rica**

Makipa: Keylor Navas (Paris St-Germain), Esteban Alvarado (Herediano), Patrick Sequeira (CD Lugo).

Mabeki: Francisco Calvo (Konyaspor), Juan Pablo Vargas(Millonarios FC), Kendall Waston (Saprissa), Oscar Duarte (Al-Wehda), Daniel Chacon (Colorado Rapids), Keysher Fuller (Herediano), Carlos Martinez (San Carlos), Bryan Oviedo (Real Salt Lake) na Ronald Matarrita (Cincinnati).

Viungo: Yeltsin Tejeda (Herediano), Celso Borges (Alajuelense), Youstin Salas (Saprissa), Roan Wilson (Grecia), Gerson Torres (Herediano), Douglas Lopez (Herediano) Jewisson Bennette (Sunderland), Alvaro Zamora (Saprissa), Anthony Hernandez (Puntarenas FC), Brandon Aguilera (Nottingham Forest) na Bryan Ruiz (Alajuelense).

Washambuliaji: Joel Campbell (Leon), Anthony Contreras (Herediano) na Johan Venegas (Alajuelense).

**UJERUMANI**

Makipa: Manuel Neuer (Bayern Munich), Marc-Andre ter Stegen (Barcelona) na Kevin Trapp (Eintracht Frankfurt)

Mabeki: Matthias Ginter (Freiburg), Antonio Rudiger (Real Madrid), Niklas Suele (Borussia Dortmund), Nico Schlotterbeck (Borussia Dortmund), Thilo Kehrer (West Ham United), David Raum (RB Leipzig), Lukas Klostermann, Armel Bella Kotchap (Southampton) na Christian Guenter (Freiburg)

Viungo: Ilkay Gundogan (Manchester City), Jonas Hofmann (Borussia Monchengladbach), Leon Goretzka (Bayern Munich), Serge Gnabry (Bayern Munich), Leroy Sane (Bayern Munich), Jamal Musiala (Bayern Munich), Joshua Kimmich (Bayern Munich), Thomas Muller (Bayern Munich), Julian Brandt (Borussia Dortmund) na Mario Gotze (Eintracht Frankfurt)

Washambuliaji: Kai Havertz (Chelsea), Youssoufa Moukoko (Borussia Dortmund), Niklas Fuellkrug (Werder Bremen) na Karim Adeyemi (Borussia Dortmund)

**Japan**

Makipa: Eiji Kawashima (Strasbourg), Daniel Schmidt (Sint Truiden) na Shuichi Gonda (Shimizu S-Pulse)

Mabeki: Hiroki Sakai (Urawa Red Diamonds), Miki Yamane (Kawasaki Frontale), Ko Itakura (Borussia Monchengladbach), Takehiro Tomiyasu (Arsenal), Maya Yoshida (Schalke 04), Shogo Taniguchi (Kawasaki Frontale), Hiroki Ito (VfB Stuttgart) na Yuto Nagatomo (FC Tokyo)

Viungo: Junya Ito (Stade de Reims), Ritsu Doan (SC Freiburg), Wataru Endo (VfB Stuttgart), Hidemasa Morita (Sporting), Ao Tanaka (Fortuna Dusseldorf), Daichi Kamada (Eintracht Frankfurt), Gaku Shibasaki (Leganes) na Yuki Soma (Nagoya Grampus)

Washambuliaji: Takuma Asano (Vfl Bochum), Daizen Maeda (Celtic), Ayase Ueda (Cercle Brugge), Shuto Machino (Shonan Bellmare),Takefusa Kubo (Real Sociedad), Takumi Minamino (AS Monaco) na Kaoru Mitoma (Brighton & Hove Albion).

**KUNDI F - Ubelgiji, Canada, Morocco na Croatia**

INAENDELEA UK. 18

## Nukuu

"Kama ukichambua mpira wa miguu katika miaka 10/15 iliyopita, watu wawili wakuu wamekuwa Messi [Lionel] na Cristiano Ronaldo na, mwishowe, ukifikiria nani anastahili kushinda Kombe hili la Dunia, majina haya mawili yanajitokeza kila wakati. Ni magwiji,**" Nyota wa Timu ya Taifa ya Poland na Barcelona, Robert Lewandowski.**



"Kutoka wakati wangu kama mchezaji lazima nimtaje Van Basten, Baresi na Maldini. Kisha, kama kocha Ronaldo Nazario, Cristiano Ronaldo, Ibrahimovic [Zlatan], Benzema [Karim] na Vinicius [Junior]. Wapo wengi wao…,**" Kocha wa Real Madrid, Carlo Ancelotti akitaja wachezaji wakubwa aliocheza nao soka na aliowanoa akiwa Madrid.**



"Argentina inapewa nafasi zaidi miaka kwa minne iliyopita, hasa baada ya kutwaa taji la Copa America. Unapokuwa na Messi [Lionel], na kila mtu anaelewa ni lazima unakuwa na nafasi [ya kutwaa Kombe la Dunia],**"aliyekuwa Kocha wa Paris Saint-Germain, Mauricio Pochettino.**



# VIKOSI VYOTE 32 KOMBE LA DUNIA QATAR 2022

INATOKA UK. 17

**UBELGIJI**

Makipa: Thibaut Courtois (Real Madrid), Simon Mignolet (Club Brugge) na Koen Casteels (VfL Wolfsburg)

Mabeki: Jan Vertonghen (Anderlecht), Toby Alderweireld (Royal Antwerp), Wout Faes (Leicester), Arthur Theate (Rennes), Zeno Debast (Anderlecht), Thomas Meunier (Borussia Dortmund) na Timothy Castagne (Leicester).

Viungo: Kevin De Bruyne (Man City), Youri Tielemans (Leicester), Amadou Onana (Everton), Axel Witsel (Atletico Madrid), Hans Vanaken (Club Brugge), Leander Dendoncker (Aston Villa), Yannick Carrasco (Atletico Madrid) na Thorgan Hazard (Borussia Dortmund).

Washambuliaji: Eden Hazard (Real Madrid), Charles De Ketelaere (AC Milan), Leandro Trossard (Brighton), Dries Mertens (Galatasaray), Jeremy Doku (Rennes), Romelu Lukaku (Inter Milan), Michy Batshuayi (Fenerbahce) na Lois Openda (Lens).

**Canada**

Makipa: Milan Borjan (Red Star Belgrade), Dayne St Clair (Minnesota United) na James Pantemis (CF Montreal).

Mabeki: Steven Vitoria (Chaves), Alistair Johnston (CF Montreal), Richie Laryea (Nottingham Forest/Toronto FC on loan), Kamal Miller (CF Montreal), Sam Adekugbe (Hatayspor), Joel Waterman (CF Montreal) na Derek Cornelius (Panetolikos).

Viungo: Atiba Hutchinson (Besiktas), Jonathan Osorio (Toronto FC), Stephen Eustaquio (FC Porto), Liam Fraser (Deinze), Samuel Piette (CF Montreal), Mark-Anthony Kaye (Toronto FC), Ismael Kone (CF Montreal) na David Wotherspoon (St. Johnstone FC).

Washambuliaji: Alphonso Davies (Bayern Munich), Jonathan David (Lille), Cyle Larin (Club Brugge), Ike Ugbo (Troyes), Lucas Cavallini (Vancouver Whitecaps), Tajon Buchanan (Club Brugge), Junior Hoilett (Reading) na Liam Millar (Basel).

**Morocco**

Makipa: Yassine Bounou (Sevilla), Munir El Kajoui (Al Wehda), Ahmed Reda Tagnaouti (Wydad Casablanca).

Mabeki: Nayef Aguerd (West Ham United), Yahia Attiat Allah (Wydad Casablanca), Badr Benoun (Qatar SC), Achraf Dari (Stade Brest), Jawad El Yamiq (Real Valladolid), Achraf Hakimi (Paris Saint-Germain), Noussair Mazraoui (Bayern Munich) na Romain Saiss (Besiktas).



Viungo: Sofyan Amrabat (Fiorentina), Selim Amallah (Standard Liege), Bilal El Khannouss (Racing Genk), Yahya Jabrane (Wydad Casablanca), Azzedine Ounahi (Angers) na Abdelhamid Sabiri (Sampdoria).

Washambuliaji: Zakaria Aboukhlal (Toulouse), Soufiane Boufal (Angers), Ilias Chair (Queens Park Rangers), Walid Cheddira (Bari), Youssef En-Nesyri (Sevilla), Abde Ezzalzouli (Osasuna), Abderrazak Hamdallah (Al Ittihad), Amine Harit (Olympique Marseille) na Hakim Ziyech (Chelsea).

**Croatia**

Makipas: Dominik Livakovic (Dinamo Zagreb), Ivica Ivusic (Osijek) na Ivo Grbic (Atletico Madrid)

Mabeki: Domagoj Vida (AEK Athens), Dejan Lovren (Zenit Saint Petersburg), Borna Barisic (Rangers), Josip Juranovic (Celtic), Josko Gvardiol (RB Leipzig), Borna Sosa (Stuttgart), Josip Stanisic (Bayern Munich), Martin Erlic (Sassuolo) na Josip Sutalo (Dinamo Zagreb)

Viungo: Luka Modric (Real Madrid), Mateo Kovacic (Chelsea), Marcelo Brozovic (Inter Milan), Mario Pasalaic (Atalanta), Nikola Vlasic (Torino), Lovro Majer (Rennes), Kristijan Jakic (Eintracht Frankfurt) na Luka Sucic (Red Bull Salzburg)

Washambuliaji: Ivan Perisic (Tottenham), Andrej Kramaric (1899 Hoffenheim), Bruno Petkovic (Dinamo Zagreb), Mislav Orsic (Dinamo Zagreb), Ante Budimir (Osasuna) na Marko Livaja (Hajduk Split)

**KUNDI G - Brazil, Serbia, Uswisi na Cameroon**

**Brazil**

Makipa: Alisson (Liverpool), Ederson (Man City) na Weverton (Palmeiras)

Mabeki: Dani Alves (Pumas), Danilo (Juventus), Alex Sandro (Juventus), Alex Telles (Seville), Bremer (Juventus), Eder Militao (Real Madrid), Marquinhos (PSG) na Thiago Silva (Chelsea)

Viungo: Bruno Guimaraes (Newcastle), Casemiro (Manchester United), Everton Ribeiro (Flamengo), Fabinho (Liverpool), Fred (Manchester United) na Lucas Paqueta (West Ham)

Washambuliaji: Antony (Manchester United), Gabriel Jesus (Arsenal), Gabriel Martinelli (Arsenal), Neymar (PSG), Pedro (Flamengo), Raphinha (Barcelona), Richarlison (Tottenham), Rodrygo (Real Madrid) na Vinicius Jr (Real Madrid)

**Serbia**

Makipa: Marko Dmitrovic (Sevilla), Predrag Rajkovic (Mallorca) na Vanja Milinkovic-Savic (Torino).

Mabeki: Stefan Mitrovic (Getafe), Nikola Milenkovic (Fiorentina), Strahinja Pavlovic (Red Bull Salzburg), Milos Veljkovic (Werder Bremen), Filip Mladenovic (Legia Warsaw), Strahinja Erakovic (Red Star Belgrade) na Srdjan Babic (Almeria).

Viungo: Nemanja Gudelj (Sevilla), Sergej Milinkovic-Savic (Lazio), Sasa Lukic (Torino), Marko Grujic (Porto), Filip Kostic (Juventus), Uros Racic (Braga, on loan from Valencia), Nemanja Maksimovic (Getafe), Ivan Ilic (Hellas Verona), Andrija Zivkovic (PAOK) na Darko Lazovic (Hellas Verona).

Washambuliaji: Dusan Tadic (Ajax), Aleksandar Mitrovic (Fulham), Dusan Vlahovic (Juventus), Filip Duricic (Sampdoria), Luka Jovic (Fiortentina) na Nemanja Radonjic (Torino).

**USWISI**

Makipa: Gregor Kobel (Borussia Dortmund), Philipp Kohn (RB Salzburg), Jonas Omlin (Montpellier) na Yann Sommer (Borussia Monchengladbach)

Mabeki: Manuel Akanji (Manchester City), Eray Comert (Valencia), Nico Elvedi (Borussia Monchengladbach), Ricardo Rodriguez (Torino), Fabian Schar (Newcastle United) na Silvan Widmer (Mainz)

Viungo: Granit Xhaka (Arsenal), Edimilson Fernandes (Mainz), Fabian Frei (Basel), Remo Freuler (Nottingham Forest), Ardon Jashari (Luzern), Fabian Rieder (Young Boys), Xherdan Shaqiri (Chicago Fire), Djibril Sow (Eintracht Frankfurt), Renato Steffen (Lugano), Denis Zakaria (Chelsea) na Michel Aebischer (Bologna)

Washambuliaji: Breel Embolo (Monaco), Christian Fassnacht (Young Boys), Noah Okafor (RB Salzburg), Haris Seferovic (Galatasaray) na Ruben Vargas (Augsburg)

**Cameroon**

Makipa: Devis Epassy (Abha Club), Simon Ngapandouetnbu (Marseille) na Andre Onana (Inter Milan).

Mabeki: Jean-Charles Castelletto (Nantes), Enzo Ebosse (Udinese), Collins Fai (Al Tai), Olivier Mbaizo (Philadelphia Union), Nicolas Nkoulou (Aris Salonika), Tolo Nouhou (Seattle Sounders) na Christopher Wooh (Stade Rennes).

Viungo: Martin Hongla (Verona), Pierre Kunde (Olympiakos), Olivier Ntcham (Swansea City), Gael Ondoua (Hannover 96), Samuel Oum Gouet (Mechelen) na Andre-Frank Zambo Anguissa (Napoli).

Washambuliaji: Vincent Aboubakar (Al Nassr), Christian Bassogog (Shanghai Shenhua), Eric-Maxim Choupo Moting (Bayern Munich), Souaibou Marou (Coton Sport), Bryan Mbeumo (Brentford), Nicolas Moumi Ngamaleu (Young Boys Berne), Jerome Ngom (Colombe Dja), Georges-Kevin Nkoudou (Besiktas), Jean-Pierre Nsame (Young Boys Berne) na Karl Toko Ekambi (Lyon).

**KUNDI H - Ureno, Ghana, Uruguay na Korea Kusini**

**URENO**

Makipa: Diogo Costa (Porto), Jose Sa (Wolves) na Rui Patricio (Roma).

Mabeki: Diogo Dalot (Manchester United), Joao Cancelo (Manchester City), Danilo Pereira (PSG), Pepe (Porto), Ruben Dias (Manchester City), Antonio Silva (Benfica), Nuno Mendes (PSG) na Raphael Guerreiro (Borussia Dortmund).

Viungo: Joao Palhinha (Fulham), Ruben Neves (Wolves), Bernardo Silva (Manchester City), Bruno Fernandes (Manchester United), Joao Mario (Benfica), Matheus Nunes (Wolves), Otavio Monteiro (Porto), Vitinha (PSG) na William Carvalho (Real Betis).

Washambuliaji: Andre Silva (RB Leipzig), Cristiano Ronaldo (Manchester United), Goncalo Ramos (Benfica), Joao Felix (Atletico Madrid), Rafael Leao (AC Milan) na Ricardo Horta (Braga).

**Ghana**

Makipa: Manaf Nurudeen (Eupen), Danlad Ibrahim (Asante Kotoko) na Lawrence Ati Zigi (St Gallen).

Mabeki: Denis Odoi (Fulham), Tariq Lamptey (Brighton), Alidu Seidu (Clermont), Daniel Amartey (Leicester), Joseph Aidoo (Celta Vigo), Alexander Djiku (Strasbourg), Mohammed Salisu (Southampton) Abdul-Rahman Baba (Reading) na Gideon Mensah (Auxerre).

Viungo: Andre Ayew (Al-Sadd) Thomas Partey (Arsenal) Elisha Owusu (Gent), Salis Abdul Samed (Lens), Mohammed Kudus (Ajax) na Daniel Kofi Kyereh (Freiburg).

Washambuliaji: Daniel Barnieh Afriyie (Hearts of Oak), Kamal Sowah (Club Brugge), Issahaku Abdul Fatawu (Sporting Lisbon), Osman Bukari (Red Star Belgrade), Inaki Williams (Athletic Bilbao), Antoine Semenyo (Bristol City), Jordan Ayew (Crystal Palace)na Kamaldeen Sulemana (Rennes).

**Uruguay**

Makipa: Fernando Muslera (Galatasaray), Sergio Rochet (Nacional) na Sebastian Sosa (Independiente).

Mabeki: Ronald Araujo (Barcelona), Martin Caceres (LA Galaxy), Sebastian Coates (Sporting Lisbon), Jose Gimenez (Atletico Madrid), Diego Godin (Velez Sarsfield), Mathias Olivera (Napoli), Jose Rodriguez (Nacional), Guillermo Varela (Flamengo) na Matias Vina (Roma).

Viungo: Rodrigo Bentancur (Tottenham), Nicolas De Cruz (River Plate), Facundo Pellistri (Man Utd), Lucas Torreira (Galatasaray), Manuel Ugarte (Sporting Lisbon), Federico Valverde (Real Madrid) na Matias Vecino (Lazio).

Washambuliaji: Luis Suarez (Nacional), Darwin Nunez (Liverpool), Maxi Gomez (Trabzonspor), Edinson Cavani (Valencia), Agustin Canobbio (Athletico Paranense), Giorgian De Arrascaeta (Flamengo) na Facundo Torres (Orlando City).

**Korea Kusini**

Makipa: Kim Seung-gyu (Al Shabab), Jo Hyeon-woo (Ulsan Hyundai) na Song Bum-keun (Jeonbuk Motors)

Mabeki: Kim Min-jae (Napoli), Kim Jin-su (Jeonbuk Motors), Hong Chul (Daegu FC), Kim Moon-hwan (Jeonbuk Motors), Yoon Jong-gyu (FC Seoul), Kim Young-gwon (Ulsan Hyundai), Kim Tae-hwan (Ulsan Hyundai), Kwon Kyung-won (Gamba Osaka) na Cho Yu-min (Daejon Citizen)

Viungo: Jung Woo-young (Al Sadd), Na Sang-ho (FC Seoul), Paik Seung-ho (Jeonbuk Motors), Son Jun-ho (Shandong Taishan), Song Min-kyu (Jeonbuk Motors), Kwon Chang-hoon (Gimcheon Sangmu), Lee Jae-sung (Mainz), Hwang Hee-chan (Wolverhampton Wanderers), Hwang In-beom (Olympiacos), Jeong Woo-yeong (Freiburg) na Lee Kang-in (Real Mallorca)

Washambuliaji: Hwang Uijo (Olympiacos), Cho Gue-sung (Jeonbuk Motors) na Son Heung-min (Tottenham Hotspur)

Soka Bongo

# SIMBA KATIKA MKAKATI WA KUJIIMARISHA DIRISHA DOGO

**Na Adam Fungamwango**

SIMBA bado haichezi kama mashabiki wake wanavyotaka kama ilivyokuwa misimu minne mfululizo iliyopita. Inateswa na kiwango chake yenyewe ilichokiweka ilichosababisha itinge hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa mara mbili na Kombe la Shirikisho Afrika mara moja.

Kwa sasa wanachama na mashabiki wa Simba, pamoja na kwamba timu imepoteza mechi moja tu dhidi ya Azam, lakini bado hawaoni kama inaweza kwenda kufanya chochote kwenye Ligi ya Mabingwa hatua ya makundi.

Badala yake wanataka usajili ufanyike haraka sana kipindi cha dirisha dogo. Simba imeonekana kuwa na mapungufu makubwa kwenye baadhi ya maeneo kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo kushuka kwa viwango vya baadhi ya wachezaji, pamoja na baadhi ya nyota wapya iliyowaajili kutolipa.

Hivi majuzi Bodi ya Wakurugenzi ya klabu hiyo ilikaa kujadili mambo mbalimbali na taarifa za ndani zinasema kuwa moja ya maazimio ni kuhakikisha inasajili wachezaji watatu wa kimataifa kwa ajili ya kukiongezea nguvu kikosi chao.

Hata hivyo, ukiiangalia timu kiufundi unaona ili ifanye vema inahitaji wachezaji watano. Inawezekana ikawa watatu wa kimataifa na wawili wa ndani, lakini inahitaji idadi hiyo ya wachezaji wenye uwezo mkubwa kwa ajili ya kukibadilisha kikosi kiweze kuwa na uwezo wa kukabiliana na timu kubwa za Afrika.

**Mastraika wawili**

Simba inahitaji mastrika wawili asili si wenye uwezo mkubwa wa kufunga mabao tu, lakini wenye uwezo wa kukaa na mpira kwa sekunde kadhaa.

Kwa sasa haina straika wa aina hiyo, ikimtegemea zaidi Moses Phiri ambaye kiasili si mshambuliajii msaidizi.

Kuna taarifa za klabu hiyo kumleta Cesar Manzoki raia wa Jamhuri ya Kati mwenye asili ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo ambaye kwa sasa anacheza soka la kulipwa nchini China. Hata kama atajiunga na timu hiyo kipindi cha dirisha dogo, bado timu hiyo inahitaji straika mwingine ambaye atakuwa mbadala kama likitokea lolote lile, majeraha, kadi, au fatiki ya kucheza mechi nyingi.

Timu hiyo imeonekana inatengeneza nafasi nyingi, lakini zinashindwa kutumiwa vema kwa sababu haina straika asilia, badala yake inawatumia kina Phiri, mawinga na viungo washambuliaji kufunga.

Clatous Chama ambaye ndiye mpishi mkuu wa mabao wa timu hiyo, msimu huu hajafunga mabao mengi kwa sababu timu haina straika asilia.

Ikipata straika asilia na mwenye uwezo wa kukaa na mpira kama alivyokuwa Chris Mugalu wakati huo, anakuwa anachungwa na mabeki wawili na kiungo mkabaji mmoja, hii inawapa nafasi kina Chama kufanya wanavyotaka wakiwa ndani ya boksi.

Straika wa aina hiyo anaweza kuwahamisha mabeki hao kwenda nao pembeni, na kuwapa uhuru viungo kufunga mabao, lakini kukaa na mpira akiwasubiri kina Chama wasogee na kuwarudishia tena mipira kwenye maeneo ya hatari.

**Kiungo mkabaji**

Dirisha dogo timu hiyo viongozi hawatakiwi kufanya tena uzembe, badala yake kushusha kiungo mkabaji mwenye uwezo mkubwa wa kukaba, kuwalinda mabeki na kuzuia mashambulizi ya timu pinzani.

Kwa sasa Simba inawatumia Mzamiru Yassin na Sadio Kanoute, lakini kwenye hadhi ya Ligi ya Mabingwa wanatakiwa kuwa na kiungo mkabaji mwenye kiwango cha hali ya juu kuliko hao. Mzamiru na Kanoute wanatakiwa mmoja kumsaidia kiungo huyo na mwingine kukaa benchi akisubiri lolote kutokea.



Manzoki

Pia kiasili ukiwatazama wote hao si viungo wakabaji kama Gerson Fraga na Thadeo Lwanga, bali ni wasaidizi.

Eneo hilo kwa sababu ni la kugongana, lazima wachezaji wawe na kadi pamoja na majeruhi, hivyo kuwa na hao wawili tegemeo kuna wasiwasi sana kwa mashabiki kama mmoja akiumia au wote wawili.

Ukitazama timu zote kubwa za Afrika, zinakuwa na kiungo mkabaji asilia mwenye uwezo wa hali ya juu. Wataalamu wa masuala ya soka wanasema kama eneo hili tu litafanyiwa kazi, Simba inaweza kufika mbali kwenye Ligi ya Mabingwa kwa sababu ndilo huwa linawatesa zaidi hata ilipokuwa inatolewa hatua za robo fainali ya michuano ya kimataifa, eneo hili lilichangia sana kwa kuwa dhaifu.

**Kiungo mshambuliaji**

Anatakiwa mchezaji mwingine mwenye uwezo wa kutoa pasi za mwisho kama anavyofanya Chama. Ukweli ni kwamba Chama ni mmoja tu na hakuna mchezaji mwingine anayeweza kuwa kama yeye, lakini Simba inatakiwa kuwa na mbadala ambaye hata kama asipokuwapo kwa sababu zozote zile, wanachama na mashabiki wa Simba hawatowewseka.

Pamoja na timu kuwa na wachezaji zaidi ya 20, lakini asipokuwapo mchezaji huyo mashabiki wanakuwa na wasiwasi na kunakuwa na kweli, kwani hata ukiitazama timu haichezi vizuri na haitengenezi nafasi rahisi kama akiwapo.

Timu kubwa kama Simba inakuwa na michuano mingi kama Ligi ya Mabingwa, Ligi Kuu, Kombe la FA, hivyo haiwezekani imtegemee mchezaji mmoja kwenye michuano yote hiyo, badala yake anatakiwa kusajiliwa kiungo mwingine mshambuliaji mbunifu na mwenye jicho la pasi za mwisho.

**Beki wa kucheza kulia, kushoto**

Pia timu hiyo kwa sasa inatakiwa kusajili beki mmoja ambaye ana uwezo wa kucheza kulia na kushoto kwa ajili ya kuwasaidia Shomari Kapombe na Mohamed Hussein 'Tshabalala'.

Kwa misimu mitano mfululizo wachezaji hawa wamekuwa tegemeo kwenye michuano yote ambayo Simba imecheza tena mfululizo, hivyo kwa sasa wanahitaji kupumzika mara kwa mara kwa ajili ya kuondoa fatiki.

Anahitajia beki mwenye uwezo mkubwa ambaye akikaa sehemu yoyote kati ya hizo, mmoja anapumzika na wala mashabiki hawawi na wasiwasi au kukaa roho juu.

## NDANI YA 18



HADI kumalizika kwa hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu, Kylian Mbappe (PSG) na Mohamed Salah (Liverpool), ndio wanaongoza kwa kufunga mabao mengi kila mmoja akicheka na nyavu mara saba wakifuatiwa na Erling Haaland (Man City), Mehdi Taremi (Porto) na Robert Lewandowski (Barca) wenye mabao matano kila mmoja.

# MAMBO MA5 HUJUI KUHUSU DE BRUYNE

**LONDON, England**

KEVIN De Bruyne amebarikiwa na ustadi wa ajabu wa kucheza mpira. Winga huyo, katika kipindi cha wiki 10 zilizopita, amejidhihirisha kuwa kiungo bora zaidi barani Ulaya kwa sasa.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 26, katika ushindi wa mabao 2-0 wa Manchester City dhidi ya Leicester City, mapema mwezi huu, ulikuwa wa 50 katika mechi 76, na wa haraka zaidi kuliko kiungo mwingine yeyote katika historia ya Ligi Kuu England.

Akiwa na asisti 20 na mabao manne katika michuano yote msimu huu, De Bruyne ndiye mwanasoka bora zaidi kwenye Ligi Kuu England, kwa mujibu wa mchezaji mwenzake wa Ubelgiji, Eden Hazard.

Sasa, hebu tujue mambo matano yasiyojulikana sana kuhusu Kevin De Bruyne...

**#1. Angeweza kuichezea Burundi**

Ingawa De Bruyne alizaliwa huko Drongen nchini Ubelgiji, mizizi yake inaweza kufuatiliwa hadi Jamhuri ya Burundi, nchi isiyo na bandari katika eneo la Maziwa Makuu barani Afrika.

Anna De Bruyne, mamake Kevin, mtaalam wa Uhandisi wa Petroli, alizaliwa Burundi na alitumia muda mwingi wa miaka yake ya awali katika nchi hiyo ya Afrika Mashariki kabla ya kuhamia Ulaya baada ya ndoa yake na Herwig.

Anna pia aliishi Ealing, London Magharibi, kwa sababu ya kazi ya baba yake katika sekta ya mafuta. Kwa sababu ya ukoo wake, De Bruyne alistahili kuichezea Burundi, lakini akachagua kuwawakilisha 'Mashetani Wekundu' (Ubelgiji) badala yake.

Kiungo huyo anajua kwa ufasaha kabisa lugha nne, Kiholanzi, Kifaransa, Kijerumani na Kiingereza.

**#2. Jina lake la utani ni 'Kauzu'**

Licha ya uwezo wake wa ajabu dimbani, De Bruyne mara nyingi ndiye mchezaji aliyetulia zaidi uwanjani.

Mbelgiji huyo mara chache huonyesha hisia zake uwanjani na anashindwa hata baada ya kufunga mabao ya kuvutia.

Kwa hiyo, bila kujali ladha ya msimu, De Bruyne 'mnyenyekevu' anaendelea kuwa na tabia tulivu ndani na nje ya uwanja.

Hakuna kinachomsisimua zaidi ya kufunga mabao. De Bruyne huwa anajibu meseji za WhatsApp kwa kifupi sana na ndiyo maana marafiki zake humwita 'kauzu'.

**#3. Ana chapa ya nguo**

Mwanzoni mwa 2014, Kevin De Bruyne alikua balozi wa Olimpiki maalum. Mwaka uliofuata, aliamua kuwekeza katika mavazi kwa ushirikiano na Kampuni ya Cult Eleven.

Chapa hiyo inaitwa 'KDB' na sehemu ya faida inayotoka hapo huenda kwa shirika liitwalo Specials Olympics ambalo lina jukumu la kusaidia watu wenye mahitaji maalum kupitia mchezo ambao Kevin amekuwa akishiriki kwa muda.

Nyota wa kandanda, kwa sababu ya mvuto wao mkubwa wa kimataifa, daima hujitahidi kutafsiri umaarufu wao katika biashara zilizofanikiwa.

CR7 na Cristiano Ronaldo, A-Z na Zlatan Ibrahimovic na FIVE Supply na Rio Ferdinand ni baadhi ya chapa chache maarufu za nguo zinazomilikiwa na wanasoka.

**#4. Ana kitabu chake**

Kitabu cha wasifu wa Kevin De Bruyne, kinachoitwa 'Keep It Simple', kiliandikwa na Raoul de Groote, na kilitolewa Oktoba 2014.

De Bruyne alishiriki kikamilifu katika uandishi wa kitabu chake, ambacho kimeweka wazi maisha yake binafsi.

"Wakati wa maisha yake yote ya soka, Kevin De Bruyne amebaki mwenyewe; mvulana wa kawaida, ambaye anapenda 'kuweka kila kitu kuwa rahisi', katika maisha yake ya binafsi na uwanjani," inasomeka sehemu ya kitabu hicho.

Wazazi wa De Bruyne walifichua kuwa mtoto wao alipenda kurahisisha mambo, ndio maana ya kitabu hicho.

**#5. Yeye ni mcheshi, mkali**

Hili lingeshangaza, lakini kiungo mshambuliaji, ambaye alikuwa na pasi nyingi za mabao kuliko Cristiano Ronaldo msimu wa 2014-15, ni mtu anayependa mambo ya asili.

Hutumia vema wakati wake wa kutembelea nchi na kutazama wanyamapori. Aliteuliwa kuwa balozi wa hifadhi ya ndege ya Weltvogelpark mnamo Agosti 2014. Mahali patakatifu huko Walsrode, Ujerumani, ndio pakubwa zaidi ulimwenguni, nyumbani kwa aina tofauti 675 za ndege.

Alipoteuliwa, De Bruyne alisema: "Natumaini ninaweza kusaidia masaibu ya aina za ndege walio hatarini kutoweka na kuleta umakini zaidi kupitia ufadhili wangu."




**JE, WAJUA?**

WAKATI nyota wa Argentina, Lionel Messi, akishuka dimbani wiki hii kuichezea timu yake kwenye Kombe la Dunia nchini Qatar, atakuwa na nafasi ya kuvunja rekodi mbili za raia mwenza, Diego Maradona, katika michuano hiyo. Messi hadi sasa amecheza mechi 19 Kombe la Dunia, mbili pungufu ya Maradona, lakini mkongwe huyo aliyetangulia mbele za haki ana pasi za mwisho 'assists' nane alizotengeneza mwaka 1986 wakibeba ubingwa huo, ambazo ni tatu zaidi ya Messi.







# Mashamba 100 kufundishia wafugaji mbinu bora

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

WIZARA ya Mifugo imetenga mashamba 100 yatakayotumika kama mashamba darasa ya kuwafundisha wafugaji mbinu bora za ufugaji.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alitoa kauli hiyo jana kwenye mkutano wa nane wa mwaka Bodi za Maji za Mabonde unaofanyika kitaifa jijini hapo.

Alisema lengo la mashamba hayo ni kuwafundisha wafugaji kuachana na ufugaji wa kuhamahama unaoharibu mazingira na badala yake watumie ardhi kidogo kufuga kisasa.

Alisema mashamba hayo yatakwenda sambamba na kilimo cha malisho ya mifugo ili kuepuka uchungaji holela unaosababisha uharibifu wa mazingira na vyanzo vya maji.

Ulega alisema, zimeshaandaliwa tani mbili za mbegu bora za malisho katika Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI), kituo cha Uyole ili kuwapatia wafugaji wazitumie kuandaa malisho yatakayoboresha afya za mifugo ikiwamo ng'ombe.

Alisema jitihada hizo zina lengo la kuongeza ufanisi na upatikanaji wa mbegu bora za mifugo na malisho kwa ajili ya kukuza sekta ya nyama nchini.

"Wizara ya Mifugo ni moja ya kisekta zinazotekeleza mkakati wa kukabiliana na tatizo la uhaba wa maji nchini, ufugaji holela unachangia uharibifu wa vyanzo vya maji hivyo kwa mwaka 2022/2023, tumejipanga kutoa elimu ya ufugaji wa kisasa na kuhamasisha matumizi ya dawa na chanjo ya mifugo," alisema Ulega.

Hivi karibuni Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vicent Anney, aliiomba serikali kuajiri Ofisa Mifugo wilayani humo ili awapatie elimu bora ya ufugaji itakayowasaidia kukabiliana na magonjwa.

Alisema kwa sasa wafugaji wanakosa mbinu za ufugaji wa kisasa na kusababisha kuzalisha maziwa yasiyokuwa na ubora.



Daktari wa Mifupa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya, Moshi Shaban (kulia), akijadiliana jambo na mmoja wa vijana washiriki wa kongamano la wanaume katika Mkoa wa Mbeya la Broo Funguka ambalo limewakutanisha kwa ajili ya kujadili masuala mbalimbali yanayowakabili ikiwamo ukatili wa kijinsia na namna bora ya kujikwamua kiuchumi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Waomba taa za barabarani wafanye biashara usiku

**Na Grace Mwakalinga,**
RUNGWE

WAFANYABIASHARA wa Soko la Tandale, Kata ya Kiwira Wilaya ya Rungwe, wameiomba serikali kuboresha miundombinu ya taa za barabarani ili kuondokana na adha ya kutumia vibatari na mishumaa kufanya biashara nyakati za usiku.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, walisema kuwa soko hilo limekuwa tegemezi kwa wananchi hususani wasafiri wanaokwenda maeneo mbalimbali kupitia barabara ya Mbeya-Kyela mpaka nchi jirani ya Malawi.

Abigael Tuntufye, mfanyabiashara wa ndizi alisema kutokana na umuhimu wa soko hilo maarufu kama (Lembuka), serikali iwasaidie kuboresha miundombinu kama vile taa za barabara pamoja na eneo la kuhifadhi taka ambalo kuna mrundikano mkubwa wa taka zinazozalishwa sokoni hapo.

"Uwapo wa soko hili umetusaidia sana sisi kinamama kuendesha maisha yetu kwa miaka saba nilifanya biashara hii kuendesha maisha yangu tunaomba tuwekewe miundombinu ya kutuwezesha kufanya biashara zetu," alisema Abigael.

Mfanyabiashara wa parachichi, Devitha Solomon, alisema licha ya miundombinu ya taa pia kuna kikwazo cha mfereji wa kutiririsha maji na kuleta tatizo kubwa msimu wa mvua.

"Tunaomba serikali itusaidie kuboresha mazingira yetu ya wajasiriamali kwa kutuboreshea maeneo ya kufanya biashara kabla ya msimu wa mvua kuanza kwani kumekuwapo na adha ya maji kutuama na kutengeneza madimbwi," alisema Devitha.

Diwani wa Kata ya Kiwira, Michael Mwamwimbe, alikiri kuwapo kwa vikwazo hivyo na alishawasilisha kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe kwa ajili ya taratibu za utekelezaji.

Alisema soko hilo ni tegemeo kubwa kwa wananchi wa Rungwe na maeneo mengine, wanaomba serikali kuharakisha utekelezaji wa kufunga taa ili wafanyabiashara watoe huduma usiku na mchana.

"Hapa wanauza kwa kutumia vibatari na taa zinazotumia betri zinazotengenezwa nchini China ili kupata mwanga na kuendelea kutoa huduma kwa wananchi," alisema.

Akizungumza suala hilo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Rungwe mkoani hapa, Lenatus Mchau, alisema mpango wa kufunga taa uko hatua za mwisho na tayari wameshafanya mazungumzo na Shirika la Umeme (TANESCO) kwa ajili ya kutengeneza miundombinu.

"Tayari tumeweka kwenye mpango na utekelezaji wake ambao unatarajiwa kuanza hivi karibuni lengo ni kuona wafanyabiashara wanauza usiku na mchana ili kukuza kipato na kuchangia mapato ya serikali," alisema.

Kuhusu suala la taka alisema kuna tatizo la magari na halmashauri imeweka mikakati ya kununua gari la kuzoa taka ambalo litakuwa mwarobaini wa kuondokana na hadha ya mrundikano wa taka na kuondolewa kwa wakati.

# DC apiga marufuku uuzaji, unywaji pombe asubuhi

**Na Grace Mwakalinga,**
RUNGWE

MKUU wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vicent Anney, amepiga marufuku unywaji wa pombe nyakati za asubuhi kutokana na kukithiri kwa matukio ya ubakaji, uhalifu na wizi wa mazao.

Dk. Anney alitoa kauli hiyo alipozungumza na Nipashe baada ya kuwapo na matangazo katika maeneo mbalimbali wilayani humo yakionesha kupigwa marufuku matumizi ya pombe na uuzwaji.

"Baada ya mimi kutoa agizo kwa watendaji wa kata, mitaa na vijiji ndio mnaona hayo matangazo kwani kuliibuka matukio mengi ya ubakaji, uhalifu na wizi wa mazao ya wakulima hususan ndizi mashambani," alisema. Dk. Anney.

"Nimepokea malalamiko ya wananchi wakihusisha matukio hayo yanatokana na vijana kuacha shughuli za kilimo na kuendekeza matumizi ya pombe kuanzia alfajiri mpaka jioni."

Alisema kutokana na malalamiko hayo ya wananchi alianza kufanya uchunguzi na kuagiza Jeshi la Polisi kufanya msako ambao umezaa matunda na matukio ya ubakaji, uhalifu yamepungua.

Dk. Anney alisema awali matukio hayo yalitikisa na kutishia hali katika sekta ya kilimo na elimu kwa kuwa kumekuwapo na wanafunzi wanaotembea umbali mrefu kufuata elimu.

Baadhi ya wakazi wa Tandale Mji wa Tukuyu, walisema kitendo cha serikali kupiga marufuku ulevi muda wa kazi kumerejesha hali ya usalama.

Subilaga Mwakyusa, alisema walijenga hofu kutokana na kushamiri kwa matukio ya wizi wa mazao na mali nyingine kwenye makazi ya watu na kwamba marufuku ya unywaji wa pombe nyakati za asubuhi itasaidia vitendo hivyo kupungua au kukoma.

Joshua Saimon, aliomba kuwapo utaratibu wa doria kwa kushirikiana na wananchi ili kudhibiti matukio ya uhalifu hususan wafanyabiashara kufunga maeneo ya vilevi kwa muda uliopangwa na serikali na sio kukesha.





# Vigogo waanguka uchaguzi CCM

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SURA mpya za wenyeviti wa mikoa na wajumbe wa Baraza Kuu la Jumuiya ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) zimeingia kwa kiwango kikubwa kwenye uchaguzi uliofanyika ngazi ya mikoa mwishoni mwa wiki, zikiwaangusha waliokuwa wakitetea nafasi zao.

Miongoni mwa mikoa yenye sura mpya ni Dodoma ambapo aliyekuwa Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Dk. Damas Mukasa, alishindwa kwa kupata kura 192 huku Samwel Malecela akiibuka mshindi kwenye nafasi hiyo kwa kupata kura 480.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapo kuhusu uchaguzi wa nafasi mbalimbali za jumuiya hiyo ngazi ya taifa utakaofanyika Novemba 24-25 mwaka huu jijini Dodoma, Katibu Mkuu wa Jumuiya hiyo, Gilbert Kalima alisema uchaguzi uliofanyika Novemba 18 mwaka huu kwenye mikoa mbalimbali, wengi wa waliokuwa wakitetea nafasi za uenyekiti na ujumbe wa Baraza Kuu la Jumuiya hiyo hawakushinda.

"Uchaguzi uliofanyika umekwenda vizuri na kwa ujumla wake umefanyika vizuri lakini kwa taarifa za juu juu ni kwamba katika mikoa mingi wale waliokuwa wanashika nafasi hizo hasa kwa wenyeviti na Baraza Kuu Taifa wamedondoka, hivyo tunaweza kuwa na sura nyingi katika nafasi hizo kwa kipindi cha miaka mitano inayokuja yaani sura mpya," alisema.

Kalima alisema kuanguka huko huenda kumesababishwa na kutofanya vizuri kwenye nafasi zao miaka mitano iliyopita.

"Pia inawezekana wajumbe wametaka kufanya mabadiliko tu kuona kwamba tubadilishe aina ya uongozi katika maeneo husika ili kuongeza kasi ya utekelezaji au uimarishaji wa chama na jumuiya," alisema.

Alisema hadi sasa hajapokea malalamiko kwenye uchaguzi uliofanyika na kwamba kama yapo, kanuni zinaruhusu mgombea kulalamika vitendo ambavyo vilijitokeza ndani ya siku 14 na yakijitokeza yatashughulikiwa.

Aliwataka viongozi waliochaguliwa kutambua wajumbe wamewaamini kwa nafasi husika ili kuimarisha jumuiya na kuunda timu ya ushindi kuelekea uchaguzi wa mwaka 2024 na 2025.

"Nafasi walizopewa tutahukumiwa kwa miaka mitano ijayo kutokana na matendo tutakayokuwa tunayafanya. Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba tumeshika nafasi hizi kubwa kuimarisha umoja ndani ya chama na jumuiya zetu.

"Na pili kuimarisha chama kuelekea uchaguzi wa mwaka 2024 na 2025, pia kuhakikisha ilani ya uchaguzi ya chama chetu inatekelezwa kikamilifu," alisema.

Kuhusu uchaguzi ngazi ya taifa, katibu huyo alisema mkutano mkuu wa 10 wa jumuiya hiyo utafanyika Dodoma Novemba 24-25 mwaka huu na kutakuwa na wajumbe 893 kutoka mikoa yote nchini watakaoshiriki kuchagua viongozi wa jumuiya hiyo.

"Viongozi wanaotarajiwa kuchaguliwa ngazi ya taifa ni nafasi ya Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo ngazi ya taifa, ambaye atakuwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM.

"Nafasi nyingine ni Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya ambaye atakuwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa kwa nafasi yake, zingine ni nafasi tano za wajumbe wa NEC, ambapo tatu kutoka Tanzania Bara na mbili Zanzibar.

"Pia kutakuwa na wajumbe wa Baraza Kuu la Wazazi Taifa ambapo nafasi sita zitagombewa pamoja na uwakilishi wa jumuiya zingine ngazi ya taifa," alisema.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyumule (aliyevaa gauni la zambarau), akicheza na wanawake pamoja mabinti baada ya kufungua kongamano la kuwainua kiuchumi, kiroho na kijamii lililoandaliwa na Mchungaji Josephin Kihonza jijini Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Waziri aagiza kuanzishwa kozi biashara mafuta, gesi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

NAIBU Waziri, Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, ameagiza Chuo cha Biashara (CBE) kuanzisha kozi ya masuala ya uwekezaji na biashara ya mafuta na gesi kwa kuwa ni biashara kubwa kwa sasa duniani.

Akizungumza juzi kwenye mahafali ya 57 ya chuo hicho Kampasi ya Dodoma, Kigahe alisema biashara hiyo ni mhimili mkubwa wa uchumi nchini na nje ya mipaka ya Tanzania katika miaka michache ijayo na kutaka ianzishwe shahada ya masuala hayo yatakayokuwa na mchango mkubwa kwa nchi.

Alisema chuo hicho katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM, kinatakiwa kuchochea uchumi wa viwanda kwa maendeleo ya watu.

"Pamoja na kusambaza huduma za chuo, uwezo wa kujiendesha angalau kwa faida lazima uzingatiwe, ubora wa kimiundombinu uzingatiwe sana, chuo sasa kianze kufikiria kuanzisha kozi za masuala ya kiuwekezaji na biashara nzima ya mafuta na gesi, maendeleo ya viwanda bado ni taaluma ngeni kwa Watanzania wengi. CBE inaweza kuwa kinara wa utoaji wa mafunzo kuhusu uchumi wa viwanda katika ngazi mbalimbali," aliagiza. Alisema viwanda ni jambo kubwa la kibiashara, hivyo ni muhimu kwa chuo hicho kuamka na kutambua Tanzania ya viwanda inategemea mchango wao wa kutoa elimu sahihi ya kuchangia sekta hiyo.

"Shahada za uzamili zinaweza kuwa na wigo mpana zaidi wa kuibuka na shahada za aina hiyo kwenye maeneo bobezi kama sheria zinazotawala biashara ya mafuta na gesi, utawala wa viwanda, uendeshaji wa mashirika, uongozi, masuala ya sekta isiyo rasmi, yaani biashara ndogo na za kati, ujasiriamali ni muhimu sana kuzingatia," aliagiza.

Naibu waziri huyo alisema wahitimu wa chuo hicho wameiva kutokana na CBE kuwa mahali sahihi pa kujenga nidhamu na umahiri wa kitaaluma.

Alishukuru serikali za Finland, India na Poland kwa kuwa mstari wa mbele kukisaidia chuo hicho na kuwa na historia ya ushirikiano mwema kwa muda mrefu.

## Chuo cha Mifugo kujengwa Songwe

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi kupitia Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (LITA), imeingia makubaliano ya ushirikiano na Chuo cha Shandong cha China kwa ajili ya masuala mbalimbali ikiwamo kujenga chuo cha mifugo mkoani Songwe.

Akizungumza jana jijini hapo wakati wa kutia saini mkataba huo, Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Charles Mhina alitaja maeneo mengine ya ushirikiano huo ni pamoja na kubadilishana mitaala, wanafunzi na wakufunzi ili kuongeza ubora wa wataalamu katika sekta ya mifugo.

Dk. Mhina alisema katika uhusiano huo ambao tayari wameyaanza tangu mwaka 2021, walikubaliana na walikuwa na rasimu ya mkataba kwamba waanzishe kituo cha mafunzo ndani ya LITA.

Alisema baada ya kutia saini nyaraka hizo, sasa wamefungua rasmi uanzishwaji wa kituo hicho ambacho kitakuwa cha kisasa.

"Ushirikiano wetu unalenga kuboresha uhusiano katika utekelezaji, kuna maeneo yatahusika ikiwamo kuijengea uwezo LITA pamoja na kuboresha ufundishaji katika matawi yote na kuongeza uwezo wa walimu kutoa mafunzo, tuna mengi ya kujifunza kutoka kwa Wachina.

"Tunadhani kwa ushirikiano huu, tutafungua wigo wa kushirikiana zaidi na kuboresha, baada ya hili tunaamini na taasisi zetu zingine nazo zitajifunza," alisema.

Mtendaji Mkuu wa Wakala huo, Dk. Pius Mwambene, alisema walianza mazungumzo na chuo hicho mwaka 2019 kwa msaada mkubwa wa Balozi wa Tanzania China, Mberwa Kairuki.

"Alijaribu kutuunganisha hasa katika sekta kuu ya kilimo, bahati nzuri tuliwapata na mwaka 2021 tulitia saini makubaliano katika kutoa mafunzo," alisema.

Dk. Mwambene alisema mafunzo wanayotoa ni ya kuwatengeneza vijana wataalamu wa mifugo ambao wanakwenda kuwa watoa huduma katika ngazi ya kijiji, kata na wilaya kama maofisa mifugo wasaidizi.

Alisema baada ya kuanzisha uhusiano huo, wameendelea kuangalia maeneo ambayo wanaanza nayo na wamekubaliana kuanzisha chuo hicho.

Alisema wameandaa mkataba wa kujenga chuo hicho ndani ya miaka mitatu katika Mkoa wa Songwe na kitafundisha vijana hao.

"Pia kitatumika kuwaandaa vijana ambao watakuwa tayari kwenda kusoma China kwa mwaka wa tatu, hapa watasoma kwa miaka miwili halafu mwaka wa tatu watakwenda kuumalizia China. Tunashukuru Serikali ya China na tunategemea kujenga chuo ambacho kitakuwa cha mfano," alisema.



## Mariamu Mwinyi akipigia chapuo kilimo cha mwani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKE wa Rais wa Zanzibar, Mama Mariamu Mwinyi, amesema kilimo cha zao la mwani kina manufaa makubwa kwa afya na uchumi wa Wazanzibari.

Alisema hayo juzi Ikulu ndogo Migombani Zanzibar, alipozungumza na mabalozi wanawake wanaoiwakilisha Tanzania katika mataifa mbalimbali duniani.

Mama Mariyam ambaye ni Mwenyekiti wa Taasisi ya Maisha Bora (ZMBF), alisema wastani wa asilimia 80 ya wakuliwa wa kilimo cha mwani ni wanawake, huku akibainisha malengo ya kuliongezea thamani zao hilo ili kuleta tija kwa wakulima na taifa.

Alisema changamoto zinazowakabili walengwa wa programu ya miaka mitatu ya taasisi yake ikiwamo inayowalenga wanawake, vijana na watoto ni kukabiliana na vitendo vya udhalilishaji na ukatili wa kijinsia pamoja na azma ya kuwapatia taulo za kike wanafunzi wa kike walioko shuleni.

Alisema pamoja na juhudi kubwa zinazochukuliwa na serikali kukabiliana na vitendo vya udhalilishaji, bado hali sio nzuri, kutokana na wimbi kubwa la vitendo hivyo nchini, huku tatizo hilo likichangiwa kwa kiasi kikubwa na jamii kutokana na aibu pamoja na muhali.

Aidha, alisema kumekuwa na juhudi za kuimarisha afya za vijana kwa kufanya mazoezi, lengo likiwa ni kuhakikisha taifa linakuwa na wananchi wenye uwezo wa kufanya kazi.

Mama Mariam alieleza kuwa ZMBF ipo katika juhudi za kukabiliana na vifo vya mama na watoto kupitia programu yenye lengo la kuielimisha jamii umuhimu wa lishe bora kwa watoto.

"Malengo yameelekezwa kwa watoto hususan walio chini ya umri wa miaka mitano, huku mkazo ukiwekwa katika uimarishaji wa afya ya mama kabla ya uzazi," alisema.

Amidi wa mabalozi hao, Balozi Asha Rose Migoro, alipongeza juhudi zinazochukuliwa na taaasisi ya ZMBF na kuahidi kushirikiana na washirika wa maendeleo katika nchi wanazofanyia kazi ili kufanikisha malengo ya taasisi.

Alisema takriban nchi zote zenye uwakilishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, zimeweka vipaumbele katika ushughulikiaji wa masuala ambayo ZMBF imelenga kuyatekeleza.

# Hospitali Mkoa kumaliza msongamano Mnazi Mmoja

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KUKAMILIKA kwa ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Mjini Magharib Unguja iliyoko Lumumba kutapunguza msongamano wa wagonjwa wanaofika Hospitali ya Rufani Mnazi Mmoja kupata matibabu.

Akizungumza jana wakati akikagua ujenzi wa jengo la hospitali hiyo unaoendelea kujengwa, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alisema ameridhishwa hatua zilizofikiwa za ujenzi huo.

Dk. Mwinyi alisema amefurahishwa na kasi ya mkandarasi anayeendeleza mradi huo, hadi sasa hatua za ujenzi zimefikia asilimia 69 na Aprili mwakani jengo hilo litaanza kutoa huduma za afya.

"Kuna kila sababu ya kujivunia kwa uwapo wa hospitali hii ambayo ni ya aina yake hapa Zanzibar," alisema Dk. Mwinyi.

Alisema hospitali hiyo itakuwa mbadala katika kuendeleza tiba na kupisha ukarabati mkubwa unaotarajiwa kufanyika katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Hospitali la Lumumba ni miongoni mwa zinazojengwa katika mikoa yote ya Zanzibar na gharama za ujenzi zinatokana na fedha za ahuweni za UVIKO-19.

Aidha, Dk. Mwinyi aliwatoa hofu wajasiriamali wanaojihusisha na kazi za kutengeneza vyombo vya moto (gereji) ambao wamelazimika kusimamisha shughuli zao na kuhama eneo hilo ili kupisha ujenzi wa hospitali hiyo ya Lumumba.

Alisema tathmini kwa ajili ya malipo yao tayari imefanyika na wanatarajiwa kulipwa katika kipindi kifupi kijacho ili kuendelea na kazi zao katika eneo lingine walilopangiwa.

Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, alisema hospitali hiyo ilitarajiwa kukamilika Januari 2023, lakini baadhi ya vifaa vilivyotarajiwa kutumika vilichelewa kufika nchini.

Alisema kwa sasa mahitaji mengi ya vifaa yameshakamilika na mafundi wanaendelea na ujenzi.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi (wa pili kulia), akipata maelezo ya maendeleo ya ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja kutoka kwa Waziri wa Afya Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, inayojengwa katika eneo la Lumumba Wilaya ya Mjini Unguja. **PICHA: IKULU**

# Othman ataka vijana kutumia vyema fursa za ajira

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman, amewataka vijana kuzitumia vyema fursa za kutengeneza ajira zinazoanzishwa na serikali ili kufikia ndoto zao za kuwa na ajira za uhakika kwa maendeleo ya taifa.

Aliyasema hayo jana Tunguu visiwani humo, alipozungumza katika kongamano la vijana la ndoto ajira lililowakutanisha kutoka ndani na nje ya Tanzania.

Othman alisema ukosefu wa ajira kwa vijana ni moja ya changamoto kubwa za kijamii inayozikabili nchi nyingi duniani na zaidi barani Afrika, kwa kiasi kikubwa inachangiwa na mitazamo ya vijana kutegemea kuajiriwa serikalini.

Alisema tamasha hilo la ndoto ajira ni fursa kubwa kwa vijana wa Afrika Mashariki kujionea namna wanavyowasilisha mawazo yao na ubunifu walionao katika nyanja za biashara na sekta ya uchumi wa buluu ili kutimiza malengo yao ya kujiajiri na kuondokana na mawazo ya kuajiriwa serikalini kama fursa pekee ya ajira.

Aidha, alisema serikali imeunda chombo cha wakala wa uwezeshaji wananchi kiuchumi ili kuwasaidia vijana kutimiza ndoto zao kwa kupatiwa mafunzo ya ujasiriamali, mikopo na kutafutiwa masoko kwa bidhaa wanazozalisha na kusaidia kukuza pato kwa vijana.


Alisema serikali kupitia taasisi zake na kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo imeandaa programu maalum za kuwawezesha vijana kwa kuwakuza ujuzi kupitia shule na vyuo vya ufundi, vituo vya uwezeshaji ili kuingia katika soko la ajira, kujikwamua kiuchumi na kupunguza tatizo la ajira.

"Kufanya hivyo ni jitihada maalumu za kutafuta suluhisho muhimu la tatizo la ajira kwa kuwaandaa vyema vijana wenye elimu sahihi, ujuzi na maarifa ya kazi kwa kujiajiri na kutimiza ndoto yao ya ajira," alisema.

Alisema serikali inafahamu vyema kundi kubwa la vijana linapaswa kuangaliwa vyema kwa mtazamo wa aina yake kwa lengo la kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika shughuli za kukuza uchumi na kuleta maendeleo nchini.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Suraga, alisema ukosefu wa ajira kwa vijana ni kilio cha muda mrefu na ndoto- ajira wamekuja na mtazamo mpya kuhusu changamoto hiyo kwa vijana.

Alisema vijana wanaweza kuzitumia fursa mbalimbali zinazoanzishwa katika jitihada za kuwa wabunifu, kutumia elimu na maarifa wanayopatiwa na hatimaye kupata mafanikio katika jitihada zao za kuleta maendeleo.





# Watoa ushuhuda madhila walioozeshwa umri mdogo

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WANAFUNZI wa Shule ya Sekondari Nyikoboko, Kata ya Shilela Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama mkoani Shinyanga wameeleza masikitiko dhidi ya wenzao walioshindwa kumaliza masomo kutokana na kuozeshwa katika umri mdogo.

Ndoa za utotoni zipo wilayani humo kwa kile kinachoelezwa wazazi kuwashinikiza watoto wao kufanya vibaya kwenye mitihani ya kitaifa ili waoelewe na hivyo kupata fedha na mifugo.

Walibainisha hayo jana wakati wa kujengewa uwezo namna ya kukabiliana na vitendo vya kikatili wa kijinsia na kutengeneza mpango kazi na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) katika Shule ya Msingi Shilela, Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama mkoani Shinyanga.

Mwanafunzi wa Kidato cha Tatu, Othumani Oswadi alisema mwenzao alipata ujauzito wakiwa kidato cha pili na kujifungua kwa upasuaji, mtoto yupo salama lakini mama alipata maradhi anayohangaika nayo hadi sasa.

Alisema mwanafunzi mwingine alifaulu kujiunga na Shule ya Sekondari Mwalimu Nyerere, lakini wazazi wake walikataa kumsomesha wakidai hawana fedha kumbe walitaka kumwozesha na walipotoa taarifa polisi, mpango wao ukashindikana na sasa anaendelea vema na masomo yake.

Mwanafunzi wa Kidato cha Tatu, Salumu Mashaka alisema wakiwa kidato cha pili, mwanafunzi mwenzao alipata ujauzito na kushindwa kuendelea na masomo na hivi karibuni walishiriki kwenye sherehe yake ya kutolewa mahari na ameolewa na mtu mzima, hivyo kukatisha ndoto zake.

"Sisi kwa sasa tumeingiwa na wasiwasi wa wanafunzi wenzetu wa kike kushindwa kuhitimu masomo yao kwa kuendelea kupata ujauzito, tuwaombe TGNP kwa kushirikana na serikali kutokomeza tabia hii inayokatisha ndoto za dada zetu," alisema Mashaka.

Mwalimu wa Taalumu Shule ye Sekondari Mwalimu Nyerere, John Banda, alikiri kuwapo tatizo la wanafunzi kupata ujauzito na kushindwa kuendelea na masomo yao, akirejea taarifa za Januari mwaka huu iliripotiwa kesi ya mwanafunzi wa kidato cha tatu kupata ujauzito.

Alisema kuwa mwaka jana mwanafunzi alifanya mtihani wa kidato cha pili akiwa mjamzito bila uongozi wa shule kujua na alifaulu kuingia kidato cha tatu, lakini alishindwa kuendelea na masomo.

Mwakilishi wa Kituo cha Taarifa na Maarifa, Joseph Samwel alisema Kata ya Shilela kila mwezi wanatembelea vijijini kutoa elimu ya ukatili na ndoa za utotoni na wanapobaini tatizo wanaripoti kwenye vyombo vya sheria.

Mtaalamu wa Jinsia na Maendeleo wa TGNP, Hancy Obote, alisema lengo la kukutana na wanafunzi hao ni kuwashawishi kuwa sehemu ya harakati za kukomesha ukatili wa kijinsia kwa kuwaelimisha kuhusu madhara ya ukatili wa kijinsia na wasaidie kuunga mkono juhudi za wasichana katika kupambana na ukatili.



Mwanafunzi wa kidato cha pili Shule ya Sekondari Nyikoboko iliyoko Kata ya Shilela Msalala wilayani Kahama, Joseph Masanja, akieleza namna wanafunzi wa kike wanavyofanyiwa vitendo vya kikatili shuleni na mitaani wakati wakipewa elimu ya kupambana na ukatili wa kijinsia na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Wananchi Kahama wamilikishwa ardhi

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

MKOA wa Shinyanga umegawa hati miliki 500 za viwanja katika Wilaya ya Kahama kwa lengo la kuongeza thamani ya ardhi na wananchi kumiliki kisheria.

Mwishoni mwa wiki katika eneo la mradi wa viwanja la Sunu, Kata ya Nyahanga, Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Shinyanga, Leo Komba, alibainisha hayo wakati wa utoaji wa hati kwa wananchi.

Alisema wananchi wengi hawana mwamko wa kushughulikia hati za umiliki za viwanja na kuwataka ambao hawana kufuatilia ili wawe na umiliki na kutambulika kwenye nyaraka ambazo zitawasaidia kupata huduma sehemu mbalimbali.

"Tumeanzia Wilaya ya Kahama na tunafanya kazi hii muda wa siku mbili na tukimaliza tunahamia wilaya nyingine, tunataka kazi hii iwe endelevu na kila mtu apate hati ya kiwanja," alisema.

Komba alisema zipo hati 220 ambazo zinafanyiwa mchakato kupitia utaratibu huo ili kusogeza huduma hiyo karibu na wananchi na kuwapunguzia kero ya kusafiri kwenda mkoani kupata huduma hiyo.

Msajili wa Hati Msaidizi mkoani Shinyanga, Emanuel Gwaltu, alisema mwitikio wa wananchi ni mkubwa na kwamba hati zote zilizokamilika zitakabidhiwa kwa wahusika.

Alisema faida ya kuwa na hati ni kutambulika kwa eneo ambalo mtu analimiliki na pia anaweza kupata mikopo kwenye taasisi za kifedha na hivyo kujiendeleza kiuchumi.

Mmoja wa wananchi waliokabidhiwa hati miliki, Juma Ramadhani alisema amefurahi kwa kuwa hakuwahi kutarajia kumiliki ardhi kisheria na ataitumia kwa manufaa ya kiuchumi.

Alisema utaratibu wa kuwafuata wananchi walioko utaondoa urasimu na usumbufu wanaoupata wananchi kwenda mkoani na kuepuka gharama za ziada.

# Madiwani wapewa jukumu kuukabili uvuvi haramu

**Na Lilian Lugakingira,** MULEBA

MADIWANI wa Halmashauri ya Muleba mkoani Kagera wanaotoka katika kata za mwambao na visiwa vya Ziwa Victoria, wametakiwa kuwa mfano na kutumia nyadhifa zao kudhibiti uvuvi haramu unaofanywa na wananchi wao.

Katibu Tawala Wilaya ya Muleba, Greyson Mwengu, alitoa rai hiyo kwa wanasiasa hao wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani mwishoni mwa wiki.

Alisema uvuvi haramu bado upo, hivyo madiwani ambao wako karibu na wananchi, wanaweza kuwa na taarifa nyingi zaidi ikiwamo kuelimisha jamii kuachana na vitendo hivyo.

"Uvuvi ni uchumi, kuvua kwa njia haramu ni kuharibu mazalia ya samaki ziwani na anayetetea hilo ajue mwisho wa siku samaki wataisha, tukabakia na maji ya kuoga na kupikia, ikifikia hatua hiyo mtakaogeukiwa ni nyie madiwani kuwa hamfai," alihadharisha.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Muleba, Stewart Butondo, aliwataka viongozi, watendaji na wananchi kuendelea kutoa taarifa za watu wanaojihusisha na vitendo hivyo, ili wakamatwe na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Diwani wa Bumbile, Winchislaus Balongo alithibitisha kuwapo kwa uvuvi haramu maeneo mengi na vitendo hivyo vinafanyika usiku wa manani, hivyo akaoimba serikali kuongeza nguvu kwenye kutoa elimu na kuchukua hatua stahiki.

Diwani wa Nyakabango, Pastory Rwanchele, alisema wanaendelea kuhamasisha wavuvi walioko kwenye vikundi ili wanufaike na huduma mbalimbali ikiwamo mikopo ya serikali, jambo litakalowasaidia kununua zana za kisasa na kufanya uvuvi endelevu.

HABARI KIMATAIFA

# EU yakataa pendekezo la Misri

**SHARM EL-SHEIKH,** Misri

MAZUNGUMZO ya hali ya hewa ya Umoja wa Mataifa (UN) hayakwenda vizuri baada ya Umoja wa Ulaya (EU) kukataa pendekezo la Misri juu ya kupunguzwa uzalishaji wa gesi chafu na kuonya kuwa ni bora kuondoka bila makubaliano yoyote kuliko kuwa na makubaliano mabaya.

Hayo yalijiri mwishoni mwa wiki iliyopita katika mkutano wa COP27 unaoendelea nchini Mistri, ambapo takriban wawakilishi 200 wa nchi wamekusanyika kwa lengo la kusukuma mbele hatua za kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa wakati dunia ikikabiliwa na hali mbaya ya hewa.

**Pia inaelezwa kuwa umoja huo wenye mataifa wanachama 27 bado una matumaini ya kupata ma-**

Pia ilielezwa kuwa mazungumzo hayo yalikwama kutokana na wito kwamba mataifa tajiri wachafuzi wa hewa wanatoa ufadhili wa hasara na uharibifu kwa nchi zilizokumbwa na majanga ya hali ya hewa, na pia juu ya matarajio ya kukabiliana na ongezeko la joto duniani.

Baada ya mashauriano kurefushwa kufuatia siku rasmi ya mwisho iliyokuwa Ijumaa, Umoja wa Ulaya ulikataa rasimu ya waraka kutoka Misri.

Makamu wa Rais wa kamisheni ya Ulaya, Frans Timmermans, alisema EU ni bora ikose matokeo mbadala kuliko kuwa na matokeo mabaya, huku ikibainishwa kuwa walikuwa tayari kuondoka kwenye mazungumzo hayo kabisa.

Pia inaelezwa kuwa umoja huo wenye mataifa wanachama 27 bado una matumaini ya kupata matokeo mazuri.

EU inataka COP27 kuwa na matamshi makali juu ya kupunguza uzalishaji wa gesi chafu na kuthibitisha lengo la matarajio ya kupunguza ongezeko la joto duniani hadi nyuzi joto 1.5 kutoka viwango vya kabla ya viwanda. **VOA**

## Kampuni ya Elon Musk kuzindua mtandao Tanzania

HUDUMA ya mtandao ya Elon Musk ya Starlink inatarajiwa kupatikana nchini Tanzania katika robo ya kwanza ya 2023, huku wachambuzi wakisema maendeleo hayo mapya yatakuza uchumi wa kidijitali.

Kwa mujibu wa BBC, huduma hiyo, ambayo inamilikiwa na Kampuni ya SpaceX, imekuwa ikitoa muunganisho wa intaneti kwa kutumia maelfu ya satelaiti angani ambazo huwasiliana na vipitishio vilivyoteuliwa vya ardhini.

Wadau mbalimbali, walisema kuwa huduma hiyo mpya itachochea sekta ya kidijitali iwapo itauzwa kwa bei nafuu na kutoa mtandao wa kasi.

Kwenye tovuti yao rasmi, Starlink ilitangaza mpango wao wa kuleta huduma hizo kati ya mwezi Januari na Machi kulingana na idhini ya udhibiti.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Dk. Jabiri Bakari, alithibitisha kuwa Kampuni ya Starlink ilituma maombi.

Alipoulizwa iwapo anafahamu kuhusu kuwasili kwa Starlink Corporation, Dk. Bakari alijibu "Ndiyo, ninafahamu kuwa kampuni hiyo ilituma maombi kupitia tovuti".

Mataifa pekee ya Kiafrika ambayo hadi sasa yameiruhusu Starlink kufanya kazi ni Nigeria na Msumbiji.

Hii ilifanyika baada ya kupata vibali vya udhibiti kutoka kwa mataifa yote mawili.

Ikiwa Starlink itakuwa na athari kubwa au laa, itategemea jinsi biashara hiyo inatarajia kutoa huduma kwa haraka na kwa bei nafuu, kulingana na mwanauchumi Abel Kinyondo kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

"Huduma ya mtandao sio anasa bali ni hitaji la msingi. Kasi yake ya juu na uwezo wake wa kumudu inaweza kumaanisha kasi kubwa na upatikanaji wa haraka wa habari," alisema.**BBC**



Waziri Mkuu wa Uingereza, Rishi Sunak, akisalimiana na Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, baada ya kuwasili nchini humo juzi kwa ziara ya kushtukiza. **PICHA: AFP**

## Waziri Mkuu Sunak atembelea Ukraine

**LONDON,** Uingereza

KWA mara ya kwanza tangu aingie madarakani, Waziri Mkuu wa Uingereza, Rishi Sunak, amefanya ziara ya kiserikali mjini Kyiv nchini Ukraine na kukutana na Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, na kumthibitishia uungaji mkono wa Uingereza kwa Ukraine.

Kwa mujibu wa RFI, Rais wa Ukraine Zelensky, ndiye ambaye alitangaza ziara ya kushtukiza ya waziri wa Uingereza Sunak mjini Kyiv.

Rais wa Ukraine, Zelensky aliandika kwenye Telegram kuwa tangu siku za kwanza za vita, Ukraine na Uingereza zimekuwa washirika wa nguvu.

Katika video iliyotolewa na ofisi ya rais wa Ukraine waziri mkuu wa Uingereza Sunak, alimhakikishia Rais wa Ukraine kwamba taifa lake litaindelea kumuunga mkono.

"Niko hapa leo kusema kwamba Uingereza itaendelea kukuunga mkono, tutashirikiana nanyi hadi Ukraine itakapopata amani na usalama inayohitaji na inayostahili," alisema.

"Ni somo kubwa la unyenyekevu kuwa nanyi katika nchi yenu leo, ujasiri wa raia wa Ukraine ni msukumo kwa ulimwengu, tutawaambia wajukuu wetu historia yenu, jinsi watu wenye ujasiri na wakuu wamesimama dhidi ya shambulio baya, jinsi ulivyopigana, ulivyojitolea na ulivyoshinda," alisema.

Pia London, ilisema kuwa Sunak amesafiri kwenda Kyiv kuthibitisha uungaji mkono wa Uingereza kwa Ukraine.

"Waziri Mkuu yuko Ukraine leo 'jana' katika ziara yake ya kwanza huko Kyiv kukutana na Rais Zelensky na kuthibitisha uungaji mkono wa Uingereza unaoendelea," ilisema.

Pia waziri huyo alisema nchi yake inajua maana ya kupigania uhuru, huku akimwahidi Rais wa Ukraine kuwa wako pamoja na yeye siku zote.

Vile vile inaelezwa kuwa katika hafla ya ziara hiyo ya kushtukiza, Waziri Sunak, aliahidi kuipa Ukraine pauni milioni 50 ambazo ni sawa na Euro milioni 57, kwa ajili ya zana za kijeshi zitakazotumika dhidi ya mashambulizi ya angani nchini Ukraine. **RFI**

## COP27 yaidhinisha mfuko kuzisaidia nchi maskini

**SHARM EL-SHEIKH,** Misri

WAJUMBE katika mkutano wa Umoja wa Mataifa kuhusu mazingira wa COP27 wamefikia makubaliano ya kihistoria ambayo yataanzisha mfuko maalum wa kuzifidia nchi maskini ambazo zinaathiriwa zaidi na mabadiliko ya tabianchi.

Makubaliano ya kuundwa kwa mfuko wa kuzifidia nchi maskini zinazoathiriwa na uchafuzi wa gesi ya kaboni unaosababishwa na nchi tajiri, yalifikiwa jana asubuhi katika kikao cha mashauriano kwenye mkutano huo unaofanyika nchini Misri.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Misri, Sameh Shoukry ambaye ni Rais wa COP27, alipendekeza kuanzishwa kwa mfuko huo Jumamosi mchana na kufikiwa na pande husika siku hiyo hiyo, ambapo ilipofika jana aliyatangaza rasmi makubaliano hayo.

Pia inaelezwa kwamba, makubaliano makubwa bado hayajafikiwa kutokana na mvutano ulioko kuhusu juhudi za kupunguza matumizi ya gesi ya kaboni inayochafua mazingira. **DW**

# RC aagiza kufutwa kazi ofisa mtendaji wa kijiji

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Fatma Mwassa, amemwagiza Katibu Tawala wa Wilaya ya Morogoro kushirikiana na Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Morogoro kuchukua hatua ya kumfuta kazi mara moja Ofisa Mtendaji wa Kijiji Lubasazi, Kata ya Kolelo.

Ofisa mtendaji huyo ambaye jina lake halikupatikana mara moja, anatuhumiwa na wananchi kupokea rushwa kutoka kwa wafugaji ili waingize mifugo kwenye maeneo ya Kijiji cha Lubasazi.

Mwassa alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki baada ya kutokea vifo vya watu wawili wa jamii ya wafugaji na wengine watano kujeruhiwa kutokana na vurugu zilizozuka baina ya wakulima na wafugaji katika Kijiji cha Lubasazi, Kata ya Kolelo.

Kutokana na mgogoro huo, kiongozi huyo aliagiza kuwafuta kazi mara moja mtendaji wa kijiji hicho pamoja na mwenyekiti wake kutokana na kutuhumiwa kupokea rushwa kutoka kwa wafugaji.

Mkuu wa Mkoa pia aliwataka wakulima kutojichukulia sheria mikononi kwenye matukio kama hayo badala yake watoe taarifa kwenye mamlaka husika na wafugaji kutochungia mifugo yao kwenye mashamba au maeneo ya wakulima.

"Hakuna sheria inayomtaka mwananchi kuchukua sheria mkononi ya kuua mwenzake eti kwa sababu kaingia mahali fulani, na kwa sababu hiyo ndiyo maana tuliwakamata waliofanya tukio hilo na watafunguliwa mashtaka," alionya.

Mwassa pia aliwataka wafugaji kufuata sheria na kuacha kuingiza mifugo yao kwenye mashamba ya wakulima na wataokwenda kinyume chake, hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao, pia kwa wakulima wasiotii sheria za nchi.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Morogoro, Fortunatus Musilimu, alithibitisha kutokea kwa mauaji hayo Novemba 15, mwaka huu, baada ya kundi la watu 40 waliokuwa na silaha za jadi, kuvamia kambi ya wafugaji katika Kitongoji cha Kivumba katika kijiji hicho.

Kamanda Musilimu aliwataja waliofariki dunia kutokana na vurugu hizo ni Saito Molinge (50) na Salum Sambigu (40), wote wakazi wa Kitongoji cha Sangasanga, Kata ya Mvuha wilayani Morogoro.

Alisema chanzo cha tukio hilo ni wafugaji kuvamia eneo la wakulima, kitendo ambacho kilipingwa na wakazi wa eneo hilo ambao wengi wao ni wakulima na hivyo waliamua kuwashambulia kwa lengo la kuwaondoa.

## Mpango aguswa jitihada za NBC ustawishaji viwanda

**Na John Badi**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango ameipongeza Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) kwa mchango wake mkubwa katika kustawisha sekta ya viwanda nchini kupitia huduma zake mbalimbali za kifedha zinazosaidia kukuza na kuongeza ufanisi wa uzalishaji katika sekta hiyo.

Akizungumza kwenye hafla ya utoaji wa Tuzo za 16 za Rais kwa Vinara wa Uzalishaji Viwandani (PMAYA) iliyofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Dk. Mpango aliyemwakilisha Rais Samia Suluhu, alisema mchango wa taasisi za kifedha ni muhimu katika kukuza sekta ya viwanda na kuongeza ushindani katika soko la ndani na nje ya nchi.

"Kama ambavyo wadau wenyewe wa sekta ya viwanda wanavyowaita Benki ya NBC mshirika muhimu wa sekta ya viwanda, na mimi pia kwa niaba ya serikali ninawapongeza NBC pamoja na wadau wengine wote kwa kuwa pamoja na sekta hii muhimu.

Awali akizungumza kwenye hafla ya tuzo hizo zilizoratibwa na Shirikisho la Wenye Viwanda nchini (CTI), Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi alisema mafanikio makubwa ambayo benki hiyo inayapata kwa kiasi kikubwa yanachagizwa na dhamira thabiti pamoja na jitihada za serikali katika kujenga Tanzania inayoondeshwa na uchumi wa viwanda na biashara.

Kwa mujibu wa Sabi, kupitia uwekezaji mkubwa katika huduma za kidigitali, benki hiyo sasa imefanikiwa kurahisisha utoaji wa huduma zake kwa wateja wote wakiwamo wamiliki wa viwanda ambao kwa sasa hawalazimiki kutembelea matawi ya benki hiyo ili kupata huduma kwa kuwa wanaweza kukamilisha huduma zote muhimu za benki hiyo wakiwa kwenye biashara zao kupitia huduma za kidigitali.

"Mbali na ufanisi katika utoaji wa huduma, pia tunajivunia ushirikiano wetu na wadau wote wakubwa na wadogo kibiashara kupitia 'NBC Biashara Clubs' zilizoko maeneo mbalimbali nchini.




Kamishna wa Walipakodi Wakubwa wa Mamlaka ya Mapato nchini, Alfred Mregi (kushoto), akimkabidhi Tuzo ya Mlipakodi Bora, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya ujenzi ya Nanovas, Dk. Alfred Msemo, baada ya kuibuka mlipakodi bora wilayani Ilala jijini Dar es Salaam, katika hafla iliyofanyika mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Vodacom yazindua kampeni ikitoa fursa msimu wa sikukuu

**Na Halfan Chusi**

KAMPUNI ya Mawasiliano ya Vodacom Tanzania imezindua promosheni ya wiki nane ya msimu wa sikukuu iliyoipa jina la 'Amsha Ndoto, Amsha Shangwe' ikilenga kuwapa wateja wake fursa ya kujishindia zawadi mbalimbali zikiwamo fedha.

Vilevile, imesema wateja watakuwa na nafasi ya kujishindia zawadi mbalimbali zikiwamo simujanja, televisheni za kisasa, vipanganjia (Router) vya 5G, bima ya VodaBima na kupata fursa ya kusafiri bila malipo kupitia Paisha.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania Plc, Philip Besiimire, alisema Vodacom imekuwa na utamaduni wa kuwatunuku zawadi mbalimbali wateja wake katika msimu wa sikukuu na kuainisha jinsi ambavyo kampuni inathamini mchango wao.

Alisema wateja wa kampuni hiyo wanaweza kushiriki kwenye promosheni hiyo na kujishindia zawadi mbalimbali kwa kulipia bidhaa mbalimbali kupitia M-Pesa, kufanya ununuzi na miamala kupitia huduma hiyo katika kipindi hiki cha sikukuu.

Alisema miamala yote itakayofanyika kupitia M-Pesa kwa kipindi hiki cha promosheni itaingia kwenye droo na kumpa mteja nafasi ya kushinda zawadi mbalimbali.

"Msimu wa sikukuu ni muhimu na una hamasa kwetu sote. Tunapata fursa ya kupumzika na kuwa na wapendwa wetu, pia kutafakari mafanikio yetu ya mwaka wakati tunaweka malengo ya mwaka ujao.

"Kipindi hiki kwa kawaida tuna utaratibu wa kununulia ndugu na jamaa na kuwapelekea zawadi lakini zawadi zingine huwa tunawanunulia wanafamilia wetu, na sisi kama Vodacom, familia yetu ni wateja wetu na ndiyo sababu ndani ya miaka michache iliyopita tulianzisha utaratibu wa kuwapa zawadi wateja wetu ili kufanya msimu huu wa sikukuu uwe wa furaha zaidi kwao," alisema.

Besiimire alisema Vodacom ina matumaini ya kusaidia kufanikisha ndoto za wateja wake hasa katika kipindi hiki cha msimu wa sikukuu, akiwahimiza wateja wa Vodacom kutumia M-Pesa kufanya miamala na kujiongezea nafasi za kushinda zawadi kubwa.

"Inawezekana ulitaka kumiliki gari, kuanzisha biashara, kulipa ada ya shule, kumalizia ujenzi wa nyumba au kwenda kupumzika, sisi Vodacom tungependa kukusaidia kufanikisha ndoto yako.

# Aslay kurudi upya

Na Mwandishi Wetu

NYOTA wa Bongo Fleva, Isihaka Nassoro 'Aslay', rasmi ametangazwa kujiunga na Sony Music Entertainment Africa baada ya muda mrefu kupita bila ya msanii huyo kusikika akitamba kama ilivyokuwa hapo awali.

Aslay, ameingia kwenye kampuni hiyo kutokana na kupotea kwake kwenye muziki kwa kipindi kirefu bila ya kubainisha hadharani kilichosababisha nyota huyo kukaa kimya, hatua hiyo ilisababisha kuibuka kwa uvumi wa namna mbalimbali kutoka kwa mashabiki.

Baada ya Aslay kujiunga rasmi na Sony Music, Mkuu wa Sony Music Ukanda ya Afrika Mashariki, Christine 'Seven' Mosha, aliweka bayana hisia zake juu ya nyota huyo na kile ambacho wamekipanga katika kuhakikisha talanta yake inaendelea kukua na kufika mbali zaidi.

"Ninajivunia kuwa na msanii wa hadhi ya Aslay kuungana nasi Sony Music Africa, Aslay ni mwimbaji na mtunzi wa kipekee ambaye ameongoza aina ya muziki wa Bongo Fleva kote barani Afrika na sasa ulimwenguni kote, tunafurahi kushirikiana naye kuleta talanta yake ya ajabu na muziki masikioni mwa mashabiki wengi tuwezavyo ulimwenguni," alisema Seven.

Aslay anatajwa kama mmoja wa wasanii wenye umri mdogo aliyefanikiwa kujizolea idadi kubwa ya mashabiki wa kila umri barani Afrika kutokana na umahiri wake katika muziki na mpaka sasa nyota huyo ana jumla ya wafuasi milioni tano kwenye ukurasa wake wa Instagram, milioni mbili kwenye ukurasa wake wa Facebook, pamoja na wafuasi wasiopungua milioni moja kwenye chaneli yake ya YouTube.

"Napenda kuwaambia mashabiki wangu kuna kazi mpya zinakuja kwa hiyo kaeni tayari kwa album, kaeni tayari kwa nyimbo, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu, nachoweza kusema ni kuwaambia tu watu ambao wanapenda kuona Aslay anafika mbali wategemee kazi nzuri kutoka kwangu nishaingia mzigoni kwa hiyo hakuna mambo mabaya, sasa hivi tutegemee vitu vizuri," alisema Aslay.



# ZUCHU ALIA KUKOSA MASHABIKI MAREKANI



Na Mwandishi Wetu

MSANI wa Bongo Fleva, Zuhura Othman maarufu Zuchu, kupitia ukurasa wake wa Instagram amewashukuru mashabiki wake wote waliojitokeza kwenye shoo yake huko Houston, Texas nchini Marekani, licha ya shoo hiyo kutokwenda kama alivyotarajia.

Zuchu amesema kwamba kilichotokea kimempa hasira ya kufanya zaidi na anakubali kushindwa ikiwa kama sehemu ya mafanikio yake.

"Nimejiuliza sana kwa nini nilichagua kazi hii ya muziki, lakini kwa matukio kama haya yananipa majibu kwamba wachache hutolewa kama mfano ili ije kuwa rahisi kwa wengine," alisema Zuchu.

Katika shoo hiyo, Zuchu alikosa kabisa mashabiki, kwani waliohudhuria walikuwa wachache mno.

# Stara Thomas hataki kiki

Na Mwandishi Wetu

MSANII mkongwe wa Bongo Fleva, Stara Thomas, amesema kwa umri alionao hawezi kufanya kiki.

Stara amesema, kiki zinazofanyika zinahitaji mtu ujichetue vilivyo jambo ambalo kwake haliwezi kuwa la heshima.

"Mimi nina watoto, sasa hizo kiki unatakiwa kweli ufanye mambo ya ovyo kabisa hivyo siwezi kwa kweli," alisema Stara.

Alisema, amekuwa akifanya muziki wake kwa kufanya miradi na makampuni mbalimbali, lakini ni muda kidogo hajaingia studio kufanya nyimbo mpya.



# CHAMA ATAJWA KUIVURUGA RUVU SHOOTING KIPIGO SIMBA

**Na Adam Fungamwango**

GOLIKIPA wa Timu ya Ruvu Shooting, Hassan Masalanga, amemvulia kofia kiungo mshambuliaji wa Simba raia wa Zambia, Clatous Chama, akisema ndiye mchezaji aliyewavuruga na kusababisha kufungwa mabao 4-0 kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa juzi usiku katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza baada ya mechi hiyo, Masalanga alisema yeyote aliyeangalia mpira ataona kabisa kuwa sababu ya kufungwa idadi kubwa ya mabao kwa kiasi kikubwa imechangiwa na Chama ambaye alitoa pasi za mwisho kwenye bao la pili lililofungwa na John Bocco na la tatu lililowekwa wavuni na Shomari Kapombe, kwani ni mchezaji ambaye hakabiki kwa urahisi.

"Si mnaona aliyetuvuruga, ni Chama, jamaa katuvuruga kweli, kaachwa uwanja mzima anacheza yeye, hakabiki kwa sababu hakai sehemu moja, yaani unaweza kumnyang'anya mpira kama ukiwa naye karibu tu, vinginevyo hakabiki. Unajua ni ngumu sana kumkaba mtu ambaye ameachwa huru, anahama kila sehemu, halafu awe na uwezo wa kuuchezea mpira kama yule jamaa, imeniuma sana nilitaka leo nitoke na 'clean sheets' (bila kuruhusu bao) kwa sababu sijaipata kwa mechi nne nyuma, lakini leo pia imeshindikana," alisema Masalanga.

**Alisema Simba kwenye mechi hiyo hawakucheza kama walivyocheza dhidi ya Ihefu, badala yake walibadili mfumo kitu ambacho awali kiliwasumbua.**

"Sisi tulicheza mifumo miwili kwa nyakati tofauti, baada ya kuona hawachezi kama walivyocheza na Ihefu, leo walikuwa na Chama na hata mfumo wa uchezaji ulibadilika, ilibidi tubadilishe, lakini yote imegoma," alisema.

Alisema pamoja na kuumia kuruhusu 'hat-trick' ya nahodha, John Bocco, lakini amemsifu akisema ni straika mzuri mwenye uwezo wa kutumia nafasi, lakini akashauri kuwa awe anapewa mechi za mara kwa mara kwa dakika kadhaa badala ya kumuacha benchi kwa mechi nyingi, kwani hiyo itamsaidia kurejea kujiamini na kuwapa mashabiki kitu wanachohitaji.

Bocco alipiga 'hat-trick', Simba ikishinda mabao 4-0, ikiwa ni ya pili kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya Alhamisi iliyopita, Fiston Mayele kuweka rekodi ya kufunga 'hat-trick' ya kwanza msimu huu kwenye ligi, Yanga ikiifunga Singida Big Stars mabao 4-1, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Simba imefikisha jumla ya pointi 27 kwa michezo 12 iliyocheza, huku Ruvu Shoting ikiwa na pointi 11 kwa mechi 13 ambazo imecheza mpaka sasa.




Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja (kulia), akiwa na washiriki wa tamasha la michezo lililoandaliwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA), mwishoni mwa wiki katika Pori la Akiba Pande, Mabwepande jijini Dar es Salaaam. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# *Naibu Waziri anogesha tamasha la TAWA*

**Na Joseph Mwendapole**

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, ameongoza tamasha la michezo kutafuta fedha za kusaidia watu wenye ulemavu lililoandaliwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA) kwa kushirikiana na Dar Running Club.

Tamasha hilo lilifanyika jana katika Pori la Akiba Pande Mabwepande, Dar es Salaam ambapo mamia ya watu walishiriki kwenye michezo mbalimbali kuanzia asubuhi.

Baadhi ya michezo iliyokuwapo kwenye tamasha hilo maarufu kama Pande Train Run ni pamoja na mbio za Kilomita tano, 10, 15 na 33 ambazo zilishirikisha waendesha baiskeli na wakimbia kwa miguu.

Akizungumza baada ya kukamilika kwa mbio hizo, Naibu Waziri huyo alisema matamasha kama hayo ni muhimu kwani watu wanapata nafasi ya kushiriki michezo ambayo inawajenga kiafya.

Alisema serikali kupitia TAWA itajenga utamaduni wa kuendelea kuandaa matamasha kama hayo na kwamba lengo la tamasha hilo lilikuwa kuchangisha fedha kwa ajili ya watu wenye ulemavu.

Naibu Waziri alisema lengo la mbio hizo ni sehemu ya jitihada za serikali kuendelea kutangaza vivutio vya utalii na kuhamasisha wananchi kufanya utalii wa Ikolojia katika eneo zuri la kupumzika baada ya kazi.

"Kwa hiyo tunawaalika wananchi wote waje watembelee kivutio hiki kinachopatikana katika Jiji la Dar es Salaam na serikali itaendelea kuwekeza kwenye miundombinu katika Pori la Pande pamoja na kujenga maeneo ya burudani na michezo ya watoto," alisema.

Alisema sehemu ya mapato yatakayopatikana kwenye tamasha hilo yatatumika kuchangia fedha kwa ajili ya kuwanunulia vifaa vya mazoezi watoto wenye ulemavu walio chini ya uangalizi wa Asasi isiyo ya Kiserikali ya Africa Foundation For Inclusive Communities (AFIC), yenye ofisi zake Bunju B.

## Wanawake watakiwa kujitokeza michezoni

**Na Shufaa Lyimo**

MKURUGENZI wa Taasisi ya Binti Makini, Janeth John, amewataka wanawake kujitokeza kwa wingi kushiriki michezo mbalimbali ili kujenga afya na kuacha utamaduni wa kukaa mitaani.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Janeth, alisema amevutiwa kuona wasichana mbalimbali wakiwa wamejitokeza kushiriki Tamasha la Binti Makini lililofanyika hapo jana katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

"Ninawapongeza washiriki wote Wanawake ambao wameweza kuungana na sisi katika tamasha hili lenye lengo la kumuinua mwanamke na kumpa mbinu za kumfanya awe mbunifu," alisema Janeth.

Alisema kupitia tamasha hilo amegundua vipaji vingi vinavyofanywa na watoto wa kike ikiwamo mchezo wa mpira wa miguu, karate, ngumi, muziki nna mengineyo.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Lilian Liundi, aliipongeza taasisi hiyo kufanya tamasha ambalo limeshirikisha wadau mbalimbali ambalo lina lengo la kumwinua mwanamke.

## Lilian afyatua albamu mbili

**Na Sabato Kasika**

MWIMBAJI wa nyimbo za Injili, Lilian Naman, amezindua albamu mbili kwa mpigo, huku akisema kuwa huo ni mwendelezo wa kumtumikia Mungu kupitia nyimbo ambazo amekuwa akiziandaa.

Akizungumza katika uzinduzi huo uliofanyika jana katika Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Usharika wa Kinyerezi Dare es Salaam, alitaja majina ya albamu hizo kuwa ni 'Nishike Mkono na Upo Uwezekano'.

"Nishike Mkono nyimbo zake ni Asante Baba, Habadiliki, Mama Rita, Wanitosha na Yesu Ndiye Bwana Remix. Kwa upande wa Upo Uwezekano nyimbo zake ni Nikurudishie Nini, Kwa Baba, Hatuna Mji Udumuo, Tanzania Naipenda na Yesu Ndiye Bwana (remix2)," alisema.

Alifafanua kuwa 'Nishike Mkono' ni albamu ya pili na 'Upo Uwezekano' ni ya tatu, na kwamba alifyatua albamu ya kwanza mwaka 2016 yenye jina la 'Tumaini Limerudi' akiwa amemshirikisha Christina Shusho.

Alisema tangu mwaka huo alikuwa hajatoa albamu nyingine kutokana na kutingwa na majukumu mengine na sasa amekuja na albamu mbili kwa mpigo akiwa ameshirikisha waimbaji mbalimbali.

## ZISIKUPITE

### PICKFORD AFUATILIWA CHELSEA

CHELSEA itamfuatilia nyota wa Everton na England, Jordan Pickford, kwenye Kombe la Dunia huku mmiliki Todd Boehly akitafuta mlinda mlango mpya. ***(Sun on Sunday)***

### GARNACHO KUONGEZEWA NOTI

NYOTA wa Manchester United, Alejandro Garnacho, yuko mbioni kuongezewa mshahara mnono. Winga huyo wa Argentina mwenye umri wa miaka 18 anatarajiwa kulipwa pauni 50,000 kwa wiki. ***(Star)***

### SILVA AMSEMEA RONALDO

KIUNGO wa kati wa Manchester City, Bernardo Silva, amesisitiza kuwa kutoelewana kwa Cristiano Ronaldo na Manchester United si kikwazo katika kampeni ya Ureno ya Kombe la Dunia. ***(Guardian)***

### MBAPPE NA KUONDOKA PSG

KOCHA wa zamani wa Paris St-Germain, Mauricio Pochettino, amesema kwamba mshambuliaji Mfaransa Kylian Mbappe, 23, alitaka kuondoka katika klabu hiyo msimu uliopita ili kujiunga na Real Madrid. ***(Mirror)***

### CHELSEA YAMTAKA RONALDO

CHELSEA iko tayari kwa fursa iwapo Manchester United itatekeleza mpango wa kukatisha mkataba na Cristiano Ronaldo, 37 wa Ureno. ***(Sunday Mirror)***

### GILMOUR KUIKIMBIA BRIGHTON

KIUNGO wa kati wa Brighton na Scotland, Billy Gilmour yuko tayari kuhamia klabu moja ya Ulaya kwa mkopo baada ya kukosa nafasi ya kucheza tangu ajiunge na klabu hiyo. ***(Sun on Sunday)***

### BAILEY KUTUA CHELSEA

CHELSEA inafikiria kumnunua winga wa Aston Villa, Mjamaika Leon Bailey, 25, ambaye ni rafiki mkubwa wa kiungo, Raheem Sterling. ***(Mail on Sunday)***

### ENDRICK ATAKIWA ULAYA

BABA wa nyota wa Brazil, Endrick anadai kuwa ni klabu moja tu ya Ulaya ambayo imefungua rasmi mazungumzo na Palmeiras kuhusu mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 16, ingawa hawezi kuhama hadi atakapofikisha umri wa miaka 18. ***(90Min)***

### MESSI NA GUARDIOLA

MSHAMBULIAJI wa Paris St-Germain, Lionel Messi, 35, anaweza kuungana na kocha wake wa zamani, Pep Guardiola katika Klabu ya Manchester City ikiwa atashindwa kutwaa Kombe la Dunia lililoanza jana nchini Qatar. ***(El Nacional)***

### KLOPP AMSIFIA TUCHEL

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amefichua kwamba aliondoka Borussia Dortmund mapema kuliko ilivyopangwa ili kuisaidia klabu hiyo ya Ujerumani kumpata Thomas Tuchel kama mrithi wake. ***(Mirror)***

### MASKAUTI UNITED WAKUTANA

TAKRIBAN maskauti 35 wa Manchester United kutoka duniani kote wamekutana mjini Manchester katika mfululizo wa mikutano ya usajili ili kuwa na mbinu ya pamoja zaidi katika usajili. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# BENZEMA SASA ALIKOSA RASMI KOMBE LA DUNIA

**Amejiondoa kutokana na jeraha la paja, timu nzima inashiriki masikitiko haya na...**

**DOHA,** Qatar

KARIM Benzema atakosa michuano ya Kombe la Dunia baada ya mshambuliaji huyo wa Ufaransa kupata pigo la kuumia usiku wa juzi.

**Nahodha huyo wa Real Madrid, ambaye alikosa ushindi wa 'Les Bleus' kule Urusi mwaka 2018, alikuwa na jukumu kubwa wakati huu kwa timu ya Kocha Didier Deschamps.**

Benzema alishinda tuzo ya Ballon d'Or mwezi uliopita baada ya msimu mzuri wa 2021-22 na kufunga mabao 44 katika mechi 46 alizoichezea Madrid, akiwasaidia wababe hao wa Hispania kushinda LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Hata hivyo, amekuwa akisumbuliwa na matatizo ya kimwili muhula huu na pigo kubwa zaidi ambalo halikutarajiwa na kubwa zaidi kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, lilikuja siku moja kabla ya Kombe la Dunia kuanza.

Benzema alianza tena mazoezi kamili akiwa na Ufaransa Jumamosi, baada ya matatizo ya misuli hivi majuzi, lakini hakuweza kukamilisha kipindi cha mazoezi na kutokana na jeraha.

Alifanyiwa vipimo vilivyotoa matokeo yaliyomfanya akose kushiriki michuano hiyo.

Shirikisho la Soka la Ufaransa lilisema katika taarifa yake: "Karim Benzema amejiondoa kwenye Kombe la Dunia kutokana na jeraha la paja. Timu nzima inashiriki masikitiko ya Karim na inamtakia ahueni ya haraka."

Mchezaji huyo wa zamani wa Lyon alitatizwa na pigo la goti mapema msimu huu kabla ya kukosa mechi zaidi za Madrid baada ya kusumbuliwa na misuli kwenye sehemu zake za chini za mguu wa kushoto, huku pigo la Jumamosi likionekana kujirudia.

Mabingwa watetezi wa Kombe la Dunia, Ufaransa wataanza michuano hiyo kesho, Jumanne dhidi ya Australia, kabla ya kumenyana na Denmark na Tunisia katika Kundi D.

Kukosekana kwa Benzema kwenye michuano hiyo ndio msururu wa vikwazo vikubwa kwa Ufaransa, ingawa Kocha Deschamps pia ana makinda Kylian Mbappe, Antoine Griezmann na Olivier Giroud kama chaguo la washambuliaji.

Mchezaji mahiri wa RB Leipzig, Christopher Nkunku alilazimika kujiondoa kwenye kikosi wiki hii baada ya kuumia goti katika mechi ya mazoezi.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 407

MECHI KALI
ENGLAND
VERSUS
IRAN
1 | 1.40
X | 4.08
2 | 9.11

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MANCINI AIPA ARGENTINA KOMBE LA DUNIA QATAR



**ROME,** Italia

KOCHA Roberto Mancini amedokeza Argentina kutwaa Kombe lao la tatu la Dunia huku Lionel Messi na wachezaji wenzake waking'ara Qatar.

Kikosi cha Mancini cha Italia hakitahusika baada ya kichapo cha kushtukiza cha bao 1-0 dhidi ya Macedonia Kaskazini, Machi mwaka huu.

Kukosekana kwa Italia nchini Qatar kunakuja licha ya wao kuwa mabingwa watetezi wa Ulaya, baada ya kuifunga England kwa mikwaju ya penalti katika fainali ya Euro 2020.

Ushindi huo baadaye uliwafanya wakabiliane na Argentina katika Fainali ya UEFA/CONMEBOL Uwanja wa Wembley Juni, baada ya vijana wa kocha Lionel Scaloni kushinda Copa America. Argentina iliishinda Italia 3-0 kwa raha, na Mancini amesema kwamba uchezaji unachangia katika kuwapanga kama wachezaji wanaopendekezwa kwa Kombe la Dunia.

"Kuna timu nyingi zenye nguvu," Mancini aliwaambia waandishi wa habari. "Ikiwa ningehitaji kuchagua moja, ningeenda Argentina. "Walivutia sana tulipocheza."

Mancini bado anasikitishwa na kushindwa kufika Qatar, lakini amefurahishwa na majibu ya timu yake, akisema: "Tulionyesha nia ya kupambana mara moja, kushinda kundi la Ligi ya Mataifa ya Uefa ambayo haikuwa rahisi kwa Ujerumani, Hungary na Ujerumani.



# Infantino atema nyongo Qatar

**DOHA,** Qatar

RAIS wa Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), Gianni Infantino, amezishutumu nchi za Magharibi kwa "unafiki" katika ripoti yake kuhusu rekodi ya haki za binadamu ya Qatar katika mkesha wa Kombe la Dunia.

Katika mkutano na waandishi wa habari huko Doha, Infantino alizungumza kwa karibu saa moja na kutoa ulinzi mkali wa Qatar na mashindano hayo.

Michuano hiyo imegubikwa na masuala mengi nchini Qatar ikiwa ni pamoja na vifo vya wafanyakazi, wahamiaji na matibabu.

Infantino alifunguka kwa kusema: "Leo nina hisia kali. Leo ninahisi Qatar, nahisi Mwarabu, nahisi Mwafrika, nahisi mlemavu, nahisi mfanyakazi na mhamiaji."

Wenyeji Qatar jana walianza mchujo dhidi ya Ecuador katika Uwanja wa Al Bayt Jumapili katika mechi ya ufunguzi.

Februari 2021, gazeti la Guardian lilisema wafanyakazi wahamiaji 6,500 kutoka India, Pakistan, Nepal, Bangladesh na Sri Lanka walikufa nchini Qatar tangu iliposhinda zabuni yake ya Kombe la Dunia.

Idadi hiyo inatokana na takwimu zilizotolewa na balozi z
nchi hizo nchini Qatar.

Hata hivyo, Serikali ya Qata
ilisema jumla ilikuwa ya kupo
tosha, kwa sababu si vifo vyot
vilivyorekodiwa ni vya wat
wanaofanya kazi katika mirad
inayohusiana na Kombe la Du
nia.

Infantino alisema: "Tum
fundishwa masomo meng
kutoka kwa Wazungu n
ulimwengu wa Magharib
Mimi ni Mzungu. Kwa kile an
bacho tumekuwa tukifany
kwa miaka 3,000 duniani kot
tunapaswa kuomba msamah
kwa miaka 3,000 ijayo kabla y
kutoa masomo ya maadili.

,110,340

# JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01.22/11/22 | 19:00 | Mexico vs Poland | 2.74 | 2.99 | 2.69 |
| 02.22/11/22 | 22:00 | Forest Green vs Cheltenham | 2.30 | 3.60 | 2.58 |
| 03.22/11/22 | 22:30 | Grimsby vs Accrington | 2.65 | 3.80 | 2.38 |
| 04.22/11/22 | 22:30 | Salford City vs Bradford City | 2.42 | 3.65 | 2.42 |
| 05.22/11/22 | 22:45 | Crawley Town vs Gillingham | 2.37 | 3.11 | 2.97 |
| 06.22/11/22 | 22:45 | Linfield Belfast vs Larne | 2.84 | 3.28 | 2.37 |
| 07.22/11/22 | 22:45 | AFC Wimbledon vs Sutton United | 2.42 | 3.65 | 2.42 |
| 08.23/11/22 | 02:30 | Deportivo Pasto vs America De Cali | 2.61 | 2.94 | 2.65 |
| 09.23/11/22 | 18:00 | Farco FC vs Ismaily SC | 2.93 | 2.68 | 2.78 |
| 10.23/11/22 | 22:30 | Port Vale vs Barnsley | 2.45 | 3.53 | 2.45 |
| 11.23/11/22 | 22:30 | Colchester vs Bristol Rovers | 2.79 | 3.79 | 2.28 |
| 12.23/11/22 | 13:00 | Wales vs Iran | 2.31 | 3.00 | 3.30 |
| 13.23/11/22 | 16:00 | Qatar vs Senegal | 3.49 | 3.19 | 2.22 |

# RAIS ATUNUKIWA TUZO YA UONGOZI WA KIMAGEUZI

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan ametunukiwa Tuzo ya Uongozi wa Kimageuzi (Transformation Leadership Award), kwa kutambua mchango wake kwenye sekta za sanaa na utamaduni.

**Tuzo hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki jijini Dallas, Marekani na Taasisi ya Afrimma, ambao wameeleza sababu za kumtunukia ni pamoja na kurejesha tuzo za muziki, kuwasaidia kukua kiuchumi na kurekodi Filamu ya Royal Tour kwa siku nane.**

Waandaaji wa tuzo hizo za muziki zinatolewa na Diaspora wa Afrika walioko nchini Marekani katika mawanda ya sanaa na mara chache, pia inatolewa kwa kiongozi wa kisiasa anayeleta mageuzi katika sanaa barani Afrika.

Kwa mujibu wa taarifa ya viongozi wa Afrimma iliyotolewa Texas, Marekani, jopo la wachambuzi hao wameona kazi iliyofanywa na Rais Samia kurejesha tuzo kwa wasanii zilizokuwa zimekufa kwa miaka mingi ni hatua kubwa miongoni mwa viongozi wengine wa Afrika kwa mwaka huu.

Rais Samia anakuwa wa tatu Afrika na Kiongozi wa Juu wa Kwanza Mwanamke Afrika kushinda Tuzo hiyo baada ya mwaka 2015 kutolewa kwa aliyekuwa Rais wa Botswana, Luteni General Dk. Seretse Khama Ian Khama na mwaka 2017 alipewa aliyekuwa Rais wa Nigeria, Olusegun Obasanjo.

Tuzo hiyo ilipokelewa jana na Katibu Mkuu Wizara ya Sanaa, Utamaduni na Michezo, Dk. Hassan Abbas, na kuwaomba walioshiri kumwombea Rais Samia ili azidi kuleta mageuzi kwenye sekta hizo adhimu.

"Ni kiongozi wa mfano, alitumia siku nane nje ya ofisi kutengeneza Filamu ya The Royal Tour, iliyoandaliwa na CBS Travel Editor, Peter Greenberg. Alicheza nafasi ya mwongoza watalii kuonyesha dunia vivutio vilivyoko Tanzania. Ametengeneza sera zenye maana na kuonyesha upendo mkubwa kwenye sanaa," ilisema taarifa ya AFRIMMA iliyotolewa jana.

# MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMATATU - 21/11/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 3705 | FC Ingulets vs FK Lviv | 2.31 | 3.15 | 2.86 |
| 14:00 | 1469 | Hebei Zhongji vs Changchun Yatai | 29.08 | 13.57 | 1.01 |
| 14:00 | 1763 | Aizawl FC vs Sudeva Delhi FC | 2.04 | 3.21 | 3.35 |
| 14:00 | 2885 | Tianjin Teda vs Shanghai Shenhua | 2.25 | 3.26 | 2.87 |
| 14:00 | 3989 | Tanzania Prisons vs Kagera Sugar | 2.22 | 2.82 | 3.40 |
| 14:30 | 2183 | Chengdu Qianbao vs Shandong Luneng | 5.25 | 3.99 | 1.52 |
| 14:30 | 2235 | Wuhan Three Towns FC vs Meizhou Kejia | 1.36 | 4.48 | 7.01 |
| 14:30 | 5909 | Guangzhou RF vs Beijing Guoan | 8.74 | 4.86 | 1.28 |
| 15:00 | 1120 | Veres Rivne vs Dynamo Kiev | 6.81 | 4.47 | 1.37 |
| 15:00 | 1386 | Chiangmai United vs Rayong FC | 1.91 | 3.16 | 3.84 |
| 16:00 | 1334 | Yarmouk vs Kazma SC | 4.38 | 3.51 | 1.70 |
| 16:00 | 2787 | Panathinaikos B vs Almopos Arideas | 1.58 | 3.45 | 5.63 |
| 16:00 | 4048 | Anagennisi Karditsas vs Iraklis Larisas | 1.24 | 5.06 | 10.71 |
| 16:00 | 4934 | Burgan SC vs Khaitan SC | 3.98 | 3.40 | 1.80 |
| 16:00 | 5566 | Mtibwa Sugar vs Polisi Tanzania | 2.06 | 2.91 | 3.69 |
| 16:00 | 5722 | England vs Iran | 1.40 | 4.08 | 9.11 |
| 16:00 | 5741 | AS Kigali vs Rwamagana City FC | 1.26 | 4.69 | 10.74 |
| 16:30 | 3984 | Tiddim Road Athletic Club vs Kenkre FC | 1.49 | 3.84 | 6.02 |
| 16:45 | 2796 | Poland U21 vs Turkey U21 | 2.57 | 3.25 | 2.48 |
| 17:00 | 1584 | JS Bordj Menaiel vs CA Batna | 1.57 | 3.49 | 5.63 |
| 17:00 | 3785 | MO Constantine vs Ain M'lila | 1.54 | 3.59 | 5.81 |
| 17:00 | 5559 | Georgia U21 vs Ukraine U21 | 2.87 | 3.50 | 2.15 |
| 18:35 | 3376 | Al Fehaheel vs Al Salmiyah | 2.83 | 3.27 | 2.27 |
| 18:35 | 5270 | Al Kuwait SC vs AL Qadsia | 1.84 | 3.60 | 3.60 |
| 19:00 | 2170 | Senegal vs Netherlands | 6.18 | 3.89 | 1.54 |
| 19:00 | 3917 | Asi D Abengourou vs Societe Omnisport | 3.65 | 2.80 | 2.26 |
| 19:30 | 2729 | Slovenia U21 vs Bulgaria U21 | 1.80 | 3.60 | 3.75 |
| 20:00 | 3217 | Altay vs Genclerbirligi | 2.42 | 3.07 | 2.78 |
| 20:00 | 5490 | Croatia U21 vs Austria U21 | 2.01 | 3.55 | 3.11 |
| 21:30 | 1163 | Waasland Beveren U21 vs Excelsior Virton U21 | 1.76 | 4.19 | 3.41 |
| 21:30 | 1538 | St Truiden U21 vs Oostende U21 | 3.06 | 3.59 | 2.02 |
| 22:00 | 1631 | Westerlo U21 vs FCV Dender EH U21 | 2.05 | 3.89 | 2.82 |
| 22:00 | 3360 | RWD Molenbeek U21 vs Lierse SK U21 | 3.21 | 3.99 | 1.86 |
| 22:00 | 3527 | Kmsk Deinze U21 vs AS Eupen U21 | 6.43 | 5.26 | 1.33 |
| 22:00 | 4717 | USA vs Wales | 2.51 | 2.96 | 3.01 |
| 22:30 | 4062 | Torre Neapolis vs Pescara Calcio | 3.14 | 3.34 | 2.21 |
| 22:45 | 1320 | Beaconsfield Sycob vs Metropolitan Police | 2.27 | 3.82 | 2.52 |
| 22:45 | 4825 | Hitchin Town vs Rushden and Diamonds | 2.00 | 3.50 | 3.50 |
| 23:00 | 1933 | Mirandes vs FC Cartagena | 2.76 | 3.05 | 2.56 |

## JUMANNE - 22/11/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01:00 | 3800 | Waterhouse FC vs Chapelton Maroons FC | 1.18 | 6.21 | 10.67 |
| 04:00 | 3897 | Chico vs Atletico Huila | 1.56 | 3.56 | 5.65 |
| 11:30 | 3388 | Real Kashmir vs Gokulam Kerala FC | 3.22 | 3.17 | 2.11 |
| 13:00 | 4302 | Argentina vs Saudi Arabia | 1.16 | 6.79 | 16.97 |
| 14:00 | 2033 | Shijiazhuang vs Dalian Aerbing | 2.27 | 3.36 | 2.77 |
| 14:30 | 1137 | Shenzhen vs Guangzhou Evergrande | 2.04 | 3.31 | 3.26 |
| 14:30 | 4488 | Henan Jianye vs Wuhan Zall | 1.31 | 4.86 | 7.58 |
| 14:30 | 5369 | Hangzhou NG vs Shanghai SIPG | 4.68 | 4.00 | 1.57 |
| 15:00 | 3264 | Ural Yekaterinburg vs CSKA Moscow | 3.16 | 3.45 | 2.03 |
| 16:00 | 3505 | Denmark vs Tunisia | 1.46 | 4.09 | 7.18 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Nabi: Nimeisoma vizuri Dodoma Jiji

INATOKA UKURASA 32

wapinzani wetu katika mechi yao ya mwisho kabla ya kukutana nao," alisema Nabi.

Alisema ligi imekuwa ngumu kwa kila timu kuonyesha ushindani mkubwa na kwa sababu ya kuwapo kwa muda mchache wa maandalizi wanalazimika kutumia muda mwingine kuwaandaa zaidi wachezaji kisaikolojia.

Yanga ambayo imeshuka dimbani mara 10 hadi sasa msimu huu, inashika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa pointi 26 moja nyuma ya Simba iliyopo kileleni baada ya kucheza mechi 12.




Mshindi wa Jackpot Bonus, Jeremia Wilfred Mwita, akionyesha mfano wa hundi ya Sh. milioni 4.1 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot ya SportPesa wiki iliyopita. Supa Jackpot kwa wiki hii ni Sh. 1,051,207,683. **MPIGAPICHA WETU**



# Bocco afunguka hat-trick

INATOKA UKURASA 32

kucheza kwa kiwango bora kwa dakika zote 90 inategemea na ushindani wa wapinzani katika soka kupanda na kushuka ni sehemu ya pili," alisema kocha huyo.

Alisema mabadiliko ya beki wa kati, Henock Inonga yalikuwa ya kawaida, walipanga kumpumzisha kwa sababu ya kutopata muda wa kupumzika kwa muda mrefu.

Kuhusu kurejea kwa Chama, Mgunda alisema mchezaji mzuri akifanya vizuri ni wajibu wake na yuko katika majukumu ya kazi na amekuwa muhimu kwa sababu ya kuchagiza ushindi huo.

"Kila mchezaji ndani ya Simba ana umuhimu na kuhitaji kuleta mchango katika timu, Chama ni mchezaji mzuri ila uzuri huchagizwa kwa wengine waliokuwapo ndani ya kikosi," alisema Kocha huyo.

Kocha Mkuu wa Ruvu Shooting, Boniface Mkwassa, aliwapongeza Simba kwa ushindi huo na kukiri kuzidiwa katika mipango yake.

Alisema Simba walitumia makosa waliyoyafanya mabeki wake kupata ushindi, na walitawala mpira kwa sababu walizembea kuziba nafasi.

"Tumeruhusu Simba kutawala mpira na makosa ya beki wangu, nikiri wapinzani wetu walitawala mpira tumeingia na mipango kwa kuona mechi mbili zilizopita. Tumezembea kuziba nafasi walizopata tunajisahau kuziba na Simba kuzitumia," alisema Mkwassa.

Michezo
Jumatatu Novemba 21, 2022
Nipashe



Benzema alikosa rasmi Kombe la Dunia UKURASA 29

# BOCCO AFUNGUKA HAT-TRICK, MGUNDA ATOA SIRI KUWIKA

●●● Amtaja pia Chama, huku Mkwasa akikiri 'maji ya shingo'...

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

WAKATI mshambuliaji na nahodha wa Simba, John Bocco, akielezea na kufurahia kurejea uwanjani kwa kuifungia timu yake mabao matatu (hat-trick) wakati ikishinda 4-0 kwenye mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Ruvu Shooting juzi, Kaimu Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Juma Mgunda ametoa siri ya ushindi huo.

**Bocco ambaye alikuwa majeruhi kwa muda mrefu, alirejea katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na kufunga hat--trick, huku bao la nne katika mchezo huo likifungwa na Shomari Kapombe, shukrani kwa Clatous Chama aliyekuwa mpishi mkuu wa ushindi huo.**

Akizungumza na gazeti hili baada ya mchezo huo Bocco alisema ataendelea kupambana ili kuipa mafanikio timu yake hiyo na kwa ushirikiano mkubwa na wachezaji wenzake anaamini hilo linawezekana.

"Nitaendelea kupambana nikishirikiana na nguvu za wachezaji wenzangu, tuipe ushindi timu yetu," alisema Bocco.

Alisema Ligi msimu huu ina ushindani kila timu imejipanga vizuri kutokana na ongezeko la wadhamini.

"Wadhamini waliopo kipindi hiki wamefanya ligi yetu iwe na ushindani kila timu haikubali kupoteza mchezo kirahisi," alisema.

Kwa upande wa Kaimu Kocha Mkuu, Mgunda, yeye alifichua siri ya ushindi katika mchezo huo kuwa umetokana na kuingia na mikakati tofauti na michezo iliyopita.

Mgunda alisema kila mmoja kwa nafasi yake ametimiza majukumu yake kwa ufasaha na hilo ndio lililosababisha ushindi mnono ulioleta furaha kwa Wanasimba wote.

Alisema hadi kupata pointi tatu hizo kwanza kumetokana na wachezaji kufanya kazi kubwa na kufuata vizuri maelekezo waliyopewa.

"Namshukuru Mungu tumefanikiwa kupata ushindi mnono , huu umetokana na mshikamano kutoka kwa benchi la ufundi, wachezaji na mashabiki waliokuja kutupa sapoti hapa uwanjani.

"Kwenye mpira wa miguu kuna kipindi unakuwa bora wakati mwingine inakuwa tofauti kwa hiyo, mashabiki wanapaswa kukubali nyakati zote," alisema Mgunda.

Alisema timu yake kuonyesha kiwango kizuri na kumudu kwa kiwango bora inategemea na ushindani wa mpinzani wake na kuingia na mipango tofauti na mechi zilizopita.

"Tumecheza vizuri nawapongeza wachezaji wangu,

INAENDELEA UK. 31



## Nabi: Nimeisoma vizuri Dodoma Jiji

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuwasoma kwa dakika 90 Dodoma jiji FC, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema wanapaswa kuingia kwa tahadhari kubwa katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi yao, utakaopigwa kesho katika Uwanja wa Liti mkoani Singida.

Yanga imeondoka jana alfajiri kuelekea Singida kwa ajili ya mchezo huo, na Nabi ameeleza alifanikiwa kuwasoma Dodoma jiji FC Jumanne iliyopita wakati 'Wakulima wa Zabibu' hao wakicheza dhidi ya KMC FC katika Uwanja wa Uhuru Dar es Salaam na kukubali kipigo cha mabao 2-1.

Kocha huyo pamoja na msaidizi wake, Cedric Kaze, walionekana katika mchezo huo wakisoma mbinu, ubora na madhaifu ya wapinzani wao, jambo ambalo ameliambia Nipashe kuwa tayari wazifanyia kazi.



Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi, alisema baada ya ushindi mnono dhidi ya Singida Big Stars walirudi uwanja wa mazoezi kufanyia kazi mbinu za wapinzani wao hao kuelekea mechi hiyo ya kesho.

"Wachezaji wanatambua kila mechi kwetu ni fainali na kutakiwa kucheza kwa tahadhari kubwa kwa sababu hakuna timu nyepesi katika ligi, ukizingatia tuliwaona

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >